

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi – Tarehe 8 Februari, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2018/2019 *(Statement of Re-allocation Warrant No. 1 between Votes for the First Half of 2018/2019).*

Hati ya Uhamiaji Fedha Na. 2 kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2018/2019 *(Statement of Re-allocation Warrant No. 2 between Votes for the First Half of 2018/2019).*

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha, Mapitio ya Nusu Mwaka 2018/2019 *(The Monetary Policy Statement, The Mid-year Review for the Year 2018/2019).*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA - K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO (MHE.
ANDREW J. CHENGE):**

Taarifa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tunaanza na maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Leah Jeremiah, Komanya.

Na. 109

**Mkakati wa EQUIP wa Kuinua Elimu
kwa Watoto wa Kike**

NHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Moja ya mkakati wa *EQUIP*– Tanzania ni kuinua ubora wa elimu inayotolewa kwa watoto wa kike ili waweze kuhitimu Shule ya Msingi na kuendelea na Sekondari, lakini mtoto wa kike ana vikwazo vinavyoweza kukatiza ndoto hii:-

(a) Je, mpango huu umejikita vipi katika kutokomeza mimba na ndoto za utotoni, udhalilishaji kingono, ukeketaji na masuala ya adhabu zenye kudhuru mwili na akili za watoto?

(b) Je, ni upi usaidizi wa mpango wa wanafunzi walio katika hatari zaidi kwa makundi kama vile waliotelekezwa, walio katika umasikini wa kupindukia, yatima na walionusurika kutokana na unyanyasaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, udhalilishaji kongono na ukeketaji, Serikali kupitia programu ya *EQIP Tanzania* imeanzisha *clubs* za wanafunzi zilitwazo Jiamini Uwezo Unao (JUU) kwenye Shule za Msingi 4,476. Malengo ya *clubs* hizo ni kuwajengea wanafunzi hasa wa kike uwezo wa kujiamini, kujieleza na kujitambua. Kupitia *clubs* hizo, wanafunzi wanajifunza masuala mbalimbali ikiwemo hedhi salama na athari za kupata mimba katika umri mdogo.

Aidha, ili kuboresha mazingira ya watoto wa kike, mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kwa kupitia programu hii ilitoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 2.46 kwenye shule 4,476 ambazo kila shule ilipewa shilingi 550,000/=. Kupitia ruzuku hiyo, elimu ilitolewa kwa wanafunzi wa kike na wazazi kupitia ushirikiano wa Wazazi na Waalimu (UWAWA), kuhusu namna ya kutengeneza taalo salama za kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali kupitia programu ya *EQUIP Tanzania* imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kutoa elimu na kuhamasisha jamii wakiwemo wanafunzi, wazazi na Walimu kupiga vita vitendo vya ukatili kwa watoto na kujenga mazingira rafiki ya kujifunzia kwa makundi maalum wakiwemo watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia programu ya *EQUIP Tanzania*, Serikali imeongeza fursa ya kujifunza kwa watoto wa kike sawa na wa kiume na kuwakinga na masuala ya adhabu zenye kudhuru mwili na akili za watoto. Jumla ya shilingi bilioni 6.8 zimetumika kuwajengea uwezo Walimu 50,446 kuhusu mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji ikiwemo matumizi ya mbinu zinazojali jinsia na ujenzi wa mazingira rafiki na salama ya kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huo umeboresha mbinu rafiki na zinazozingatia jinsia katika ufundishaji na ujifunzaji kutoka asilimia 54 mwaka 2014 hadi asilimia 65 mwaka 2016 katika shule zilizo katika Mikoa iliyotekeleza programu hiyo ya *EQUIP Tanzania*. Tathimini inaonesha kuwa wasichana waliopata wastani wa juu katika kumudu stadi za kusoma na kuandika, walifikia asilimia 26.7 ikilinganishwa na wavulana asilimia 18 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Leah.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa fedha za mafunzo zimekuwa zikibaki kila mwaka kutokana na wawezeshaji kutoka Vyuho vikuu Vya Tanzania; fedha hizo zimekuwa zikibaki kwa sababu wakati wa kutekeleza, wawezeshaji kutoka Vyuho Vikuu wamekuwa na programu nyingine katika vyuo vyao. Je, Serikali haioni ipo haja ya kutengeneza *TOT* wa Mkoa ili hata kama mradi utakapokwisha wanafunzi waendeleo kupewa mafunzo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mimba katika Mkoa wa Simiyu bado ni kubwa. Kwa mwaka 2017 wanafunzi 37 wa Shule za Msingi walipata ujauzito; 2018 wanafunzi 38; halikadhalika katika Sekondari kwa mwaka 2017 wanafunzi 159 walipata ujauzito; na mwaka 2018 wanafunzi 153.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchungu huo mkubwa wananchi waliamua kuanzisha ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Mwanjoro: Je, Serikali ipo tayari kuunga nguvu za wananchi waliofikisha jengo usawa wa boma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Leah Komanya kwa kuendelea kutaka watoto wa kike wapate elimu nzuri na juhudi hizi za kuunga mkono Serikali ambazo imeziweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza anasema kuna fedha zinabaki kwenye programu hii. Ni kweli katika mazingira mbalimbali fedha inaweza kubaki, lakini maelekezo ya Serikali ni kwamba fedha ikibaki, wahusika wanapewa taarifa kwenye Wizara na inapangiwa majukumu mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo Mheshimiwa Mbunge aliyotoa ni mazuri, tuyapokee; kuandaa *TOT* ili programu itakapoisha wawezeshwe watu wa eneo husika kwani itapunguza gharama, wenyewe kwa wenyewe watafundishana kwa lugha zao za nyumbani, hii kazi itaenda vizuri. Kwa hiyo, tunapokea wazo hili, tunalifanyia kazi. Ni wazo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anazungumza habari ya mimba na kuunga mkono juhudi za kujenga mabweni. Utakumbuka tangu juzi mpaka jana kumekuwa na mjadala katika Bunge hili Tukufu la kumaliza maboma ya madarasa lakini pia na mabweni na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba kazi hii inatekelezwa na Serikali inaunga mkono juhudi za wananchi, tunafanya mpango, tukipata fedha tutaweka nguvu katika maeneo hayo. Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa ambayo imepewa miradi mingi ya kuwezesha watoto wa kike wasome, kujenga madarasa, matundu ya vyoo na mabweni. Jambo hili tunalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika programu ijayo, fedha ikipatikana tutatoka hapa kuunga mkono nguvu za wananchi katika kumaliza mabweni ambayo wananchi wamechangia wenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimba za watoto mashuleni ni jambo la aibu kweli kweli; nasi kama wazazi lazima tulichukulie *very serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tulivyoanza programu ya kujenga madarasa ya Shule za Kata, tukajenga mabweni, ni kwa nini Serikali isiagize Halmashauri kwa makusudi kabisa kwamba ni lazima katika Halmashauri bajeti itengwe ili mabweni yajengwe, lisiwe ni suala la hiari? Kwa sababu hawa watoto wanapata mimba kutokana na bodaboda, kutokana na njaa, watoto wamechoka kwa sababu ya umbali wa shule; kwa nini Serikali isiamue kabisa kwamba mwaka huu wa fedha kila Halmashauri ihakikishe angalau wamejenga mabweni mawili au matatu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli kwamba jambo la kujenga mabweni na hasa ya watoto wa kike ni jambo ambalo haliepukiki, ni jambo la lazima na naomba pia tulizingatie. Ndiyo maana kwenye miradi mbalimbali ya Serikali, kwa

mfano mradi wa *EP4R* tumeshajenga mabweni 533 katika shule zote za Sekondari katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu hoja ni kwamba tutenge fedha kwenye bajeti hii, Mheshimiwa Mbunge ni Mbunge; na Waheshimiwa Wabunge wote nawaomba sana, wakati huu ndiyo tunaandaa bajeti zetu za Halmashauri. Kila Halmashauri ina maelekezo mahususi ya Serikali, asilimia 40 au 60 kulingana na mapato ya Halmashauri inaenda kwenye shughuli za maendeleo na hasa miundombinu ikiwepo mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwenye bajeti ambazo zinaandaliwa sasa, hiki kipengele tumetoa maelekezo, Serikali ngazi ya juu ya Taifa tunapanga fedha, Halmashauri zitenge fedha. Wakuu wa Mikoa wameelekezwa, tunapozungumza maboma ni pamoja na madarasa na mabweni haya. Nasi tunapanga, Waheshimiwa Wabunge mtusaidie, tunalisimamia hilo. Kwenye ziara zangu zote, katika maeneo mbalimbali tunazingatia kukagua hosteli ambazo zinajengwa na wananchi, wadau mbalimbali na Serikali Kuu.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Fakharia Shomar.

Na. 110

Mikakati ya Kukubaliana na Rushwa Nchini

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Rushwa ni adui mkubwa wa haki. Aidha, rushwa ikishamiri husababisha athari hasi kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiteknolojia na hivyo kuchangia ongezeko la umasikini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinusuru Taifa dhidi ya Rushwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba rushwa ni adui wa haki, kwani ni kikwazo katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua athari za rushwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini, Serikali imeandaa kutekeleza mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa na mpango wa utekelezaji Awamu ya Tatu kwa maana ya NACCSAP III ule wa mwaka 2017 hadi 2022.

Mkakati huu unalenga kuzuia na kupambana na rushwa katika Sekta za uchumi za kimkakati zenye mazingira shawishi ya rushwa ambazo ni manunuzi ya Umma, ukusanyaji wa mapato, uvunaji na matumizi ya maliasili, madini, nishati, mafuta na gesi, utawala, vyombo vya utoaji wa haki na shughuli za Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya mkakati huu ni kuimarisha na kuboresha mifumo ya utawala ya vyombo vya utoaji wa haki, kuimarisha elimu ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa na kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za Umma na vilevile za binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba wala rushwa na wahujumu uchumi wanachukuliwa hatua za kisheria, Sheria ya Uhujumu Uchumi ile Sura ya 200 imefanyiwa marekebisha kupitia Sheria ya Marekebisha ya Sheria Mbalimbali Na.3 ya Mwaka 2016 kwa kurekebisha vifungu kadhaa kwa kupanua wigo na kuongeza makosa ya uhujumu uchumi pamoja na kuanzisha *Division* ya Mahakama ya Ufisadi

na Uhujumu Uchumi katika muundo wa Mahakama Kuu na Mahakama hii imeshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya rushwa yameonesha mafanikio ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa kitengo cha urejeshaji mali chini ya TAKUKURU kwa ajili ya urejeshaji mali zilizopatikana kwa njia za rushwa kwa maana ya *Asset Tracing and Recovery Unit*. Kupitia kitengo hiki, Serikali imefanikiwa kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 127.9 na kutaifisha au kuzuia akaunti za fedha zenye shilingi bilioni 4.5. Kesi 1,340 zimefunguliwa Mahakamani na Serikali imeshinda kesi 685.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, miradi ya maendeleo 899 yenye thamani ya shilingi 1,642,522,950,825.10 ilifuatiliwa ambapo miradi ipatayo 111 yenye thamani ya shilingi bilioni 23,256,624,083.40 iligundulika kuwa na kasoro au kufanyiwa ubadhirifu. Hivyo, uchunguzi unafanyika na upo katika hatua tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri, amenijibu vizuri na ametoa faida kwa Watanzania katika kuona Serikali imeishupalia rushwa ili iwe mfano kwa wengine. Nina maswali mawili madogo ambayo ningetaka pia anipatie ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mtoa rushwa na mpokea rushwa ni tendo la siri kubwa ingawa wote kisheria wana. Je, ni jambo lipi na wanalithibitishaje? Kitu kinachofanyika kwa siri wanawezaje kukijua wakati kitendo hiki hakifaywi hadharani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ziko za aina mbalimbali, mojawapo ni rushwa ya ngono na hii pia imejificha, kuitambua siyo rahisi, inataka mbinu kubwa: Je,

atawasaidia vipi vijana wetu kubaini mbinu hii ya rushwa ya ngono ili kabla ya tatizo hili halijawafika wakaweza kuliabini? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwenda. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa jinsi ambavyo amekuwa ni sehemu ya wapambanaji katika mapambano haya dhidi ya rushwa. La kwanza, anazungumzia suala la kukamatwa kwa hawa wala rushwa na anasema kabisa tuna uhakika gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba katika ile Sheria Na. 11 ya mwaka 2007 ina makosa 24, lakini katika kile kifungu cha 15 kinazungumzia suala la hongo, nasi kama TAKUKURU tutamkamata mtu kama tukiwa na ushahidi katika suala zima la kile kitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linategemea na *circumstantial evidence*, inategemea na mazingira; nasi sote humu ndani ni wanasiasa. Kwa hiyo, mfano katika ile Sheria ya Uchaguzi, mambo mengi huwa yanatokea na sote humu ndani tunaelewa. Kwa hiyo, hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kuhusu ngono ya rushwa, naomba niseme kwamba hili limekuwa ni tatizo, kubwa ngono ya rushwa iko katika kifungu Na. 25. Ninapomjibu swali lake Mheshimiwa Mbunge, hata ninyi Wabunge humu ndani mnafuatiliwa kwa sababu ni kosa na huwa linatokea hata mashuleni, vyuoni, maofisini, unakuta wanawake wananyanyaswa kutokana na tatizo hili la ngono ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama *TAKUKURU*...

MWENYEKITI: Waheshimiwa mmeelewa, endelea.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, tuna wataalam wa kutosha kugundua kwamba, hii ni ngono ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makodfi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Kaboyoka uliza swali lako, kwa niaba yake.

Na. 111

**Kutorejeshwa kwa Mikopo Iliyotolewa
na SUMA-JKT**

MHE. RUTH H. MOLLEL (K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA) Aliuliza:-

SUMA-JKT Idara ya Zana za Kilimo ilikopesha 5,355,153,000/= kwa idara mbalimbali ndani ya SUMA-JKT. Taarifa za CAG zimeonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 ni kiasi cha Sh.534,785,000/= ambayo ni kiasi chini ya asilimia 10 ndio kilirejeshwa:-

(a) Je, ni kiasi gani hadi sasa kimerejeshwa kwenye Idara hiyo ya Zana za Kilimo?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, uzembe huu wa kutohakikisha mikopo ya fedha za Serikali inarudishwa kwa wakati ili wakulima wengine nao waweze kukopeshwa kumechangia kukwamisha juhudi za kupunguza umaskini nchini?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kuwawajibisha waliohusika na utoaji huo wa mikopo bila kuhakikisha inarudishwa kwa wakati?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye Sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mradi wa zana za kilimo wa SUMA-JKT ulikopesha miradi mingine ndani ya SUMA-JKT jumla ya shilingi 5,355,153,000/= kama ilivyoelezwa katika Taarifa ya CAG ya mwaka 2015/2016 na kwamba mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2016, kiasi cha shilingi 534,785,000/= ndicho kilikuwa kimerejeshwa. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019, jumla ya shilingi 2,389,082,000/= zimerejeshwa katika mradi wa zana za kilimo ambayo ni sawa na asilimia 45 ya fedha zote zilizokopesha. Hivyo, mpaka sasa fedha ambazo bado hazijarejeshwa ni shilingi 2,966,071,000/=.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la kukopesha fedha hizo lilikuwa ni kuiwezesha kimtaji miradi ndani ya SUMA-JKT pamoja na miradi mingine mipya baada ya kujiridhisha kuwa ina tija. Hivyo, lengo hili halikwamishi juhudi za kupunguza umasikini nchini, basi linaongeza mapato katika miradi ya shirika kwa ujumla.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la SUMA-JKT limeendelea kuhakikisha fedha zilizobaki zinarejeshwa katika mradi wa zana za kilimo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhakikisha uwepo wa mikataba kati ya mradi wa zana za kilimo na mkopaji, pia mikataba iliyokuwa na upungufu imerekebishwa;

(ii) Kuhakikisha miradi iliyokopesha inazalisha kwa faida ambapo sehemu ya fedha hiyo huwasilishwa moja kwa moja katika mradi wa zana za kilimo; na

(iii) Kuweka baadhi ya miradi iliyokopesha chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa mradi wa zana za kilimo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth Mollel, jiandae Mheshimiwa Bulembo.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pesa hizo zilizokwenda kununua hayo matrekta ni pesa za walipakodi wa nchi hii na ni nyingi sana na mpaka sasa hivi karibu *2.9 billion* hazijarejeshwa. Mkakati mahususi a kuhakikisha kwamba, hii pesa inarudi, ni upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwa nini sasa wale wote ambao walikopa haya matrekta majina yao yasiwekwe kwenye magazeti tuwajue ni akinanani hao wanaokwamisha kurudisha mikopo ya Serikali? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ruth Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, fedha zilizokuwa zimekopeshwa ni bilioni tano na kitu ambazo zimesharudishwa ni bilioni mbili, yani tuko kwenye asilimia 45 ya urejeshaji, maana yake ni jitihada kubwa zimefanyika hapo na kiwango kilichobaki kitarejeshwa kwa sababu, fedha hizi hawajakopeshwa watu nje, zimekopeshwa ndani ya Mashirika ya SUMA-JKT lenyewe kwa maana hiyo wanafanya biashara mbalimbali. Sina shaka kabisa kwamba, fedha hizi zote zitarudi na faida itapatikana kwa sababu, SUMA-JKT limejiwezesha kimtaji kuanzisha biashara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu majina ya waliokopa matrekta kwamba, yawekwe kwenye magazeti. Jambo hili lilishafanyika, majina yaliwekwa kwenye magazeti na fedha hizi zimeendelea kukusanywa. Naomba nitoe taarifa kwamba, tokea Mheshimiwa Rais ametoa kauli ya kwamba, watu wote waliokopa warejeshe, tayari wamekusanya bilioni mbili na milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na jitihada hizi na kama tulivyosema SUMA-JKT itaanza kuuza mali za walikopa endapo hawatarejesha baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa madeni.

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Bulembo.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Waziri mhusika, kuna viongozi wa Serikali na hata humu Bungeni waliokopa SUMA katika matrekta haya. Mheshimiwa Waziri licha ya kuwatangaza wamefikishwa kwa Spika ili tutangaziwe humu Bungeni tujue ni wapi wanaodaiwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wako viongozi wa Serikali na baadhi ya Wabunge waliokopa matrekta haya. Juhudi tulizozifanya ni kwamba, tuliziandikia mamlaka za ajira za kila mmoja, kwa hivyo, Mheshimiwa Spika anayo orodha ya Wabunge na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waliohusika tumeandika barua TAMISEMI na Wizara zote kwa ujumla, kila mamlaka ya ajira imeandikiwa barua. Ni mategemeo yangu kwamba, kila mamlaka ya ajira itachukua hatua stahili ili kuweza kuzipata fedha hizi.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa sababu ya muda Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

Na. 112

Fidia kwa Wananchi wa Igwata – Maswa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Mipaka ya Mradi wa Mafunzo ya Msitu wa Kijiji cha Igwata, Kata ya Nyabubinza, Wilaya ya Maswa imepanuliwa na kuchukua baadhi ya Mashamba ya Wanakijiji na hivyo kusababisha wananchi kukosa maeneo ya kulima:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi hao ili waweze kununua maeneo mengine ya kufanya shughuli zao za kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa Hifadhi ya Igwata unahifadhiwa kisheria kwa Tangazo la Serikali Na. 324 la Mwaka 1953. Msitu huo una eneo la ukubwa wa hekta 132,851 ambapo hekta 85.19 ziko Wilaya ya Kwimba na hekta 47.678 ziko Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania ilianza kusimamia Msitu wa Igwata tangu mwaka 2010. Aidha, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1953 msitu huu haujawahi kupanuliwa; katika mwaka 1915/1916 kazi zilizofanyika ilikuwa ni uimarishaji wa mpaka, uwekaji wa maboya ambao ulifanywa na *TFS* kwa kushirikiana na uongozi wa vijiji vyote vinavyozunguka msitu huo. Vilevile mwaka 2015/2016 kazi ya tathmini, *Forest Inventory*, ilifanyika kwa ajili ya kutayarisha mpango wa usimamizi wa msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hajjawahi kupokea malalamiko au madai yoyote ya wananchi kuchukuliwa

mashamba yao kwa lengo la kuongeza ukubwa wa eneo la msitu. Aidha, hakuna mgogoro kati ya wananchi na taasisi zinazosimamia msitu huu, wananchi wanaendelea kutoa ushirikiano katika usimamizi na ulinzi wa msitu huo ambao ni hazina kubwa ya mbegu za miti asilia na urithi wa aina ya miti iliyopo katika hatari ya kutoweka ambayo inatumika katika tiba za jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ndiye mwakilishi wa wananchi wa Kijiji cha Igwata na Jimbo la Maswa Magharibi. Msitu huu ulipanuliwa na wakati wanapanua hawakushirikisha wananchi, ukamega mashamba ya watu. Sasa nataka niulize maswali ya nyongeza. Moja; kwa nini Serikali isirejeshe mashamba haya yaliyomegwa kwa wananchi ili waendeleo kuyatumia kwa shughuli zao za kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sehemu ya mashamba au eneo lililomegwa kuna makazi ya watu, Serikali inasemaje juu ya watu hawa ambao wameweka makazi kwenye eneo ambalo limeongezwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia sana malalamiko ya wananchi wake ambayo yalitokana na uwekaji wa alama. Sisi kwenye Wizara yetu kimsingi hatukuchukua mashamba mapya ila tuliweka alama, lakini naomba nimpongeze sana kwa namna alivyofuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi ambalo tunaendelea nalo sasa katika Wizara yetu ni kupitia upya malalamiko yote yanayoletwa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na viongozi wa Serikali katika maeneo husika. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama uchukuaji wa eneo hili una malalamiko, Wizara yetu inapokea malalamiko hayo na tunatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha kwamba, tunarejesha maeneo ambayo yana malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, iwapo kuna wakazi ambao wakati wa uwekaji wa mipaka hii walikumbwa na zoezi hili nitamtuma Afisa wetu wa *TFS* kwenda kuangalia. Iwapo itathibika kwamba, maeneo hayo wananchi bado wanayahitaji tuta-*review* mipaka ili kuweza kuwaachia waweze kukaa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mama Sitta, jandae Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Wananchi walioko Urambo katika Kata za Senda, Ukondamoyo na hasa Kijiji cha Yueta wana matatizo makubwa sana ya migogoro ya ardhi kutokana na kupakana na Pori la Akiba la Ugawa na kuwasababishia kukosa nafasi ya kulima na kufanya shughuli zao za mifugo. Je, Serikali itakuja lini Urambo kutatua tatizo hili ili wananchi hawa wanaopakana na Pori la Ugawa wafanye shughuli zao za kilimo na mifugo kwa raha? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana, anataka kujua ni lini tu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki,

tumeelekezwa kupitia upya mipaka na malalamiko ya wananchi kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema. Kwa hiyo, katika zoezi hili linaloendelea namwomba Mheshimiwa Margareth Sitta kwa sababu, wanaoleta malalamiko haya ni Halmashauri na Mkoa, atulettee malalmiko haya na tutayafanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Minja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Rais alipokuja Mkoani Morogoro kwa ziara aliagiza wananchi wa Mtaa wa CCT Mkundi ndani na Manispaa ya Morogoro wasibughudhiwe, lakini hivi sasa Maafisa wa Maliasili wameendelea kuwabughudhi wananchi wale. Je, ni kwa nini maafisa hawa wanapuuza agizo la Mheshimiwa Rais?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minja, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa wetu wa Maliasili, kwa maana ya TFS, wamekuwa wakisimamia sheria hasa kuangalia mipaka ya kihalali ambayo ipo katika maeneo husika, lakini kama kuna maagizo ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Rais kwamba, wananchi wasibughudhiwe, nitakwenda kufuatilia kuona ni kwa namna gani maafisa hao wanakiuka na tutatoa maelekezo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, muda haupo upande wetu; tunaendelea na Wizara hiyohiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi.

Na. 113

**Fidia kwa Wananchi Walioathiriwa na
Mamba – Mto Ruvuma**

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Wananchi wengi wameendelea kupoteza maisha na kujeruhiwa na mamba katika Mto Ruvuma:-

Je, ni lini wananchi walioathirika na mamba katika Vijiji vya Miesi Utimbe, Naliongolo, Mtolya, Geuza na Mchoti watalipwa fidia zao kwa mujibu wa sheria?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikilipa kifuta machozi kwa wananchi ambao wameshambuliwa na wanyamapori wakali kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Machozi za Mwaka 2011. Kuanzia mwaka 2013 mpaka 2018 jumla ya Sh.37,300,000/= zimelipwa kwa wananchi 65 waliopatwa na madhara kutokana na wanyamapori wakali, hususan mamba, katika Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza matukio ya wananchi kuendelea kupoteza maisha na kujeruhiwa na mamba, hasa wanapokwenda kuchota maji mtoni, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imechimba visima vya maji tisa katika vijiji vilivyo kandokando ya Mto Ruvuma. Vijiji hivyo, ni chipingo, Nalimbudi, Chikolopora, Maparawe, Mbangala, Geuza na Mkowo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika kukabiliana na changamoto za athari zilizosababishwa na mamba, mwezi

Julai, 2016, Wizara ilitoa kibali kwa Kampuni ya *Ontour Tanzania Limited* ambayo ilivuna mamba nane katika Mto Ruvuma na kupunguza kwa kiasi kikubwa matukio ya wananchi kujeruhiwa na kuuawa na mamba. Mfano katika kipindi cha Februari, 2018 mpaka sasa Wizara yetu haijapokea taarifa yoyote kuhusu wananchi waliouawa na kujeruhiwa na mamba katika eneo hilo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwanausi.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, bado wananchi wa jimbo langu hasa wanaoishi kandokando mwa Mto Ruvuma wameendelea kupoteza maisha na kupoteza viungo vyao kwa kasi kubwa sana. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuendelea kutimiza makubaliano yetu ya kuchimba visima katika vijiji sita vilivyobaki ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata unafuu wa kuathirika na suala la mamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba, lipo tatizo kubwa, lakini tatizo lililopo ni kwamba, wenzetu wa *TAWIRI* ambao wanatoa vibali vya kuvuna mamba wanatoa idadi ndogo sana ya vibali, kama alivyoeleza ni mamba tisa, lakini takwimu zinaonesha katika eneo hilo pekee lina mamba zaidi ya 300. Je, yupo tayari kutoa vibali zaidi ili wananchi hao waweze kuondokana na tatizo hili kwa kuvuna mamba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Bwanausi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa namna anavyofuatilia haki za wananchi wake walioshambuliwa na mamba. Kuhusu swali lake la kwanza amesema tatizo la wananchi kushambuliwa

na mamba bado linaendelea na palikuwa na makubaliano na Wizara yangu kupitia *TAWA* ya kuchimba visima. Kama makubaliano hayo yalifanyika na Serikali haina kipingamizi, nitawaelekeza *TAWA* kuhakikisha kwamba, makubaliano hayo yanatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, ni kweli kwamba, kabla ya kuvuna mamba Shirika letu ya Utafiti la *TAWIRI* huwa linafanya utafiti kujiridhisha na idadi sahihi na kama idadi hiyo ni tishio katika eneo husika. Nitawaelekeza pia, *TAWIRI* wafanye upya utafiti na iwapo itathibitika kwamba, idadi ya mamba waliopo sasa ni tishio tutatoa tena kibali cha kuvuna mamba hao kupunguza athari kwa wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Sisi Babati tuna ziwa ambalo lina viboko na wavuvi wanapokwenda kufanya kazi zao wamekuwa wakiuawa na viboko hao, lakini hakuna fidia. Tulipohoji pia, hata kwa Wataalam wa Halmashauri wanadai kwamba, wavuvi wanakuwa wamefuata viboko hivyo, hawastahili fidia. Naomba nifahamu Wizara inatusaidiaje ili kujua kwamba, wavuvi wa Babati na wananchi wale wanastahili fidia au la?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, Mbunge wa Babati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yapo matukio ya wananchi wa Babati kushambuliwa wao wenyewe na viboko, lakini pia mashamba yao kuharibiwa na mamba. Kimsingi wananchi wale wanastahili kupata fidia iwapo shambulio hilo litatokea nje ya eneo la makazi ya viboko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya sheria viboko hawa wanapokuwa katika eneo lao makazi

wanapomshambulia mtu inakuwa ni mtu ndiye aliyekwenda kuwavamia katika eneo lao. Nimhakikishie Mheshimiwa Gekul, iwapo kuna wananchi ambao malalamiko yao yapo na walishambuliwa nje ya eneo ambalo ni makazi ya viboko, Wizara yetu itachukuwa hatua ikiwa ni pamoja na kuagiza pia watu wa *TAWIR*/kufanya utafiti na kuona idadi ya mamba hao kama wanaleta tishio ili waweze kuvunwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Balozi Adadi.

Na. 114

Biashara ya Vipepeo Nje ya Nchi

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Katika kijiji cha Fanusi, Kata ya Kisiwani, Wilayani Muheza wapo wananchi wanaofanya biashara ya kutega vipepeo na kuvipeleka nje ya nchi kwa ajili ya kupata kipato na pia njia ya kukuza utalii:-

(a) Je, ni lini wataruhusiwa kupeleka tena vipepeo nje ya nchi badala ya Serikali kuzuia kama ni wanyama hai?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuboresha maeneo hayo ili kuwavutia watalii waweze kuja kwa wingi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Jimbo la Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipepeo ni moja ya aina za wanyamapori waliokuwa wakifanyiwa biashara ya

wanyamapori hai kwa kusafirishwa nje ya nchi kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wafanyabiashara kukiuka Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 na Kanuni zake; Serikali ilisitisha biashara ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi kwa muda wa miaka mitatu kuanzia Mei, 2016. Aidha, kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, Serikali imeamua kuendelea kufunga biashara ya usafirishaji wanyamapori hai nje ya nchi. Kufuatia uamuzi huo, Wizara inaandaa namna bora ya kushughulikia wanyamapori waliopo kwenye mashamba/mazizi. Aidha, wafanyabiashara walioathirika kutokana na zuio la kusafirisha wanyamapori nje ya nchi watarudishiwa fedha zao walizotumia kulipia Serikalini kwa ajili ya huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaboresha maeneo ya kuvutia watalii yaliyopo katika Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia wa Amani ambapo Kijiji cha Fanusi na vijiji vingine 20 vinapakana. Hifadhi hiyo ina vivutio vingi ikiwemo misitu minene, mito, wanyamapori na mimea adimu isiyopatikana maeneo mengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu huo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS inatekeleza mpango wa kuendeleza utalii wa ikolojia na kiutamaduni katika hifadhi ya Amani. Mpango huu unahusu kuboresha miundombinu ikiwemo barabara ya kuelekea Msitu wa Amani, nyumba za kulala wageni zilizopo ndani ya msitu, vituo vya kupumzikia watalii (*camp sites*) na njia za watalii (*nature trails*). Juhudi hizi zinatarajiwa kuongeza idadi ya watalii, kuongezeka kwa biashara, fursa za ajira na uwekezaji kwa maeneo yaliyo karibu na msitu huo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Balozi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo sjaridhika nayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali la kuzuia wanyama hai kusafirishwa nje ya nchi nina hakika lilikuwa ni zuri lakini lilikuwa linalenga wanyama hai wakubwa, sidhani kama Serikali ilikuwa inalenga vipepeo ambao ni kama wadudu. Wananchi hawa wa Fanusi wamekuwa wakifanya biashara hii ya kupeleka vipepeo nje ya nchi kwa muda na walikuwa wanapata pato zuri tu, karibu shilingi laki tatu mpaka nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki ambacho Serikali imezua biashara hii wananchi wamepata matatizo sana. Naibu Waziri mmepiga marufuku biashara hii kwa muda wa miaka mitatu ambayo inakwisha Mei mwaka huu. Je, baada ya muda huo Wizara itakuwa tayari kuwapelekea rasmi barua wanakijiji wa Fanusi ili biashara hiyo iweze kuanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri mwenyewe alifika kwenye maeneo haya na alitembea pale kwenye Kijiji cha Fanusi na kuona wananchi namna walivyobuni na kuanza huu mradi wa kufuga hawa vipepeo. Aliahidi na kumwelekeza Mkurungezi Mkuu wa *TFS* apeleke wataalam ili aweze kuwasaidia wale wananchi kukuza ubunifu wao na pia kuboresha mazingira yale. Ni lini wataalam hao na uboreshaji huo utaanza? Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakati tunazuia uuzwaji wa wanyama hawa hai nje ya nchi wapo wananchi wa vikundi mbalimbali walikuwa na vikundi vyao na walikuwa wanapata mapato na kulipa kodi kutoka na mauzo hayo. Hata hivyo, kama nilivyojibu kwenye swali

langu la msingi ni kwamba ulitokea ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu na Serikali ikaona itafute utaratibu mwingine wa kusimamia zoezi hili. Kama alivyosema itakapofika Mei, Serikali itatoa tamko sasa ni kwa namna gani tutaendelea na zoezi hili ili kutoaathiri kabisa shughuli hii hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu Mheshimiwa Waziri kuagiza kupelekwa wataalam, ni imani yangu kwamba baada ya agizo la Mheshimiwa Waziri wataalam hao walielekezwa kwenda lakini kama bado hawajafika nitahakikisha kwamba wanakwenda kutoa elimu kwenye vikundi hivi ambavyo vinashughulika na biashara hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mhusika.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuongezea ziada ifuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika katika Kijiji cha Fanusi, niliona jitihada za akina mama wale katika kikundi kile na niliona adha wanayoipata kwa Serikali kuzuia kusafirisha vipepeo nje ya nchi kutokana na ile *blanket ban* ambayo kama Serikali tuliitoa miaka mitatu iliyopita. Naomba kuweka sawa tu rekodi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa hatutaruhusu tena usafirishaji wa wanyama hai kutoka nchini mwetu kwenda nchi yoyote ile na tutafanya mabadiliko ya sheria ili kuzuia jambo hilo lisitokee tena katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, utaratibu ambao tunaushauri kwa wananchi wote ambao wamekuwa wakifuga wanyamapori hawa watafute namna nyingine ya kupata faida kutokana na maliasili hiyo na siyo kutegemea kusafirisha kwenda nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa akina mama wa pale Fanusi niliwashauri Halmashauri na nikaagiza washirikiane na

TFSkutafuta namna ya kufanya shughuli ya utalii wa vipepeo katika eneo lile kwa sababu kwa kweli vipepeo walioko pale ni wazuri mno na watu wangeweza kwenda kuwaona pale na kingekuwa ni kivutio cha utalii na wangepata kipato ambacho walikuwa wanakitarajia. Kwa hiyo, huo ndiyo uelekeo, waondokane na *mentality* kwamba kuna siku tutafungulia vibali vya kusafirisha nje ya nchi kwa sababu tumezuia na hatutafungua tena.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf bado una swali baada ya majibu haya ambayo yamezuia kila kitu?

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo swali, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na faida ya watalii kuja kuona vipepeo, nimegundua watalii wengi wakishaona wanafanya *identification* na wanachukua *sample* za vipepeo na kuondoka nazo. Je, Serikali yetu imeshafanya utafiti wanaenda kufanyia nini hivyo vipepeo wanavyochukua ili kuhakikisha hatupotezi rasilimali ya Taifa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yussuf, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba watalii wengi baada ya kuona vipepeo hutamani kuondoka nao na baada ya kuondoka nao kitu ambacho tumegundua ni kwamba nao wanakwenda kufanya biashara ileile ambayo sisi tunafanya ili watalii waje Tanzania. Kwa hiyo, ni kwa sababu hiyo Wizara ikaona hamna sababu tena ya kuendelea kuuza wanyama hai nje ya nchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali la Wizara ya Afya, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe.

Na.115

Utekelezaji wa Dira ya Taifa kupitia Wizara ya Afya

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Moja ya Dira ya Taifa kupitia Wizara ya Afya ni huduma bora ya afya ya wazazi na kupunguza vifo vya watoto na wazazi:-

Je, ni kwa kiasi gani Dira hii imetekelezwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto huandaa Sera na miongozo mbalimbali yakiwemo masuala ya afya ya uzazi na mtoto. Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga ni suala linalopewa kipaumbele cha kwanza katika Wizara. Dhamira hii inaonekana na kuthibitishwa katika miongozo mbalimbali ya Serikali kama vile Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007; Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); Mpango Mkakati wa Nne wa Afya; Mkakati wa Kupunguza na Kuimarisha Afya ya Uzazi, Watoto na Vijana; na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Wizara ni kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi 292 kwa kila vizazi

hai 100,000 na kupunguza vifo vya watoto kutoka 21 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi 16 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanikiwa kuongeza kiwango cha akina mama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka asilimia 51 mwaka 2012 hadi asilimia 73 mwaka 2018. Aidha, wanawake wajawazito wanaohudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi wameongezeka kutoka asilimia 40 mwaka 2012 hadi asilimia 72 mwaka 2018. Idadi ya wanawake wajawazito wanaohudhuria kliniki, mahudhurio manne na zaidi wameongezeka kutoka asilimia 46 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 57 mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanyika mwaka 2015/2016 unaonesha kwamba vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, vimepungua kutoka 90 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2010 na kufikia 67 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016. Vilevile, vifo vya kina mama vimepungua kutoka 578 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2010 na kufikia 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016. Ni matarajio yetu kuwa utafiti unaofuata wa mwaka 2019/2020 utatupa matokeo chanya zaidi katika kupunguza vifo vya akinamama na wajawazito Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, niMshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kama utafiti wa *UNICEF - Tanzania* ni sahihi kwamba akina mama 24 na watoto 144 wanafariki kwa siku na kwa mwezi kufanya idadi ya 5,040 na Serikali iliingia makubaliano mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ili kuhakikisha kwamba wanaboresha huduma za afya kutoka asilimia 28 hadi asilimia 60 ili kuokoa watoto 102,000,000 na wanawake 16,000,000, je, ni kwa nini sasa Serikali imeshindwa kufikia makubaliano haya ya asilimia 60 ya huduma ya afya ili kuokoa maisha ya watoto na akina mama hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali kwa sababu imeshindwa kufikia asilimia 60 ya huduma ya afya, ina mikakati gani ya makusudi kuweza kuimarisha ili kuondokana na vifo hivi vya watoto na akina mama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, jandae Mheshimiwa Mwambe.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijashindwa kufikia hayo makubaliano na haya niliyokuwa nayasema ni mlolongo wa utekelezaji wa maazimio hayo. Katika takwimu zangu nimeonyesha kwamba tunaendelea kupata mafanikio. Moja ni kwamba sasa hivi tumeongeza idadi ya akina mama ambao wanajifungulia kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya kutoka asilimia 50 – 73, haya ni mafanikio, akina mama wengi wanaenda kujifungulia katika vituo vyetu vyakutolea huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesema kwamba akina mama wanaohudumiwa na wataalam wa afya wameongezeka kutoka asilimia 40 – 72. Sambamba na hilo, tumeendelea kuboresha mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma za dharura na uzazi na vituo zaidi ya 300 vimeboreshwa na kuwekewa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumezindua Mpango wa Tujiongeze Tuwavushe Salama ambapo Makamu wa Rais alizindua ukishirikisha Wakuu wa Mkoa na kila Mkuu wa Mkoa amepewa majukumu yake na kila Mkuu wa Mkoa ameenda kusimamia haya katika wilaya zake. Kama Wizara tumeanza kuchukua takwimu ambazo siyo rasmi lakini mwelekeo wetu unaonyesha kwamba vifo vya akina mama vimepungua sana ndani ya nchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe, baadaye Mheshimiwa mama Salima.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa niaba ya akina mama wote wa Tanzania, napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze waziwazi, nafahamu wazi kabisa huduma ya bure iliyokuwa inatolewa kwa mama na mtoto kupitia Huduma ya Tumaini la Mama imefutwa na kwamba hakuna mzazi yeyote anayeandikishwa sasa hivi kuanzia tarehe 31 Desemba.

MWENYEKITI: Swali.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ni nini tamko la Serikali kutokana na jambo hili kwa sababu hailijatangaza waziwazi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa swali nzuri kwa niaba ya wanawake wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunakiri kwamba huu utaratibu wa Tumaini la Mama ulikuwa na mchango mkubwa sana katika afya ya uzazi katika Mikoa ya Kusini. Mkataba ule umekwisha na sisi ndani ya Serikali bado tunaendelea kuufanyia kazi pamoja na Wizara ya Fedha. Taratibu zitakapokamilika tutatoa taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa mama Salima Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 14 inasema kila mtu anayo haki ya kuishi. Mwanamke

na mtoto hawatakiwi kufa hasa mama wakati analeta kiumbe kingine dunia. Tunaona vifo ni 556 kati ya vizazi hai 100,000 na kule kwa watoto 21 kati ya vizazi hai 1,000 na tunaambiwa tufikapo 2020 tufikie 10 kati ya vizazi hai 1,000. Je, Dira hii ifikapo 2020 au 2025 tunaweza kuifikia ili kunusuru maisha ya hawa wazazi pamoja na watoto wao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Salima Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali na Serikali hii ya Awamu ya Tano imedhamiria kabisa kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akina mama na watoto. Nikiri kauli ambayo ameisema Mheshimiwa Salma Kikwete kwamba ujauzito haujawahi kuwa ni ugonjwa na mama mjamzito hapaswi kufariki kutokana na uzazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe tu *comfort* Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imewekeza nguvu sana na kipaumbele chetu kikubwa sana ndani Wizara ni kuhakikisha tunapunguza vifo vya akinamama na watoto. Tumeongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba katika masuala ya uzazi; tumeboresha vituo vya afya; tumeendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wetu wa afya na tumeendelea kuweka mifumo mbalimbali na kuhakikisha kwamba tunatoa hamasa katika jamii na viongozi wote katika ngazi zote kuwajibika. Mimi niseme tu *in a very an official way* kwamba tutakapofanya utafiti mwakani nina uhakika tutapata takwimu nzuri zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Janet Mbene.

Na. 116

**Baadhi ya Dawa Kutumiwa kama Mbadala
wa Dawa za Kulevya?**

MHE.JANET Z. MBENE aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la matumizi ya dawa za kupunguza maumivu zenye Codeine, Valium, Morphine, Amphetamine, Phenorbabitone ambazo zinouzwa bila cheti cha daktari na zinatumiwa kama mbadala wa dawa za kulevya:-

(a) Je, Sheria zinasemaje kuhusu hilo linalosababisha vijana kuwa mateja wa dawa za kawaida?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha hakuna *prescription drugs* inauzwa bila cheti cha daktari?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Sheria ya Chakula na Dawa, Sura Na. 219 katika kifungu chake 77(2) inatambua makundi matatu ya dawa ambayo ni:

(i) Dawa zinazodhibitiwa ama kwa jina la kigeni inaitwa *controlled drugs* kama *Morphine*, *Pethidine* na *Diazepines* kama vile *valium*:-

(ii) Dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari, *prescription only medicines* mfano dawa za *antibiotic*, shinikizo la damu, kisukari, za saratani na dawa zenye viambata vya *Codeine*; na

- (iii) Dawa za kawaida ambazo kwa lugha ya kigeni tunaita *Over the counter/general medicine* dawa hizi hazihitaji cheti cha daktari. Mfano kama dawa za kikozi, mafua na maumivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Mamlaka ya Chakula na Dawa, Sura 219 kifungu cha 77(4) kinatoa adhabu ya faini au kifungo kwa mtu yeyote atakayekutwa akitoa dawa za zinazodhibitiwa na zinahitaji cheti cha Daktari.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pamoja na uwepo wa sheria na adhabu hizo bado kumekuwa na changamoto za uuzwaji wa dawa zinazohitaji cheti cha daktari pasipokuwa na chetu hicho. Wizara imeandaa mikakati mbalimbali ya kukabiliana na suala hili kwa kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuandaa kanuni za usimamizi na udhibiti wa dawa za cheti ambapo pamoja na mambo mengine zitaainisha namna dawa zinazodhibitiwa (*Tramadol, Diazepam, Pethidine na Morphine*) ambapo kwa sasa rasimu ya awali imeshakamilika. Aidha, adhabu kali zimebainishwa kwa watakaokiuka taratibu hizo;
- (ii) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeandaa mifumo ya udhibiti ukaguzi katika meneo yanayotoa huduma za dawa nchini; na
- (iii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara yanayoweza kupatikana kutokana na matumizi holela ya dawa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yaliyotuelimisha, lakini kama alivyokiri mwenye pamoja sheria zilizopo bado dawa za makundi yote matau zinauzwa holela. Swali la kwanza, je, Serikali inatathimini yoyote inayoonesha madhara gani yanatokea kwa matumizi haya ya hovyoyote ya dawa za maumivu na *antibiotic* na dawa zote alizozitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jem haoni sasa kuna haja ya kuhamisha hizi dawa ambazo ni *restricted* kwa maduka ya *MSD* yaliyoenezwa nchi nzima ili *pharmacy* zingine ambazo zitatoa dawa hizi ziwe rahisi kufuatilia? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ongezea na *panadol* watu wanatumia ovyo ovyo, inaharibu maini.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Janeth Mbene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa maelezo ya awali, tunakiri kwamba pamoja na kwamba dawa hizi zipo katika makundi haya bado kuna changamoto ya matumizi ya dawa pasipo na cheti cha daktari. Wimbi la tatizo hii limeanza kuwa kubwa na nitumie fursa hii kutoa elimu kwenye jamii, baada ya Serikali kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, tumeanza kuona matumizi ya madawa ambayo kwa lugha ya kigeni tunaita *prescription drugs* zimeanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ambao wanaendelea kutusikiliza, matumizi ya dawa hizi za hospitali na matumizi ya vileo na tumeanza kuona kwamba kuna tatizo kubwa sana ya *prescription drugs* pamoja na vileo ambavyo vinapelekea athari kubwa sana kwa wananchi. Matumizi ya pombe yana athari katika ubongo wa mtumiaji na

prescription drugs zina athari katika mapafu na katika maini ya watumiaji. Kwa hiyo, mtu ambaye anatumia dawa hizi kwa pamoja na pombe yuko katika hatari kubwa zaidi ya kuweza kupoteza maisha kwa sababu hivi vyote vinafanya kazi za aina moja yaani dawa hizi zinaongeza kasi ya zile athari za pombe na zile dawa zinapokuwepo mwilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumellona hili na tumelibaini tatizo na tumeanza ndani ya Wizara kuweka utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba hizi dawa ambazo zipo *control* tumeweka mfumo mzuri toka zinaingizwa nchini mpaka pale ambako zinakwenda kutumika na mtumiaji wa mwisho. Hili ni jambo ambalo tunaendelea kulifanyia kazi ndani ya Wizara.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy, Mheshimiwa Kabati ajjandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Watumiaji wa madawa ya kulevya hivi sasa Serikali kutokana na jitihada kubwa na nzuri za mapambano dhidi ya madawa sasa hivi wamegeuza kibao wameanza kutumia dawa kama *pethidine*, *benzodiazepine* dawa hizi zimekuwa zikisabisha kwamba watu ambao wanatumia madawa kulevya madawa hakuna wanatumia dawa hizi. Je, Serikali iko tayari sasa kuleta sheria ambazo zitakuwa kali sana ili kuweza kudhibiti usambazaji na manunuzi ya dawa hizi ili zifanane na jitihada kubwa na nzuri zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya Tanzania?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali zuri la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya awali tumeanza kuona ongezeko

la madawa ya hospitali ama *prescription drugs* zikianza kutumika ndivyo sivyo kama mbadala wa madawa haya ya kulevya. Sisi kama Wizara tumeanza kuchukua hatua na ni mambo ambayo tunaendelea kuyafanya kama ndani ya Serikali. Kuanza kutoa elimu kama ambayo nimeitoa hapa kwamba hizi dawa zinatakiwa zitumike kwa malengo ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tumeanza sasa kuweka utaratibu mzuri wa kufanya udhibiti wa hizi dawa kuhakikisha pale tangu zinapoingia mpaka kwa mtumiaji wa mwisho. Niseme kwamba uratibu huu tumeshauanza ndani ya Wizara na tutaendelea nao. Sheria tulizonazo za matumizi ya madawa ya kulevya zinaongelea vilevile hizi dawa za *prescription drugs* na sheria ni nzuri tu zinajitosheleza kwa adhabu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kabati, jandae Mheshimiwa Sanga.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la vijana wetu kutumia madawa ya kulevya na kwa kuwa *sobernyingi* sana zinamilikiwa na watu binafsi na kwa kweli zimekuwa zikifanya vizuri, lakini gharama za kuziendesha tunaona ni kubwa kiasi kwamba vijana wengi wanashindwa kumudu gharama zake. Je, ni kwa nini sasa Serikali isitoe ruzuku kwa hizi *sober house* za watu binafsi au kuanzisha za kwake ili kusaidia vijana wetu kurudi katika hali zao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba kumekuwa na tatizo la dawa ya kulevya na Serikali imechukua juhudi

na hatua ya kuhakikisha kwamba tunadhibiti uingizaji wa dawa za kulevya na kwa kiasi kikubwa kwamba tumepunguza sana matumizi ya madawa za kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunatambua vilevile kwamba kuna wahanga ambao walikuwa wanatumia hizi dawa za kulevya, sisi Serikali tumeendelea tukishirikiana na wadau binafsi. Kwa upande wa Serikali tumeanzisha vituo mbalimbali vya matibabu katika hospitali zetu za Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na hivi karibuni tumezindua hapa Itega Dodoma, lakini tunatambua mchango mkubwa wa *sober houses* na sisi kama Serikali tumetoa mwongozo wa usimamizi wa hizi *sober houses*, lakini sasa hivi bado ni mapema sana kusema kwamba Serikali itakuwa inachangia Ruzuku kwa uendeshaji wa hizi *sober houses*.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Deo Sanga aulize swali lake.

Na. 117

Ujenzi wa *One Stop Centre* – Makambako

MHE. DEO K. SANGA aliuza:-

Serikali ilichukua eneo la Idofu kwa ajili ya kujenga *One Stop Center* lakini hadi leo wananchi hawajalipwa fidia:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga *One Stop Center* kama ilivyokudia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya uthamini wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (*One Stop Inspection Station – OSIS*) cha Makambako katika eneo la Idofu Makambako. Tayari kazi ya uthamini wa mali na mazao yatakayoathiriwa na mradi huo imekamika. Wananchi ambapo mali zao zimeathirika na maradi watalipwa fidia kwa kuzingatia Sheria Na.4 ya Ardhi ya mwaka 2001 kabla ya ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeanza hatua za maandalizi ya awali wa ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa pamoja kwa kusaini mkataba na Mhandisi Mshauri *UWP Consulting (T) Limited* akishirikiana na *UWP Consulting* ya Afrika kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa vituo vya Ukaguzi wa Pamoja vya Mikumi, Makambako na Mpemba. Mhandisi Mshauri amekamilisha kazi ya awamu ya kwanza ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali mwezi Juni, 2018. Kazi ya usanifu wa kina itakamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizi zinatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Malipo ya fidia yakikamilika na Serikali kupata fedha ndipo ujenzi kwa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Makambako utaanza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Deo.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Mwaka 2015, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli aliwaahidi wananchi wa Makambako kulipa fidia kwa ajili ya eneo hili linalojengwa Kituo cha *One Stop Centre* yalikuwa maeneo mawili, tunaishukuru Serikali imelipa fidia kwa ajili ya kujenga soko la kimataifa na sasa bado hili la Idofi ambalo

linajengwa kituo hiki. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alipotoka Njombe alifika eneo la Makambako na tukampeleka pale Idofi ambapo alikutana na wananchi na Mheshimiwa Diwani mhusika na wananchi wana imani kubwa na Serikali juu ya kulipa fidia zao. Je, ni lini sasa Serikali itawalipa fidia wananchi wa Idofi ili waweze kuendelea na shughuli mahali pengine watakapohamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mwaka huu wa fedha wa 2019/2020, hivi sasa tutaanza kuandaa bajeti, naiomba Serikali, ni kwa nini kwenye bajeti hii ya 2019/2020 usiingizwe mpango huu ambao umeingizwa hapa? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, Waziri mhusika Mheshimiwa Kamwelwe.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Deo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi, lakini aliahidi kujenga mradi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja sasa katika ujenzi wa kituo hicho kuna *process* kama ambavyo jibu la msingi limesema; kuna usanifu wa awali usanifu wa kina na hatuwezi kujenga mradi bila kulipa fidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Deo pamoja na wananchi wa Jimbo lake Makambako ni kwamba mradi ni ujenzi wa kituo cha pamoja lakini katika mradi ndio kuna hizo hatua zingine, kwa hiyo nimhakikishie kwamba...

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Kwa hiyo nimwahidi Mbunge na wananchi wa Makambako kwamba mradi utatekelezwa hatua zote pamoja na ulipaji wa fidia utafanyika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniphace.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, niwashukuru sana Wizara ya Ujenzi kwa kunipa fedha za kutengeneza barabara ya Mugeta Siloli Simba. Na kwa kuwa ile barabara ilikuwa na km 21 na zimetengenezwa kilomita fulani na zimebaki kilomita tisa. Naomba kujua kutoka kwa Waziri ni lini sasa watapeleka fedha ili kumalizia kilomita tisa zilizobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Pareso, halafu Mheshimiwa Chikambo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumefanya ujenzi wa kuboresha sehemu ya barabara ya Mugeta kwenda Siloli Simba, lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana name kwamba sehemu ya kilomita 11 iliyojengwa, barabara haikuwepo kabisa, lakini kile kiwango cha barabara kimewavutia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo hili ili sehemu ambayo ilikuwa na barabara awali na yenyewe ifanyiwe maboresho. Kadri tunavyopata fedha kilomita hizi chache zilizobaki tunafanya maboresho.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Pareso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Madai ya wananchi ya kudai fidia kutokana na miradi ya ujenzi nchini yapo kila siku, ni mengi na ni makubwa. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanawalipa wananchi hawa kwa uhakika na kwa wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pareso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu tumeendelea kufanya malipo ya fidia miradi inapotekeleza nchi kote katika maeneo mbalimbali. Pia niseme tu shughuli za miundombinu zinaendelea, kwa hiyo tutaendelea kuwalipa wananchi fidia na kadri miradi itakavyoendelea tutaendelea kufanya malipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge tusiwe na wasiwasi tumejipanga vizuri, kwa mwaka wa fedha mmetupitishia fedha zakufanya usanifu kilomita 3,856. Sasa tuone kwamba hitaji la kufanya maboresho ya miundombinu litaendelea na kulipa fidia kwa wananchi tutaendelea kulipa kulingana na sheria na taratibu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikambo, halafu Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Majibu mazuri. Pamoja na majibu yake, lakini naomba niulize swali la nyongeza. Katika kutekeleza mradi wa barabara kwa kiwango cha lami barabara ya Namtumbo - Tunduru – Tunduru – Mjini Nakapanya wananchi wale wamekuwa wakusubiri kulipwa fidia zao kwa muda mrefu. Je, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha wanalipwa na kuwaondolea adha hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chikambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, mradi huu ulikopita wananchi walipwa fidia isipokuwa natambua tumezungumza na Mheshimiwa Chikambo, wapo wananchi

wachache sana ambao walikuwa wana malalamiko yao, suala hili tunaendelea kulifuatilia, tukitatuwa tutawalipa hawa wachache kulingana na stahili zao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nchambi atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi shapu wa Jimbo la Kishapu, naomba nitoe pongezi kwa Wizara kwa kazi nzuri manayoifanya, lakini nina swali la nyongeza kwakuwa bararaba ya Kolandoto kwenda Kishapu ni muhimu kwa kuwekwa lami kwa sababu za kiuchumi na mambo mengine

Je ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo ya lami kutoka angalau Kolandoto kwenda Kishapu?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, anataka kujua ni lini tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nchambi, Mbunge shapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba eneo hili kutoka Kolandoto kwenda Mwangongo na bararaba hii inaenda kuunganisha kupita Sibiti na maeneo ya mikoa mingine. Kwa hiyo, tutakapopata fedha tutaanza kujenga barabara hii muhimu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, ni lini sasa watamalizia barabara ya Kimanga ambayo inajengwa sasa kwa muda wa miaka miwili, mpaka sasa imeleta usumbufu mkubwa katika Kata ya Kimanga na mpaka sasa haijamalizika imesimama na mkandarasi hayupo, ni lini Serikali itamalizia hiyo barabara?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Halima Mdee.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaluwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, baada ya Bunge hili nitatembelea mradi huu niangalie pamoja na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona changamoto zilizopo ili tujue hatua za kuchukua kwa haraka ili barabara iweze kuboreshwa.

MWENYEKITI: Kwa hiyo unakwenda jimboni kwake?

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mradi.

MWENYEKITI: Haya, ahsante. Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya barabara ambayo nimeizungumza sana na Mheshimiwa Waziri pamoja na TAMISEMI wanajua, ni Barabara ya Chuo cha Ardhi – Makongo - Goba. Imekwama kutengenezwa kwa sababu ya fidia, sasa nataka Waziri aniambie, ni lini kipande hicho kitalipwa fidia ili wananchi wa Makongo waweze kujengewa barabara ya lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, kodi zilipwe na fidia itapatikana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali na nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa sana imefanyika kuboresha miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam na Mheshimiwa Mbunge anafahamu. Changamoto

ambazo zimebaki ni kulipa fidia kwa hizi kilometa nne zilizobaki. Barabara hii ni muhimu kwa sababu tunavyojenga barabara ya juu pale Ubungo, barabara hii itatumika pia kupunguza msongamano ili kufanya ujenzi uende kwa haraka. Tunatambua umuhimu huo, kwa hiyo nimwombe tu Mheshimiwa Mdee avute subira, suala hili tunalifuatilia kwa umakini kuhakikisha kwamba kipande hiki kinatengenezwa.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa. Tunaendelea na Wizara ya Habari, swali la Mheshimiwa Sabreen, kwa niaba yake Mheshimiwa Selasini.

Na. 118

Kujengwa Uwanja wa Michezo Wenye Hadhi

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA) aliuliza:-

Michezo ni afya, furaha, burudani, undugu na pia huondoa au kupunguza uhalifu nchini. Kuwa na viwanja vyenye hadhi kama kile cha Jakaya Kikwete *Youth Park* huvutia vijana wengi nchini kupenda michezo:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga viwanja vyenye hadhi hiyo nchi nzima?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa viwanja vya michezo nchini si suala la Serikali peke yake bali jamii nzima ya Watanzania zikiwemo taasisi za umma, asasi za kiraia na kampuni za watu binafsi. Wajibu wa Serikali

ni kuonesha njia kwa ujenzi mkubwa wa viwanja changamani kama vile Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru ulioko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyote viwili sasa hivi viko katika ukarabati mkubwa utakaogharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu ili kujiweka tayari kwa Mashindano ya Mpira wa Miguu wa Bara la Afrika kwa watoto chini ya umri wa miaka 17 yatakayofanyika mwezi wa Nne mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ukarabati huo mkubwa Serikali imekamilisha maandalizi yote ya awali na ya kiufundi ikiwemo upatikanaji wa eneo la hati miliki, uwekaji wa mipaka ya eneo lote pamoja na *beacons*, ununuzi wa gari mbili za mradi huo, tathmini ya kimazingira, tafiti za eneo, upembuzi yakinifu wa mradi na michoro ya ubunifu wa ujenzi wa uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kiwanja cha Jakaya Mrisho Kikwete *Youth Park* cha Dar es Salaam anachokiongelea Mheshimiwa Mbunge kimejengwa kutokana na mahusiano ya karibu kati ya Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ilala chini ya Mbunge wake Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Kampuni ya *Symbion* kwa kushirikiana na *Club ya Sanderland*.

MWENYEKITI: Hampigi makofi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kama ni kuonesha njia Serikali imeshafanyika hivyo na itaendelea kujenga viwanja vingine kadiri mahitaji yatakavyojitokeza na uwezo wa kifedha utakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kulipongeza Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (*TFF*) kwa uboreshaji wa Viwanja vya Kaitaba Kagera, Nyamagana Mwanza, na Mikoa ya Iringa, Singida na Lindi kwa kuonyesha njia katika upatikanaji wa viwanja bora vya michezo nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, ningependa tu niishauri Serikali pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wanafanya mambo yanayoacha alama katika jamii watambuliwe. Uwanja wa Jakaya Mrisho Kikwete *Youth Park* ilikuwa ni kazi nzuri iliyofanywa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. Mambo kama haya yakitajwa, kama Mheshimiwa Lema alivyojenga ile hospitali ya Mama na Mtoto kule Arusha, yanawatia moyo Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo wanaendelea kuhangaika kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo niombe kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanja vingi sana vya michezo ambavyo vimevamiwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Je, Wizara iko tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, ili kurejesha viwanja hivi na kujenga viwanja vidogo vidogo kama huu wa Jakaya Mrisho Kikwete *Youth Park* kwa ajili ya michezo ya watoto wetu ambao wanacheza hovy barabarani na kuhatarisha maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna viwanja vya mpira wa miguu hapa nchini, ambavyo kwa kweli ni vibovu. Hivi karibuni timu ya Yanga ilicheza kwenye uwanja fulani, sitaki niuseme na ilipata shida sana kwa kweli, yaani unaona hata wanavyopasiana wanavyopiga chenga na nini inaathiri matokeo. Sasa kwa nini viwanja kama hivi visifungwe ile michezo ya ligi *TFF* ikahamishia kwenye viwanja vya karibu ili kutoa nafasi viwanja kwa hivyo kukarabatiwa?

MWENYEKITI: Ahsante kwa swali zuri. Mheshimiwa Waziri si matokeo tu wachezaji wanaumia na timu hizi zinagharamia sana huduma za wachezaji. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa maswali yake mazuri ambayo ameyauliza, lakini niseme kwamba ushauri ambao ameutoa tumeupokea na tutaendelea kuufanyia kazi. Nikianza na swali lake la kwanza ambalo amezungumzia viwanja kuvamiwa. Nikiri kwamba ni kweli kuna tatizo kubwa sana la viwanja kuvamiwa nchini Tanzania na hata juzi ambapo nilikuwa Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kibondo nilikuta kwamba kuna kiwanja kizuri kabisa cha mpira lakini kimevamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho naweza kusema ni kwamba, changamoto kubwa ambayo inasababisha viwanja hivi kuweza kuvamiwa ni kwa sababu kwanza viwanja vinakua havina Hati Miliki, hilo la kwanza, lakini unakuta viwanja vipo lakini havijazungushiwa wigo. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kuweza kutoa wito kwa wamiliki wa hivyo viwanja, iwe ni Halmashauri, kampuni za watu binafsi au vyama vya kisiasa kuhakikisha kwamba cha kwanza, wanavitafutia Hati hivyo viwanja lakini jambo la pili waweze kuzungushia wigo hivyo viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake pili ameuliza kuhusu ubovu wa viwanja na ameshauri kwamba kwa nini hivyo viwanja visifungwe ili ukarabati uweze kufanyika. Niseme kwamba ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupokea, lakini kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba suala la ukarabati wa viwanja si suala la Serikali peke yake, ni suala la Serikali lakini kushirikiana na wadau wote ambao wanamiliki viwanja hivyo. Kwa hiyo nitumie fursa hii pia kwa wadau wote ambao wanamiliki hivyo viwanja kuhakikisha kwamba wanatenga fedha, lakini vilevile wanashirikiriana na TFF kuhakikisha kwamba hivyo viwanja vinaweza kukarabatiwa ili basi wanamichezo wetu waweze kucheza michezo vizuri.

MWENYEKITI: Balozi Mwamoto, atafuatia Mheshimiwa Mabula.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu viwanja, pamoja na kwamba hata viwanja vitakavyofanyika michezo ya *AFCON* naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa jana tumehakikishiwa kwamba timu yetu itakayoshiriki michezo ya *AFCON* itashinda nataka kujua tu wamefanya maandalizi gani, watuambie maandalizi yaliyofanyika ili tuwe na uhakika kwamba timu yetu sasa tunaenda kubakiza kombe hapa Tanzania?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri sana, lakini vilevile naomba nirejee kauli ya Waziri Mkuu ya jana, kwamba tumejipanga vizuri. Timu yetu ya Taifa ya Vijana Chini ya Umri wa Miaka 17 (*Serengeti Boys*) iko kambini kwa wiki tatu sasa na kazi yetu kubwa sasa hivi ni kuipambanisha na timu mbalimbali za wakubwa wao hasa wa chini ya umri wa miaka 20, kuweza kuwaimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kulikuwa na mechi kubwa sana na timu nzuri katika Afrika Mashariki Azam *FC under 20* na matokeo yake ni kwamba *Serengeti Boys* imewachapa kaka zao magoli matano kwa bila. Tukumbuke vilevile kwamba Azam *FC* ina baadhi ya wachezaji wa Ligi Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho timu ya Serengeti inakwenda Arusha angalau kuji-*acclimatize* (kujizoeshia) na hali ya Arusha na kuweza kupambana na timu mbalimbali kabla ya kwenda Uturuki kwa mwaliko wa *UEFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tujivunie ubora wa timu yetu, kwamba imeweza kutambuliwa kama moja ya timu bora katika Afrika kuitwa kwenye mashindano ambayo yanaunganisha timu nne za Afrika na timu nne za Ulaya. Tunakwenda kule na mechi yetu ya kwanza itakuwa tarehe 4 mwezi wa tatu dhidi ya Guinea; na baadaye tutacheza na Australia na kumalizia na timu yka Uturuki. Sasa hivi naongea na wenzetu wa *TBC* tuweze kupata live *coverage* kutoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano hayo yataisha tarehe 11 Machi na timu hiyo haitarudi Tanzania, tunaitafutia pesa lazima iende Spain ikafanye mazoezi na mashindano kidogo na wenzao na baadaye iende Cameroon ikashindane na baadhi ya timu kule ndipo itarejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, wiki ya kwanza mwezi wa Aprili tumekaribishwa na Rwanda kujipima nguvu na timu nne bora za Afrika ambazo ni Cameroon, Rwanda na Uganda. Baada ya hapo inarejea nchini kwa mechi ya ufunguzi dhidi ya Nigeria ambayo nina uhakika tutaishangaza Afrika katika matokeo yake. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante mnaweza mkaiweka timu ya Simba vilevile mkapata uzoefu zaidi. Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nami nianze tu kwanza kwa kuishukuru Wizara kwa kuendelea na jitihada za kuboresha na kuimarisha Uwanja wa Nyamagana. Sasa kwa sababu tunaamini kwamba ili tuwe na vijana wengi ambao wanacheza mpira vizuri ni lazima tuwe na viwanja vingi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jiji la Mwanza tuna *Milongo Sports Center* ina viwanja takribani vitano kwa wakati mmoja. Ningependa sasa kumwomba Mheshimiwa Waziri apate nafasi aje atembelee viwanja hivi na tuone

namna ya kuviboresha ili kupata vijana wengi zaidi; je, yuko tayari kufanya hivyo tukimaliza Bunge hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Jiandae Mheshimiwa Mbaruk.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mabula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote wa Jiji la Mwanza kwa jitihada kubwa sana na nzuri ambazo wanafanya katika kuboresha viwanja vyetu. Vilevile niseme kwamba ni juzi tu nilikuwa Wilaya ya Nyamagana na nikatembelea ule Uwanja wa Nyamagana ambao umekarabatiwa kwa jitihada za Halmashauri, Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wadau. Niseme kwamba ombi lako nimelipokea na nitafika tena kwenye Jiji la Mwanza ili kuweza kuangalia namna gani ambavyo tutashirikiana pamoja. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*) wametupa upendeleo Jiji la Tanga kutaka kutujengea Uwanja wa kisasa, lakini cha kushangaza eneo lile halijazungushiwa uzio na watu wameshaanza kulivamia, sasa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, je, ni lini harakati angalau za kuanza maandalizi na kujenga uzio katika lile eneo ili lisivamiwe utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jiji la Tanga ni eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya kujenga uwanja changamani wa michezo kwa fedha ambazo tunategemea zitatoka *FIFA*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *as soon as* fedha hizo zitakuwa zimefika, ujenzi wa uwanja huo utaanza. Kwa hiyo, nimtoe shaka kwamba, ujenzi utaanza mapema sana mara tu fedha zitakapokuwa zimefika. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwenda, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali linaulizwa na Mheshimiwa Ussi Pondeza.

Na. 119

Mpango wa Kuimarisha Uchumi wa Viwanda

MHE. USSI SALUM PONDEZA aliuliza:-

(a) Je, ni viwanda vingapi vimeanzishwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano ianze utekelezaji wa mpango wa kuimarisha uchumi wa kati wa viwanda?

(b) Je ni viwanda vingapi vilibinafsishwa na kushindwa kuendelezwa ambavyo vimerejeshwa Serikalini tangu kuanza utekelezaji wa mpango wa kuimarisha uchumi wa kati wa viwanda?

(c) Je sekta ya viwanda inachangia kiasi gani pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbageni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za kujenga uchumi wa viwanda zinazofanywa na Serikali ya

Awamu Tano, tangu iingie madarakani hadi kufikia Disemba, 2018 jumla ya viwanda 3,504 vimeanzishwa nchini. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda vidogo sana 2,500; viwanda vidogo 943; viwanda vya kati 51; na viwanda vikubwa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikifanya tathmini ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukulia kwa viwanda 68 ambavyo havijaendelezwa. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilijiridhisha na mapendekezo yaliyotolewa na kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Hazina kuchukua hatua. Kutokana na kuchukua hatua hiyo tayari viwanda 14 vimesharejeshwa Serikalini na juhudi za kuvitafutia wawekezaji wengine walio tayari kuviendeleza zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hali ya uchumi ya mwaka 2017, mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa ni asilimia 5.5, ikilingalishwa na asilimia 4.9 ya mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.6.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pondeza.

MHE. USSI S. PONDEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ningependa *Hansard* isomeke vizuri, mimi sio Mbunge wa Chumbageni, ni Mbunge wa Chumbuni, Zanzibar, Chumbageni ipo Tanga, kwa hiyo ningependa *hansard* isomeke vizri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza ambayo ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri. Kwanza angetupatia tafsiri ya viwanda, katika majibu yake mazuri ametuambia kuna viwanda vidogo na viwanda vidogo sana; kwa hiyo tungependa tupate tafsiri nini tofauti ya viwanda vidogo na viwanda vidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningependa kumuuliza, kwa kuwa Wizara yake haihusiki na uwekezaji wa viwanda katika Serikali ya Zanzibar; hadi sasa wawekezaji

wakitaka kuwekeza Zanzibar wanatakiwa wachukue leseni zitoke *BRELA*. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuiachia Wizara ya Viwanda ya Serikali ya Zanzibar kuweza kusimamia kazi hii ya utoaji wa leseni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe radhi kwa kukosea Jimbo lake na nashukuru amesahihisha. Pili, napenda kusema kwamba viwanda vidogo sana ni vile ambavyo mtaji wake hauzidi milioni tano na wafanyakazi wake hawazidi wane. Viwanda ni vidogo vile ambavyo mtaji wake ni ule ambao hauzidi milioni 200 na wafanyakazi wake hawazidi 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa suala la leseni; suala hilo umelizungumza lakini kimsingi ni kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara inashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Viwanda Zanzibar kiasi kwamba shughuli nyingi tunafanya pamoja. Hata hivyo maboresho yoyote yanayolenga kurekebisha na kuleta urahisi wa kuwekeza yatafanyiwa kazi ili kuwawezesha wananchi wetu na wadau mbalimbali wanaopenda kuwekeza wafanye shughuli zao bila shida na kwa uharaka iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa, atafuatia Mheshimiwa Kubenea.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sera ya Viwanda Tanzania imetamalaki. Sasa nipende kumuuliza Mheshimiwa Waziri Kiwanda cha Kufua Chuma pale Liganga kitaanza lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi, anataka kujua lini tu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngalawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi chuma cha Liganga kinahitaji uwekezaji mkubwa sana na pale tunazungumzia kuwekeza katika suala la ufuaji wa chuma, ambacho kimechanganyika na madini ya aina nyingine ikiwemo *Titanium*, *Vanadium* na *Aluminium*; wakati huo huo kuna suala la kufua umeme. Hayo yote yanafanyiwa kazi na ikizingatiwa kwamba hivi karibuni tulipitisha sheria zetu ya kutunza rasilimali zetu na kuwawezesha Watanzania kunufaika zaidi, hayo yote yanaangaliwa kwa umakini na tutakapo kuwa tayari, shughuli hiyo itaanza mara moja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kubenea, jibandae Mheshimiwa Mwanne.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongeza swali la nyongeza. Kwa kuwa miongoni mwa viwanda ambavyo vimebinafishwa na Serikali, ni Kiwanda cha Nguo cha Urafiki. Katika Kiwanda cha Nguo cha Urafiki mwekezaji hakuja na mtaji, badala yake Serikali ndiyo ilikwenda kukopa katika Benki ya *Exim* ya China na ikampa mwekezaji mtaji wa kuendesha Kiwanda cha Urafiki. Je, ni lini Serikali itakirejesha Kiwanda cha Urafiki mikononi mwa wananchi wa Dar es Salaam?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kubenea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo umezungumza, Kiwanda cha Urafiki kinatokana na urafiki kati ya nchi ya China na Tanzania. Ni Kiwanda ambacho msingi wake ulijengwa katika mahusiano hayo ya nchi mbili ya Kidiplomasia. Kwa hiyo, tunatamani kuona kiwanda hicho

kikifanya kazi vizuri zaidi na wote tumekifuatilia na kujua kwamba kuna maeneo yanayohitajika kufanyiwa marekebisho. Hivyo, Serikali hizi mbili zinashughulika kwa pamoja kuona ni namna gani kiwanda hicho kitaendelezwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanne.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aomba niulize Serikali, kwa kuwa Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora hakifanyi kazi; na kwa kuwa mpaka sasa kimeiondolea Tabora kupata mapato ya uhakika na vijana kupata ajira: Je, Serikali iko tayari sasa kukinyang'anya na kukirejesha kiwanda hicho Serikalini? Hakifai kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kimsingi Kiwanda hicho kimezungumzwa siku nyingi na mmekuwa mkikifuatilia. Niseme tu kwamba kabla ya kukirejesha kiwanda Serikalini, hatua ya kwanza ni sisi kukitembelea na kujiridhisha, kwa nini hakiwezi kufanya kazi zake inavyopaswa, ikizingatiwa kwamba Tanzania ni nchi ambayo inalima pamba kwa wingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapomaliza Bunge, nitatembelea kiwanda hicho ili kujiridhisha na niweze kutoa ushauri Serikalini juu ya utekelezaji utakaofuata. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa, tanaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi.

Na. 120

Tatizo la Maji Nchini

MHE. AMINA N. MAKILLAGI aliuliza:-

Tatizo la maji linaendelea kuwa kubwa siku hadi siku katika maeneo mbalimbali:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya majisafi na salama vijijini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha inayokabili ujenzi wa miundombinu ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia *programme* ya maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya pili iliyoanza mwezi Julai, 2016, imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kutenga na kutoa fedha za kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika maeneo ya maji Vijijini, Miji Mikuu ya Mkoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo pamoja na Miji na Vijiji vinavyohudumiwa na miradi ya maji ya Kitaifa. Lengo ni kufikia asilimia 85 ya wananchi wanaopata huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya vijijini na asilimia 95 kwa maji mijini ifikapo 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha fedha za ndani zinapatikana za kutosha na kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, Serikali imeanzisha Mfuko wa Maji ambao umekuwa chanzo cha uhakika wa fedha kwa ajili ya miradi ya maji hususan vijijini. Kutokana na jitihada hizo za kutafuta fedha za miundombinu ya maji, hadi sasa

huduma ya maji vijijini imefikia asilimia 64.8 na kwa upande wa mijini imefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha miundombinu ya maji inajengwa katika maeneo mbalimbali na kutoa huduma ya maji kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makilagi. (*Makofi*)

MHE. AMINA N. MAKILLAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana inayoifanya ya kujenga miundombinu ya maji, kiasi cha kufikia kiwango cha asilimia 80 mijini na asilimia 64.8 vijijini, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa sababu Mkoa wa Mara ni Mkoa ambao umezungukwa na Ziwa Victoria na una Mto Mara, Mto Robana, Mto Simiyu na Mto Suguti; lakini Mkoa wa Mara bado ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa majisafi na salama, kwa upande wa vijijini ni asilimia 50.7 na mijini ni asilimia 60. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Swali.

MHE. AMINA N. MAKILLAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mkoa wa Mara ambao unazungukwa na Mito na Miji unapelekewa maji safi na salama na kufikia kiwango ambacho kimetajwa kwenye Ilani ya *CCM*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kuna kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali ya kutafuta fedha na kuwalipa Makandarasi wa miradi ya maji, lakini kwa Mkoa wa Mara tunalo tatizo kubwa sana. Kuna tatizo la kutolipa Wakandarasi. Wilaya ya Serengeti kuna miradi miwili, milioni 500 tayari wamesha-*raise certificate* hawajalipwa; Musoma Vijijini miradi mitatu, tumesha-*raise certificate* bilioni 1.6

hawajalipwa, Serengeti tuna miradi mitatu, shilingi milioni 500 haijalipwa na hata Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha, kwa kuwa tumeshapeleka *certificate*, Wakandarasi waweze kulipwa fedha na miradi iweze kuendelea kwa sababu miradi yote imesimama na sasa ni mwezi wa nne? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Umeona asilimia 70 ya Waheshimiwa Wabunge wamesimama humu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Amina Makillgi, amekuwa ni mtetezi mkubwa sana hususan suala linalohusu haki za huduma ya jamii ikiwemo katika suala zima la maji. Sisi kama Wizara Maji ni jukumu letu kuhakikisha Watanzania wakiwemo wana Mara wanapata majisafi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji, Serikali imefanya jitihada kubwa sana. Ukienda Musoma, zaidi ya shilingi bilioni 45 za mradi mkubwa tumewekeza, kazi iliyobaki ni kwenda kusambaza maeneo ambayo hayana maji wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo sasa hivi, tuna miradi zaidi ya 26 ambayo hivi karibuni tunataka tuitekeleze. Tupo katika hatua ya utangazaji wa *tender* kwa maana ya manunuzi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miji 26 kupitia fedha za India, *dollar* takribani zaidi ya milioni 500 katika miji ya Tarime pamoja na Mgumu kwa kaka yangu Mheshimiwa Ryoba nao watapatiwa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tupo katika hatua za mwisho sasa za kumpata Mkandarasi katika kuhakikisha

tunaanzisha mradi ule mkubwa wa Mgango – Kyabakari mpaka Butiama katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji kwa Mheshimiwa Muhongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa na cha msingi kabisa kuhusu suala zima la kuwalipa Wakandarasi, sisi kama Wizara ya Maji, wapo baadhi ya Wakandarasi wanafanya kazi nzuri. Sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha Wakandarasi wote waliofanya kazi nzuri za kutekeleza miradi ya maji, tutawalipa kwa wakati, lakini kwa wale wababaishaji, lazima tuwashughulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa namwomba Mheshimiwa Makilagi tukutane baada ya saa 7.00 tuone *certificate* zake na tuweze kujiridhisha ili tuweze kuwalipa Wakandarasi wake na wananchi wake wa Mara weweze kupata majisafi na salama na yenye kutosheleza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi, jiandae Mheshimiwa Kiza.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuishukuru Wizara kwa kutuchimbia visima 14, kilichobaki ni ujenzi na uwekaji wa *pump*.

Je, ni lini fedha za kumalizia ufungaji wa *pump* zitaletwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Kapufi kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Alishakuja Wizarani siyo mara moja wala mara mbili katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na uwepo wa chanzo. Tumeshachimba visima vya kutosha. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kapufi, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika utoaji wa fedha ili wananchi wale waweze kutengenezewa miundombinu na waweze kupata majisafi na salama. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiza, mdada wa Kigoma.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Mji mdogo Mwandiga ni moja ya eneo ambalo linakabiliwa sana na changamoto ya kukosa majisafi na salama. Ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi yenu ya kuleta maji ya Manispaa ya Kigoma Ujiji na kufika katika mji mdogo wa Mwandiga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika Mkoa wa Kigoma una jitihada kubwa sana kwa Manispaa ile ya kutekeleza mradi wa zaidi ya *Euro* milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukamilishaji wa mradi huu, sisi kama Wizara ya Maji, tutahakikisha kupeleka maji katika Mji wa Mwandiga. Nataka nimhakikishie ndugu yangu, safari moja huanzisha nyingine. Acha tukamilishe safari hii, lakini safari nyingine tutakamilisha katika kuhakikisha tunapeleka maji Mwandiga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dau.

Waheshimiwa, najua kuna shida ya maji, lakini muda mnauona, saa tano kasorobo na maswali mwisho ni saa nne na nusu.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa. Mradi wa Maji kati ya Kisiwa cha Jibondo ambao una thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili, Mkandarasi ameshaujenga na sasa amefikia asilimia zaidi ya 70. Mradi unatakiwa ukabidhiwe mwezi Machi mwaka huu. Mpaka sasa Mkandarasi hajalipwa hata senti tano na *certificate* zipo Wizaran. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatuhakikishia ni lini sasa Mkandarasi huyo atalipwa ili aweze kumaliza mradi ule?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Kiswaga.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Dau kwa kazi nzuri sana anayofanya kwa wananchi wake wa Mafia na pamoja na Jibondo. Tunatambua kabisa wananchi wa Jibondo wamekuwa na changamoto kubwa sana katika suala zima la maji na hata chanzo cha maji kukosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumeona haja sasa ya kutekeleza mradi mkubwa na tunatambua kazi nzuri aliyofanya Mkandarasi. Nataka nimhakikishie, katika mgao wa mwezi huu Mheshimiwa Mbarawa ameshatenga fedha zaidi ya shilingi milioni 200 katika kuhakikisha tunamlipa Mkandarasi yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwaagiza Mhandisi wa Maji wa Mafia, fedha zile zitakapofika ahakikishe anamlipa Mkandarasi haraka ili asimkwamishe katika suala zima la utekelezaji na wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga. Jiandae Mheshimiwa Silinde.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Kwa kuwa Mji wa Kisesa kulikuwa na mpango wa kuwekwa maji ya bomba pamoja na Vijiji vya Mahaha,

Kabila, Dagalu huko. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafikishia maji wananchi hawa ili waweze kupata huduma hiyo inayostahili? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na jitihada kubwa sana katika Mkoa wa Mwanza katika kutatua tatizo la maji. Kuna utekelezaji wa miradi mikubwa sana Magu, Lamadi pamoja na maeneo mengine. Nataka nimhakikishie; nami kama Naibu Waziri, baada ya Bunge nataka nifike katika Jimbo lake ili twende tuka-*push* miradi ile iweze kukamilika na wananchi wake waweze kupata maji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Silinde, jia ndae na Mheshimiwa Yahya.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kifupi sana. Kwa kuwa Serikali kupitia Hazina ilitenga shilingi bilioni 299.9 katika bajeti yake ya mwaka huu wa fedha na mpaka sasa wametoa shilingi bilioni 1.67 sawa sawa na 0.6; na maji bila fedha ni sawa sawa na hakuna kitu. Kwa hiyo swali langu ni dogo; ipi ni *commitment* ya Serikali kwamba watatoa hizo fedha kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sisi kama Serikali kwamba maji ni uhai na utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha, lakini Serikali imekuwa na vyanzo mbalimbali katika kuhakikisha tunatatua matatizo ya maji.

Moja, tuna Mfuko wa Maji, Bunge lako Tukufu limeidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 158. Nataka nimhakikishie

kwamba mpaka sasa zaidi ya shilingi bilioni 80, tumeshazipata katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hii ni Serikali ya Awamu ya Tano, tunaahidi, tunatekeleza katika kuhakikisha tunamtua mwanamama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la nyongeza. Dhamira njema ya Serikali imeleta mradi mkubwa wa kusambaza maji katika Mji wa Itigi. Wakandarasi walipewa ruhusa ya kuanza mradi ule bila pesa. Je, Serikali iko tayari sasa kuwalipa *certificate* zao ambazo tayari wamesha-*raise* katika Wilaya hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini tunatambua maeneo ya Itigi ni moja ya maeneo yenye changamoto kubwa sana ya maji. Nasi kama Wizara ya Maji tukaona haja sasa ya kuutekeleza mradi ili wananchi waweze kupata maji. Sisi kama Wizara hatutakuwa kikwazo kwa Wakandarasi wenye uwezo na wenye sifa na wanaotekeleza kazi zao vizuri kuwalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutamlipa *certificate* yake ili Wakandarasi waendeleo na kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Saul Henry Amon, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Spika.

Na. 121

**Kurekebisha Miundombinu ya Maji
katika Mji wa Tukuyu**

MHE. DKT. TULIA ACKSON (K.n.y. MHE. SAUL H. AMON)
aliuliza:-

Wilaya ya Rungwe ina vyanzo vingi vya maji ambavyo vinatiririsha maji.

Je, ni lini Serikali itarekebisha miundombinu ili kuongeza kiwango cha maji ambayo kwa sasa hayatoshi kiasi cha kufanya Idara ya Maji kufunga baadhi ya maeneo kama vile Vijiji vya Ibungila, Lubiga na kadhalika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi wapatao 291,176. Huduma ya maji imegawanyika katika maeneo makuu mawili; eneo la kwanza ni huduma ya maji Mjini Tukuyu inayotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu na eneo la pili ni huduma ya maji vijijini inayotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la mijini, watu wapatao zaidi ya 32,074 wanapata huduma ya maji kati ya watu 50,000 sawa na asilimia 63. Katika maeneo ya vijijini, watu wapatao 157,750 wanapata huduma ya maji kati ya watu 240,250 sawa na asilimia 55.7. Vyanzo vya maji vinavyotegemewa na wananchi wa Rungwe ni vijito, mito na chemchemi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Ibungila na Lubiga vilikuwa vinapata huduma ya maji kutoka katika mradi wa maji wa Mji wa Tukuyu, uliojengwa tangu mwaka 1984 ambapo kuanzia mwaka 2002 unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa watu na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji, kwa sasa huduma ya maji katika Vijiji vya Ibungila na Lubiga haipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji katika Mji wa Tukuyu ambao katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetoa shilingi milioni 3,087 kupitia Mamlaka ya Maji Mjini Tukuyu ili kuongeza upatikanaji wa maji. Fedha hizo zitafanya kazi ya ujenzi wa *tank* lenye mita za ujazo 200 na kukarabati mtandao wa bomba kilomita tisa. Utekelezaji wa mradi huo unaendelea. Hadi sasa ujenzi wa *tank* umekamilika na bomba za inchi sita zenye jumla ya urefu wa mita 750 zimelazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utekelezaji wa mradi huu kukamilika vijiji vya Ibungila na Lubiga vitaweza kupata huduma ya maji kutokana na ukarabati unaoendelea kufanyika hivi sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Tulia. Jiandae Hussein Bashe.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yanayoonesha kwamba sasa Vijiji vya Ibungila na Lubiga vitapata maji kupitia mradi huu, upo mradi wa *Masoko Group* ambao umesuasua kwa muda mrefu, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie ni lini mradi huu utakamilika ili wananchi wa vijiji vya Kata ya Masoko waweze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, uchakavu wa miundombinu katika Kata mbalimbali za Mbeya Jiji hususan Kata ya Ilomba, Mtaa wa Hayanga – Ituha, Tonya na

Ihanda, Kata ya Iganjo Mtaa wa Igodima na Mwambenja, Kata ya Iyunga Mtaa wa Sistila, Kata ya Ghana Mtaa wa Magharibi na Mashariki, Iganjo Mtaa wa Iganga na Igawilo Mtaa wa Sokoni na Chemi: Ni lini Kata hizi zitapelekewa miradi ili ziweze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Tulia kwa kazi nzuri sana anayoifanya na katika kuhakikisha anawatetea wananchi waweze kupata maji. Kubwa sana ni kuhusu suala zima la kusuasua kwa mradi wa maji wa *Masoko Group*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, nilifanya ziara katika eneo lile la *Masoko Group* na tukaona usuaji wa mradi ule, tukaagiza timu ya Wizara ili iweze kufika na kuongeza nguvu katika kuhakikisha mradi ule unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Naibu Katibu Mkuu Engineer Kalebelo, alifika na timu ya Wizara pale na wakazungumza na Mkandarasi na wakampa mikakati mpaka sasa asilimia 60 ya mradi umeshakamilika na wananchi wa Mpera gwasi na Nsanga sasa hivi wanapata maji safi na salama na ya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji tutahakikisha tunausimamia mradi ule kwa dhati kabisa ili uweze kukamilika na vijiji takribani 15 vilivyopangwa kunufaika, viweze kunufaika na mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Mheshimiwa Mbunge hii ni wiki ya pili ananiulizia swali la maji katika Jiji la Mbeya. Nataka nikuhakikishie, ukimwona

mtu mzima analia, ujue kuna jambo. Hivyo, katika wiki ya kwanza tuna maswali mawili katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari sasa kukutana na wataalam wetu wa Jiji la Mbeya kwa maana ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mbeya ili tujipange ni namna gani tunaweza tukapeleka maji kwa haraka katika maeneo ambayo ameyasema ya Ilomba, Iganzo, Iyumba, Ghana na Iganjwa.

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. Mheshimiwa Bashe. Ni saa tano sasa, naomba radhi sana Waheshimiwa. Najua umuhimu wa maji, lakini naomba radhi sana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa mradi wa maji wa Ziwa Victoria na mradi wa visima 25 katika Jimbo la Nzega, sasa nilitaka nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutupatia *commitment* Halmashauri ya Mji wa Nzega kupatiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.2 katika mwaka wa fedha unaokuja ili kukamilisha mradi wa maji katika Vijiji vya Mhogola, Monyagula, Migua, Itangili, Igilali, Mwanzoli na Kitengwe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, anaomba tu hiyo pesa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kifupi kwanza, nimpongeze Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo lake la Nzega, lakini kubwa tunatambua utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha, nimwombe basi tukutane mimi na yeye, pamoja na Wataalam wetu wa Wizara, tuangalie namna gani tunaweza tukasaidiana. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema.

Na. 122

Umuhimu wa Nishati Mbadala Itokanayo na Jua

MHE. GODBLESS J. LEMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kunufaika na nishati mbadala itokanayo na jua hasa, katika mikoa yenye ukame unaosababishwa na jua kali kwa kutengeneza *Solar Village* na kuunganisha nishati hiyo kwenye Gridi ya Taifa?

MWENYEKITI: Hii Mheshimiwa ni *solar village* au ni *solar field*? Kitaalam...

MHE. GODBLESS J. LEMA: *Solar village*.

MWENYEKITI: Sio *field*?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Hapana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza Mradi wa Nishati Endelevu kwa Wote (*Sustainable Energy for all – SE4ALL*) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*).

Kazi zilizofanyika hadi kufikia Disemba, 2018 ni pamoja na uhakiki wa kubainisha sehemu zinazofaa kwa uzalishaji wa nishati ya umeme-jua katika maeneo ya Same (Kilimanjaro) Zuzu (Dodoma) na Manyoni (Singida). Ili kuwa na uhakika wa uwezo wa kuzalisha umeme katika maeneo hayo, Serikali kupitia *TANESCO* imeanza kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* imeanza kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme-jua wa *MW 150* katika Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 375.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mshauri Mwelekezi anatarajia kukamilisha upembuzi yakinifu mwezi Machi, 2019. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2019 na kukamilika mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa miradi hii, Serikali kupitia *TANESCO* mwezi Oktoba, 2018, ilitangaza zabuni kwa ajili ya kupata wawekezaji binafsi watakaozalisha umeme. Kampuni 52 zimeonesha nia ya kuzalisha umeme kutoka chanzo hicho na hivi sasa, *TANESCO* wanafanya uchambuzi kwa ajili ya kupata Kampuni ya kuzalisha umeme *MW 150* kutoka vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu pamoja na umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ripoti ya *UNDP* inatahadharisha kwamba vita nyingine ya ulimwengu katika siku zinazokuja itakuwa ni maji, pamoja na chakula na kwa sababu, umeme unaotumia mionzi ya jua umethibitika kote ulimwenguni kwamba ni umeme muafaka, ni kwa nini Serikali sasa isi-*concentrate* kwenye umeme huu, ambao katika Taifa letu la maeneo mengi sana, ambao ni *almost...*

MWENYEKITI: Swali Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Swali langu ni kwa nini Serikali isi-*concentrate* sasa, kwenye umeme huu na ikaachana na umeme wa maji ambao sehemu kubwa inakwenda kuleta uharibifu wa mazingira.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godbless Lema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake, amejielekeza, kwa nini Serikali isijielekeze zaidi kwenye umeme huu, unaotokana na jua, kwenye jibu letu la msingi tumeainisha jitihada ambazo Serikali imefanya. Tumesema kutokana na *Power System Master Plan* yetu kwamba tunatakiwa tuzalishe zaidi ya *MW 350* kwenye *Power System Master Plan* na nikaeleza kwamba hata kazi yenyewe imeanza, *TANESCO* wametangaza *Tender* kwa ajili ya *MW* zaidi ya 200 kwenye upepo na 150 kwenye jua, lakini ukiacha mradi huu wa Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imejielekeza kuhakikisha kwamba nishati jadidifu ina mchango mkubwa katika kuzalisha umeme, licha tu ya kwamba umeme wa jua, lakini kuna umeme wa makaa ya mawe ambao tumetangaza wa *MW 600*, licha ya huo pia umeme unaotokana na jotoardhi, tunatarajia kuzalisha *MW 200*, katika kipindi hiki, hii *Power System Master Plan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile amesemea kwenye miradi ya maji, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, tafiti zimefanyika za kina kuainisha *sustainability* ya miradi yote ya umeme inayotokana na miradi ya maji, lakini kwa kutambua miradi ya umeme, inayozalishwa kwa maji na gharama nafuu, zaidi zinatumiwa shilingi 36 kulinganisha na umeme wa upepo ambao ni shilingi 103; umeme wa jua, shilingi 103 kwa *per unit kilowatts*; lakini pia umeme unaotokana na makaa ya mawe 108. Kwa hiyo masuala haya ni zaidi kulinganisha gharama kwa sababu nia ya Serikali ni kumpatia Mtanzania umeme wa gharama nafuu na wa uhakika. Ahsante sana.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa, si tunaanza wageni kwanza.

Waheshimiwa muda wetu umekwisha, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wageni wawili wa Mheshimiwa Angelina Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni Viongozi wa Taasisi ya Kilimo cha Biashara ya Mihogo (*CAPAFO*) kutoka Ilemela Jijini Mwanza, Mwenyekiti Ndugu Dennis Kankono na Katibu Ndugu Emmanuel Kubambala, karibuni. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa January Makamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambao ni wasanii kutoka kikundi cha Lizombe *one Band* cha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ismail Mahoja. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Arusha, wakiongozwa na mdogo wake Ndugu Iddy Migilla (*Makofi*).

Wageni sita wa Mheshimiwa Sonia Magogo ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na kaka yake Ndugu Edwin Magogo. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Kiza Mayeye ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Rehema Mayeye. (*Makofi*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoa wa Rukwa wakiongozwa na Ndugu Veronica Nelson. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ambao ni marafiki zake kutoka Mkoani Arusha Ndugu Lucas Paschal na Ndugu Maximillian Lumalanja.

Wageni watano wa Mheshimiwa Makame Mashaka Foun ambao ni Viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Kijini, Mkoa wa Kaskazini Unguja wakiongozwa na Katibu wa CCM Jimboni Ndugu Aziza Muhamed. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Anastazia Wambura ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Katekista Kigango cha Maria De Mathias Ndugu Romanus Masululi. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zainab Bakar ambao ni ndugu zake kutoka Kusini Pemba Ndugu Abdulmatham Mussa na Ndugu Asya Othman Nassor. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Phillip Mulugo ambaye ni dada yake kutoka Mkoani Mbeya Ndugu Emiliana Barnabas. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ambao ni viongozi wa Chama cha Wavuvi Tanzania chenye Makao Makuu yake Jijini Mwanza, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi Ndugu John Bunyanya. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Aeshi Hillary ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Vijana la CCM, Mkoa wa Rukwa Ndugu Juma Abdallah. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Haydom, Ndugu Swai Sheriwandui na Diwani wa CCM Kata ya Geterer Mheshimiwa Luri Peter wanaotokea Mbulu Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mbarouk Bawazir ambao ni wanafunzi 65 na Walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Dakawa iliyopo Kilosa Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 33 kutoka Chuo cha Elimu cha Biashara (CBE) kilichopo Mkoani Dodoma. (Makofi)

Wanafunzi 85 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya St. Monica iliyopo Jijini Arusha wakiongozwa na Ndugu Samwel Laizer. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Hamoud, wapo watatu kutoka Wilayani Jimboni Kibaha ambao ni Ndugu Mapunda na Ndugu Abdallah.

MWENYEKITI: Katibu.

MWONGOZO

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa subiri, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista Mhagama.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushuru kwa kunipa nafasi kabla hujaendelea na hiyo hatua ya pili ya Miongozo ili niweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge ulioanza tarehe 29 Januari, 2019, umepangwa kumalizika tarehe 8 Februari, mwaka 2019;

NA KWA KUWA Kamati ya Uongozi ilikutana tarehe 6 Februari 2019 kupokea na kujadili hati ya dharura ya Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria Mbalimbali

(Na. 2) wa mwaka 2019 yaani *(The Written Law Miscellaneous Amendments (No. 2) The Bill, 2019)*;

NA KWA KUWA Muswada huo, unarekebisha Sheria tano muhimu, ili kuondoa upungufu uliodhihirika wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo;

NA KWA KUWA Kamati ya Uongozi katika kikao chake iliridhia kwamba Mkutano huu wa Kumi na Nne wa Bunge uliopangwa kumalizika tarehe 8 Februari, uendelee mpaka tarehe 9 Februari, 2019;

NA KWA KUWA tarehe 9 Februari, 2019 ni siku ya Jumamosi ambapo Kanuni ya 28(15) inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko.

HIVYO BASI naomba kwa heshima kubwa kuleta ufanisi katika kutekeleza na kuboresha utekelezaji bora wa shughuli za Bunge, naomba Bunge lako liliridhie Kanuni ya 28 (15) iweze kutenguliwa ili kuruhusu siku ya Jumamosi yaani tarehe 9 Februari, 2019, itumike kwa ajili ya Vikao vya Bunge isipokuwa kwamba katika siku hiyo Bunge litaanza saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Hoja imeunga mkono, Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Kanuni hii inatenguliwa na Bunge kesho lifanye kazi kwa mujibu wa mapendekezo ya Serikali kuanzia saa tatu mpaka saa nane mchana.

Mheshimiwa Mchengerwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Taifa likiadhimisha karibu miaka 58 ya uhuru na ukombozi wa Taifa letu, Uhuru ulioambata na hali kadhaa za kibinadamu zilizoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa sasa Serikali inafanya mambo mazuri ya ulinzi wa watoto wetu kule Mkoa wa Njombe zipo picha zinazosambaa katika mitandao ya kijamii, zikimuonesha mzungu anayetambulika kwa jina la la Hilgan Brusma akiwavua watoto nguo na kuwachapa viboko wakiwa uchi wa nyama katika Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe mwongozo wako, kwa kuwa tukio hili limetokea; na kwa kuwa kesi za jinai hazina mipaka ya *limitation* niombe Mwongozo wako kwa kupitia Kanuni ya 5 kwa Mamlaka uliyonayo lakini pia kwa kupitia Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utoe maelekezo kwa Tume ya Haki Binadamu kulifuatilia tukio hili, lililotokea kule Siha linalotukumbusha nyakati za mkoloni, nyakati za utumwa ambazo ni machungu makubwa kwa Watanzania wa nchi hii, utoe maelekezo kwa kupitia Kanuni ya 5 ili Tume ya Haki za Binadamu iweze kufatilia na kutuletea taarifa katika Kamati ya Katiba na Sheria ambayo ndiyo Tume inawajibika kwenye Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Nimeshakuita Mheshimiwa Haonga. Mheshimiwa Haonga akili yako iwepo Bungeni, nilishakuita, sasa bado unauliza nini tena, toa Mwongozo wako.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kumekuwa na utamaduni kwamba tukichangia hotuba mbalimbali au tukichangia labda Kamati tunaletewa michango yetu kwa maandishi ili tuweze kufanya marekebisho na baada ya hapo inapelekwa *Hansard*. Kwa bahati mbaya sana siku za hivi karibuni Wabunge tumekuwa tukichangia hatujaona kitu kama hicho, sasa nataka nijue utaratibu huu kwa nini umeanza kuondolewa kimya kimya bila kujua na bila taarifa rasmi, hakuna tangazo lolote na hamna taarifa yoyote ile, je, hii sio hujuma kwa Bunge lako? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwongozo wangu ni kama ifuatavyo: Katika kipindi cha maswali na majibu, tunapouliza maswali sisi Wabunge naamini tunauliza kwa niaba ya wananchi wote bila kuzingatia itikadi, lakini Waheshimiwa Mawaziri wanapojibu swali likiulizwa na Mpinzani hatoi pongezi, kwamba nampongeza Musa Mbarouk kwa kufanya moja, mbili, tatu, kwa jimbo lake, lakini likiulizwa na mtu wa CCM hata kama huyo Mbunge wa CCM hajakwenda hata siku moja ofisini kwa Waziri, Waziri anaenda kusema, nampongeza Mbunge fulani, kwa bidii za kuwatetea wananchi. Hiyo siyo sawa. Tupendaneni japo kinafiki. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7), katika maswali tuliyokuwa tunauliza hapa, asubuhi ya leo, hasa kwenye Wizara ya Maji, majibu yametolewa sana hapa lakini ukiangalia hali halisi, hali si nzuri sana, *certificate* nyingi sana hazijalipwa na Wakandarasi wengi sana wanadai. Naomba mwongozo kwamba, kwa nini Serikali isije na hoja mbadala ya kusaidia hata tuweke Sh.50 ili tatizo la maji likaadoka maeneo haya yote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Miongozo minne, wa Mheshimiwa Mchengerwa ambalo linahitaji ku-*consult* na Serikali, kwa hiyo tupe muda tuwape Serikali walifanyie kazi na watatupa majibu.

Mheshimiwa Haonga, kuhusu marekebisho ya michango yenu hamjaipata, tutafuatilia *hansard* na tutakupa jibu.

Mheshimiwa Mbarouk, leo nilimsikia Waziri hapa anampongenza Mpinzani, tena nafikiri alikuwa anampongeza Mheshimiwa Selasini. (*Makofi*)

Kwa hiyo, haya mambo yanatokea, kupongeza, saa zingine mnakuwa *busy* sana na mambo yenu binafsi mnashindwa kuelewa Serikali inavyojibu. Serikali hii haibagui mtu, inatetea na inasifia kila pande kwa sababu miradi hii ya Serikali, hawawezi kusema hampongezwi.

Mheshimiwa Flatei suala lako tumelipokea, tutawapa wahusika, sababu tunajua maji ni uhai, hili Serikali imelisikia mlifanyie kazi, *certificate* ambazo hazijalipwa sasa zifanyiwe mpango zilipwe na mapendekezo aliyoyatoa ya kuongeza makato fulani ili Serikali iweze kulipa. Kwa hiyo nawashukuru wote. Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018 na

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetuwezesha kuwepo katika Bunge hili Tukufu kwa kuwa hii ni nafasi hii adhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza sana kwa kuchapa kazi kwa maendeleo ya Taifa letu pamoja na Makamu wa Rais. Vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo Kamati yetu inasimamia Ofisi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kama nilivyosema namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati na Sekretarieti kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kusoma taarifa hii, napenda kumpongeza sana Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Michango na ushauri wake akiwa Mjumbe wa Kamati viliongeza ufanisi wa Kamati kwa muda wote alipokuwa kwenye Kamati hii, hivyo tunamtakia utumishi uliotukuka katika dhamana kubwa aliyopewa na Mheshimwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta ikiwemo Kamati ya Katiba na Sheria zina wajibu wa kuwasilisha taarifa za mwaka za shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019 na imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo:- Sehemu ya kwanza, inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa; sehemu ya pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati; sehemu ya tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na sehemu ya nne ni hitimisho la taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa. Katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayozitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia ambapo Kamati ilitembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(ii) Kuchambua Miswada ya Sheria. Kwa mujibu wa Kanuni ya 84 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, kifungu cha 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati hii ilishughulikia jumla ya Miswada ya Sheria minne (4) iliyofanya marekebisho katika jumla ya sheria 24 zinazohusu sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2018 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018] ambao ulifanya marekebisho katika sheria 13 kwa lengo la kuboresha mfumo wa kisheria nchini.

(b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2018 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018] ambao ulifanya marekebisho katika sheria sita (6) ili kuondoa mapungufu ambayo yalibainika katika utekelezaji wa sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa taasisi inayosimamia utekelezaji wa sheria hizo.

(c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2018 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2018] ambao ulifanya marekebisho katika sheria nne (4) ili kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria husika.

(d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 [The Political Parties (Amendment) Bill, 2018] ambao ulilengwa kuimarisha utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kulpa mamlaka zaidi ya kuratibu na kusimamia kwa ufanisi zaidi uanzishwaji na utekelezaji wa majukumu ya vyama vya siasa nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria nyingine nchini.

(iii) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara. Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili taarifa nane (8) za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazosisimamia pamoja na taasisi zake, ambapo, taarifa hizo ziliwasilishwa na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Katiba na Sheria kama inavyoonekana katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa kina kuhusu sehemu ya kwanza ni kama ilivyoanishwa katika ukurasa wa 1 - 9 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi wa kina kwa masuala yaliyobainishwa na Kamati katika sehemu hii ni kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 9 - 38 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango ya kuwajengea uwezo wakiuchumi vijana kwa kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Kamati ilibaini kuwa, kwa mwaka wa 2017/2018 na 2018/2019, Mfuko huu umekuwa ukitengewa kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2017/2018, jumla ya shilingi bilioni 2.7 zimetolewa kwa vikundi vya vijana 523 vyenye idadi ya vijana 3,781 katika Halmashauri 127 ambazo ni sawa na takribani asilimia 70% ya Halmashauri 184 zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kubaini mafanikio mbalimbali ya Mfuko wa Vijana kama vile ufanisi wa baadhi ya vikundi vya vijana kutoka uzalishaji mdogo kwenda uzalishaji mkubwa na hivyo kupunguza tatizo la ajira na umaskini kwa vijana, bado kumbainika kuwepo kwa changamoto mbalimbali hususani dosari za kiusimamizi katika baadhi ya Halmashauri nchini. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu inaainisha kuwa, baadhi ya Halmashauri za Wilaya zimeshindwa kabisa kuendelea kuzilea na kuzisimamia vizuri SACCOS za vijana ili ziendeele kukua na kutoa huduma stahiki kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari hii ya kiusimamizi imesababisha kuwepo kwa SACCOS za vijana ambazo zimekuwa zikitumia fedha za mikopo kwa matumizi mengine yasiyokusudiwa, pamoja na changamoto ya uwepo wa migogoro miongoni mwa SACCOS za vijana na hivyo kuathiri ukuaji na maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Miswada ya sheria. Katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Miswada minne (4) ya kissekta iliyofanyia marekebisho katika jumla ya sheria 24. Kamati ilichambua kwa weledi na umakini Miswada hiyo na kuwasilisha maoni na ushauri wake katika Bunge ambapo yote iliridhiwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilibaini kuwa, miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za ndani na fedha hizo zimepatikana kwa wakati. Aidha, ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya *MOLADI* ni mfumo wa gharama nafuu na unakamilisha ujenzi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu na ukomo wa bajeti kwa taasisi ambazo Kamati inazisimamia. Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mafungu yote (Fungu 26 na Fungu 31).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina mafungu sita ya kibajeti. Kamati ilibaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 jambo ambalo likiendelea linaweza kukwamisha utekelezaji wa maendeleo ya nchi hasa ukizingatia unyeti wa ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria. Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kamati inaipongeza Hazina na

Serikali kwa ujumla kwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyo dhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina na mafunzo. Katika Kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019, Kamati ilipatiwa Semina na mafunzo kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa *Legislative Support Program (LSP II)* na asasi mbalimbali za kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kujengea Kamati uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria hususan masuala ya msingi katika hatua ya uchambuzi wa Miswada. Orodha ya taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika taarifa hii. Kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe na Sekretarieti wamejengewa uwezo na uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kiseria na kisheria na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za mazingira wezeshi ya watu wenye ulemavu. Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto za uwekaji wa mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, wakati Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010 inatamka kuanzishwa kwa Baraza pamoja na Mfuko wa Watu wenye Ulemavu, bado kumekuwepo changamoto kuhusu utekelezaji wa matakwa hayo ya kisheria kwa lengo la kuwajengea mazingira wezeshi watu wenye ulemavu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa, ili kuweka mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu, wakati umefika ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie kikamilifu utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu na Kanuni zake, kwa kuainisha masuala ya watu wenye ulemavu kuwa sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu. Mapendekezo ya Kamati; masuala ya watu wenye ulemavu.

Kwa kuwa, watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii ya Watanzania na hivyo wanahitaji kuwekewa mazingira wezeshi ili waweze kujikwamua kwa maendeleo endelevu; na kwa kuwa, Serikali inatambua na imezingatia haki mbalimbali za watu wenye ulemvau kupitia Sheria na Mikataba ya Kimataifa; hivyo Basi, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha na kutangaza Wajumbe wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu,

(b) Kuanzisha na kutenga fedha za kifungu (kasma) ya masuala ya Watu wenye Ulemavu,

(c) Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu kama ilivyoanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na

(d) Kuweka usimamizi mzuri wa fedha za Watu wenye Ulemavu kwa kuhakikisha fedha hizo zinatengwa kwa kila Halmashauri na zinawafikia walengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa fedha za Mfuko wa Mendeleo ya Vijana. Kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya vijana nchini; na kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zenye kuathiri ufanisi wa Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana; hivyo basi, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

(a) Kuongeza usimamizi wa fedha za Mfuko kwa lengo la kuimarisha SACCOS zilizopo na kudhibiti SACCOS hewa za Vijana ambazo hukopeshwa na kupokea fedha za Serikali. Hii ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa na ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambao ndiyo wenye dhamana na Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inawajibika kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana na kusimamia marejesho kwa wakati.

(b) Kupanua wigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kuanza kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali ya vijana nje ya *SACCOS* kwa kuwa siyo vijana wote ni marafiki wa *SACCOS* kutokana na masharti magumu ya uendeshaji wa baadhi ya *SACCOS* nchini hatua ambayo huwa kizuizi kwa vijana wengi kuzifikia fursa za fedha. Hii ni pamoja na vikundi vya vijana vilivyosajiliwa na vyenye mipango ya miradi yenye lengo la kuongeza ajira, *CBOs* na makampuni yaliyosajiliwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya kati na mikubwa ya kutoa ajira nyingi kwa vijana.

(c) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, waandae ziara ya kikazi ambapo Kamati itatembelea na kukagua vikundi/*SACCOS* za vijana ambazo zimenufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Kamati iweze kujionea hali halisi na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi zaidi kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo changamoto za kiutendaji kwa baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; na kwa kuwa, changamoto hizo ni vyema zikatafutiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi zaidi kwa taasisi hizo; hivyo basi, Kamati inaishauri yafuatayo:-

(a) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*WCF*) ujipange na kuwa na Mkakati ambao utahakikisha unakwenda sambamba na ongezeko kubwa la waajiri wapya kutokana na kuongezeka kwa uanzishwaji wa viwanda nchini pamoja na mahitaji ya matumizi ya *TEHAMA* katika kuwahudumia wadau wengi kwa wakati na kwa ufanisi zaidi. Hii inatokana na ukweli kuwa, hadi kufikia Septemba, 2018 kulikuwa na jumla ya biashara zilizosajiliwa (*Registered Business Entities and Institutions*) 28,625 nchini ambazo zingestahili kujisajili katika Mfuko kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mamlaka ya Usalama Mahali pa Kazi (*OSHA*) iongeze mikakati ya usajili na usimamizi wa afya na usalama katika maeneo ya kazi kulingana na ongezeko la viwanda nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi

kulingana na vipaumbele vya wakala huo kwa wakati husika.

(c) Serikali ione umuhimu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya wale wafanyakazi wa mikataba ambao mikataba yao ilikuwa bado inaendelea kwenye Mifuko ya Pensheni iliyounganishwa lakini hawajaweza kuendelea na ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa utoaji wa haki nchini. Kwa kuwa, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati; na kwa kuwa, usimamizi wa utoaji wa haki nchini unategemea sana ufanisi wa taasisi husika zenye dhamana hiyo; hivyo basi, Kamati inashauri taasisi husika zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

(a) Mahakama iendelee kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake iliyojiwekea wa kuhakikisha kila Hakimu na Jaji anashughulikia na kukamilisha idadi ya mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya wananchi kwa chombo hiki cha utoaji wa haki nchini.

(b) Serikali iandae na kutekeleza Mkakati Endelevu wa kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kutoka taasisi mbalimbali za umma, hasa uwezo wa kufanya majadiliano, uandishi na uchambuzi wa mikataba ya kiuwekezaji na uwezo wa kuelewa na kutetea maslahi ya nchi katika Mahakama/Mabaraza ya ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itaiwezesha Serikali kuwa na rasilimali watu wenye uwezo wa kulinda na kutetea maslahi ya nchi katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi. Aidha, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zihakikishe zinaendelea kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje katika kutafuta nafasi za kuwajengea uwezo na uzoefu Mawakili wa Serikali kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaaluma vinavyohitajika kwa wakati husika.

(c) Serikali iajiri idadi ya watumishi wa kutosha chini ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Serikali iandae na kutekeleza mpango endelevu wa kuwajengea uwezo Mawakili/Wanasheria na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili waweze kusimamia na kuendesha mashauri ya haki jinai kwa ufanisi zaidi.

(d) Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge iandae na kuratibu mafunzo kwa Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili Wajumbe wake wawe na uelewa wa pamoja kuhusu majukumu ya Tume na mipaka yake kwa lengo la kuishauri Serikali ipasavyo. Hii ni pamoja na Wizara husika kuona umuhimu wa kuishirikisha Kamati katika hatua za awali za uandaaji Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu nchini ili Kamati ipate fursa ya kutoa mawazo na hivyo kwenda sambamba wakati wa utekelezaji.

(e) Serikali iendelee na jitihada zake za kuchukua hatua madhubuti katika udhibiti wa uvunjaji wa haki za makundi maalum kama vile watu wenye ulemavu wa ngozi, wazee, wasichana wanaosafirishwa nje ya nchi kwa biashara haramu lakini kwa mgongo wa kwenda kufanya kazi za nyumbani pamoja na udhalilishwaji wa haki za watoto wa mitaani kwenye vituo vya mabasi vya mikoa na maeneo mengine nchini.

(f) Serikali iandae na kutekeleza Mpango Mkakati chini ya Magereza ambao utahakikisha wafungwa wenye ndoa wanawekewa mazingira yatakayohakikisha wanapata haki ya kutembelewa na wenzi wao na kupata haki ya tendo la ndoa kwa kuzingatia utaratibu utakaowekwa na mamlaka husika. Hatua hii itapunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali magerezani hususan UKIMWI. *(Makofi)*

(g) Serikali iendelee kuboresha Bajeti ya Fungu 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi katika mwenendo wa bajeti za Serikali. Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa, kumekuwepo ongezeko la upatikanaji wa fedha za ndani ukilinganisha na upatikanaji usioridhisha wa fedha za nje, kwa mwenendo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha 2017/2018; na kwa kuwa, hatua hii ya kutumia fedha za ndani kuendeshea mipango ya nchi inapunguza utegemezi wa kiuchumi na ni ya uhakika zaidi; hivyo basi, Kamati inashauri kuwa:-

(a) Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali nchini badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

(b) Serikali kupitia vyombo husika, ibuni vyanzo vipya vya mapato vyenye uhakika na endelevu.

(c) Elimu ya kulipa kodi iendelee kutolewa kwa wananchi ili kila Mtanzania aone umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina na mafunzo kwa kamati. Kwa kuwa, Programu ya Utekelezaji wa Mradi wa *LSP II* chini ya *UNDP*, imekuwa msaada mkubwa sana katika kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hii kuhusu masuala mbalimbali katika uchambuzi wa miswada; na kwa kuwa, Kamati hii ina jukumu la kuchambua na kujadili Miswada mingi ya Sheria za Marekebisho ya Sheria mbalimbali ambazo zinagusa sekta mbalimbali nchini; na kwa kuwa, bado mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge na Sekretarieti ili kupanua wigo wa uelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya mwisho hiyo, malizia;

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba:-

(a) Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Waratibu wa Mradi wa LSP II waone umuhimu wa kuandaa na kuratibu mafunzo ya Kamati hii ndani na nje ya nchi kuhusu masuala ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria na Bajeti za Serikali (*Bills and Budget Scrutiny*) kwa lengo la kuongeza weledi kwa Wajumbe wa Kamati hii na Sekretarieti yake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mradi huu...

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako umekwisha, mengine yataingia kwenye *Hansard*.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Yaingize kwenye *Hansard* maneno yako yote.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yote ambayo nimeyaruka kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho naomba yaingie kwenye *Hansard*.

MWENYEKITI: Ahsante.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA
KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI
CHA KUENZIA JANUARI 2018 HADI JANUARI 2019
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka, kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusoma Taarifa hii, napenda kumpongeza sana Dkt. Damas Daniel Ndumbo (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Michango na ushauri wake akiwa Mjumbe wa Kamati viliongeza ufanisi wa Kamati kwa muda wote alipokuwa kwenye Kamati hii, hivyo tunamtakia utumishi uliotukuka katika dhamana kubwa aliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta ikiwemo Kamati ya Katiba na Sheria zina wajibu wa kuwasilisha Taarifa za Mwaka za shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo:-

- a) **Sehemu ya Kwanza** inatoa Maelezo ya Jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;
- b) **Sehemu ya Pili** inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- c) **Sehemu ya Tatu** inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- d) **Sehemu ya Nne** ni hitimisho la taarifa.

1.2 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6 (2) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambayo, imepewa jukumu la kusimamia Wizara Tatu ambazo ni:-

- a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano),
- b) Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, na
- c) Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati hii ni:-

- a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.3 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati za Kudumu za Bunge ni Mawakala wa Bunge na hivyo hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Kamati za Kudumu za Bunge huliwakilisha Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zenye kukidhi matakwa ya Katiba na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Njia hizo ni:-

a) Vikao vya uchambuzi wa Bajeti za Serikali kwa Wizara na Taasisi inazosisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

b) Vikao vya kushughulikia Miswada ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

c) Kupokea maoni ya Wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

d) Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoishia kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake, kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotengwa na kupokelewa na Taasisi husika; na

e) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara na Taasisi inazosisimamia kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge,

f) Kuwataka Mawaziri wafafanue na kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;

g) Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge.

h) Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge.

1.4 Shughuli zilizotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1.4.1 Kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayozitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilitembelea na kukagua Miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi 2018. Miradi hiyo ya Maendeleo iliyotembelewa ipo katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Wilaya ya Chato katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

1.4.2 Kuchambua Miswada ya Sheria;

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati hii ilishughulikia Jumla ya Miswada ya Sheria Minne (4) iliyofanya marekebisho katika Jumla ya Sheria Ishirini na Tano (25) zinazohusu Sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) *Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2018(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018.*

1.0 Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria 13 zifuatazo:

- (i) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27
- (ii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20
- (iii) Sheria ya Kubadilishana Wafungwa, Sura ya 368,
- (iv) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1
- (v) Sheria ya Ukomo, Sura ya 89
- (vi) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171
- (vii) Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254
- (viii) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430
- (ix) Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Utekelezaji wa Majukumu yake, Sura ya 268
- (x) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329
- (xi) Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19

(xii) Sheria ya Kuhusu Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256

(xiii) Sheria ya Chama cha Mwakili Tanganyika, Sura ya 307

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo katika Mfumo wa Taasisi za Sheria nchini ulitokana na **Hati Idhini iliyochapishwa katika Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018**, ambapo Serikali ilifanya mabadiliko katika Mfumo wa Kisheria (Legal Regime) nchini yenye kuweka au kuanzisha Mfumo mpya wa uwakilishi na utetezi wa Serikali na Taasisi zake zote katika masuala ya Kisheria ndani na nje ya nchi.

Hivyo, kutokana na mabadiliko hayo, Mfumo wa Sekta ya Sheria nchini kupitia Ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zilihitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia mabadiliko hayo ya kimfumo kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji miongoni mwa taasisi husika kupitia vifungu mbalimbali vya Sheria.

b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na.3 wa Mwaka 2018 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018]

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2018 ulifanya marekebisho katika Sheria Sita (6) zifuatazo:-

(i) Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura ya 141,

(ii) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33,

(iii) Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216,

(iv) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11,

(v) Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49 na

(vi) Sheria ya Takwimu, Sura ya 351.

Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Sita (6) husika ili kuonda mapungufu ambayo yalibainika katika utekelezaji wa Sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo. Aidha, marekebisho hayo yalilenga kuziwezesha Sheria husika kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kiteknolojia, kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyojitokeza na yenye athari katika utekelezaji wake.

c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2018 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2018]

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Nne (4) ambazo ni:

(i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Sura ya 288,

(ii) Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225,

(iii) Sheria ya Pasipoti na Hati za Kusafirira, Sura ya 42, na

(iv) Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364.

Madhumuni ya marekebisho ya Sheria hizo ni kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria husika.

d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 [The Political Parties (Amendment) Bill, 2018]

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanaimarisha Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuipa Mamlaka zaidi ya kuratibu na kusimamia kwa ufanisi zaidi

uanzishwaji na utekelezaji wa Majukumu ya Vyama vya Siasa nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa weledi na umakini Miswada hiyo na kuwasilisha Maoni na Ushauri wake katika Bunge lako ambapo yote yaliridhiwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria za nchi.

1.4.3 Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kifungu cha 6(2)(a) na(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(d) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili Taarifa Nane (8) za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake, ambapo, Taarifa Nne (4) ziliwasilishwa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taarifa nne (4) kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama ifuatavyo:-

a) Taarifa Nne (4) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu:-

(i) Utekelezaji wa Mpango wa kuwajengea Uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana,

(ii) Takwimu za mwenendo wa Waajili katika kujiandikisha kwenye Mfumo na Ulipaji wa Michango stahiki kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (Workers Compensation Fund-WCF) kwa mujibu wa Sheria,

(iii) Hatua zinazochukuliwa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) katika kulinda usalama wa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama vile Migodini na Viwandani, na

(iv) Hatua iliyofikiwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) katika kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa kuzingatia Matakwa ya Sheria ya The Public Service Social Security Fund Act (No.2 of 2018).

b) Taarifa Nne (4) kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu:-

- (i) Ufanisi wa Matumizi ya TEHAMA katika kurahisisha utoaji wa huduma za Kisheria kwenye Mahakama nchini,
- (ii) Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (5) ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
- (iii) Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, na
- (iv) Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu chini ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, lengo la kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(c) cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

1.4.4 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezwa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI;

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakatolewa Taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyobainishwa na Kamati kama ifuatavyo:-

2.2.1 Yatokanayo na Taarifa za Utendaji wa Taasisi za Serikali

a) Utekelezaji wa Mpango wa kuwajengea Uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Kamati, iliainisha kuwa, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) ulianzishwa rasmi na Serikali mwaka 1993 chini ya Kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Fedha (*The Exchequer and Audit Ordinance, Cap 439*), namba 21 ya mwaka 1961.

Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwawezesha Vijana wote Tanzania Bara kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha na kuendeleza miradi yao ya

uzalishaji mali. Hivyo, walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni Vijana wote wa Kike na Kiume walio katika vikundi vya uzalishaji mali wenye umri kati ya Miaka 15 hadi 35 kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko huu siyo wa kibiashara na hivyo hutoa huduma zake kwa kutegemea bajeti kuu ya Serikali, **Kamati ilibaini kuwa, kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 na 2018/2019 Mfuko huu umekuwa ukitengewa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Aidha, kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi 2017/2018 Jumla ya Shilingi Bilioni 2.7 zimetolewa kwa vikundi vya Vijana 523 vyenye idadi ya Vijana 3,781 katika Halmashauri 127 ambazo ni sawa na takribani aslimia 70% ya Halmashauri 184 zilizokusudiwa.**

Aidha, Kamati ilibaini kuwa Mikopo inayotolewa na Mfuko hurejeshwa kwa faida ya **asilimia 10%** ambayo hutolewa ndani ya miaka miwili ili kuuwezesha Mfuko kuwa endelevu, utaratibu ambao kwa maoni ya Kamati ni mzuri kwani utawezesha Mfuko uwe endelevu kwa kuwafikia Vijana wengi zaidi (*Revolving Fund*). Pia, **asilimia 15%** ya fedha zinazotolewa na Serikali hutumika kugharamia mafunzo ya kuwajengea uwezo Vijana kabla ya kuwakopesha, ufuatiliaji na kufanya tathmini. Hivyo, **asilimia 85%** ya fedha zinazotolewa na Serikali hutumika kwa ajili ya Mikopo kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kubaini mafanikio mbalimbali ya Mfuko wa Vijana kama vile ufanisi wa baadhi ya Vikundi vya Vijana kutoka uzalishaji mdogo kwenda uzalishaji Mkubwa, na hivyo kupunguza tatizo la Ajira na umaskini kwa Vijana, bado kumbainika kuwepo kwa changamoto mbalimbali hususani dosari za kiusimamizi katika baadhi ya Halmashauri nchini.

Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu inaainisha kuwa, baadhi ya Halmashauri za Wilaya zimeshindwa kuendelea kuzilea na

kuzisimamia vizuri SACCOS za Vijana ili ziendelee kukua na kutoa huduma stahiki kwa Vijana wengi zaidi. Dosari hii ya kiusimamizi imesababisha kuwepo kwa SACCOS za Vijana ambazo zimekuwa zikitumia fedha za Mikopo kwa matumizi mengine yasiyokusudiwa, pamoja na changamoto ya uwepo wa migogoro miongoni mwa SACCOS za Vijana na hivyo kuathiri ukuaji wa Maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kuwa, utekelezaji wa programu ya kuwajengea uwezo Vijana kabla ya kuwakopesha, iwe endelevu na ifikie vikundi vyote vya Vijana kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa kuwajengea nidhamu, ujuzi na maarifa kuhusu jinsi ya kukopa na kuzalisha kwa faida ili vikundi vyao vikue hadi kufikia Makampuni makubwa.

Aidha, kuhusu dosari za kiusimamizi katika baadhi ya Halmashauri, ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ianze kuzijengea uwezo Halmashauri kuhusu ukusanyaji na usimamizi wa Fedha za Maendeleo ya Vijana ikiwemo kuzisimamia kwa ukaribu ili kuondoa dosari hizo za kiusimamizi na kiutendaji.

b) Takwimu za mwenendo wa Waajiri katika kujiandikisha kwenye Mfumo na Ulipaji wa Michango stahiki kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Fund-WCF*) kwa mujibu wa Sheria,

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati iliainisha kuwa, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ni Taasisi ya Hifadhi ya Jamii iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 (Marejeo ya Mwaka 2015), kwa ajili ya Wafanyakazi ambao wataumia, kuugua au kufariki wakati wakiwa wanatekeleza majukumu ya mwajiri kwa mujibu wa Mikataba yao. Taarifa ilifanua kuwa, Mfuko ulianza kutekeleza majukumu yake tarehe 1 Julai 2015 kama ilivyoelekezwa katika Tangazo la Serikali Na.169 la mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, majukumu yanayotekelezwa na Mfuko huo ni pamoja na kusajili Waajiri, kukusanya michango,

kuwekeza na kutoa elimu kwa Umma kuhusu Mfuko na wajibu wa mwajiri na mwajiriwa. Mfuko huu unatoa huduma zake katika Mikoa yote Tanzania Bara, kupitia Ofisi za kazi zilizopo nchini. Mfuko ulianza kupokea madai na kulipa fidia tarehe 1 Julai 2016 baada ya kumalizika kwa kipindi cha mpito cha mwaka mmoja.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, mafao yanayohusu ukarabati (*rehabilitation*) yanatolewa kwa njia ya matibabu pamoja na uwekaji wa viungo bandia (*Clinical Rehabilitation*).

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ilibaini kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu, Mfuko umeweza kuongeza idadi ya Waajiri waliosajiliwa kwa asilimia 204.31 kutoka **Waajiri 5,178** mwezi Juni 2016 hadi kufikia **Waajiri 15,757** mwezi Septemba, 2018, ambapo, **Waajiri 571** ni kutoka katika Sekta ya Umma na **Waajiri 15,186** ni kutoka Sekta Binafsi.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, kwa upande wa uwezo wa kifedha kwa Mfuko katika kutekeleza majukumu yake, Mfuko unazo fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake. Hii ilibainishwa na taarifa ya Serikali ambapo bajeti ya Michango kwa kipindi cha miaka mitatu(3) ya mwanzo kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka 2017/2018 ilikuwa **Shilingi Bilioni 190.00** lakini makusanyo halisi yalikuwa **Shilingi bilioni 195.30**. Hivyo, katika kipindi hicho, makusanyo ya michango yamekua kwa **asilimia 139.02** kutoka **Shilingi Bilioni 35.34** zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2015/2016 na kufikia **Shilingi Bilioni 84.47** kwa mwaka 2017/2018. Aidha, kwa robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mfuko umekusanya **jumla ya Shilingi Bilioni 17.09**.

c) **Hatua zinazochukuliwa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) katika kulinda usalama wa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi**

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali iliainisha kuwa, OSHA ilianzishwa tarehe 31 Agosti, 2001 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na.30 ya mwaka 1997. Makusudi ya kuanzishwa kwa Wakala huu ni kupata chombo cha Serikali

kitakachosimamia Usalama na Afya mahali pa Kazi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira salama kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, OSHA hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia taarifa kutoka Taasisi nyingine za Serikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), BRELA, Wizara ya Madini, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC).

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, katika kipindi cha Miaka mitatu kuanzia Julai 2015 hadi Juni 2018, Wakala uliweza kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Usajili wa Viwanda na Migodi, ambapo jumla ya **Viwanda 4,972** vilisajiliwa ukilinganisha na lengo la kusajili **Viwanda 4,324**. Pia, **Migodi 244** ikiwemo **mikubwa 17** na **midogo 227** ilisajiliwa ukilinganisha na lengo la kusajili **migodi 130**.

Kamati ilibaini kuwa, ongezeko hili limetokana na hatua za Serikali katika ujenzi wa Uchumi wa Viwanda sambamba na Kampeni maalum za uhamasishaji wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa Kazi katika Sekta ya Madini na uzalishaji (Viwanda) na hivyo kuongeza uelewa wa vihatarishi vilivyopo na namna ya kujikinga pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya mahali pa Kazi.

ii) Ukaguzi wa Usalama na Afya Viwandani na Migodini, ambapo jumla ya Viwanda 14,897 vikiwemo vipya 3,977 na Migodi 298 ilifanyiwa idadi ya kaguzi 215, 793.

iii) Upimaji wa Afya katika maeneo hatarishi ikiwemo viwandani na migodini(Fitness to work Medical Examination), ambapo jumla ya **Wafanyakazi 145,008** walipimwa afya ukilinganisha na lengo la kupima **Wafanyakazi 115,000** ambapo **Wafanyakazi 12,446** walikutwa na matatizo ya mapafu (*Obstructive Lung*

Diseases), **Wafanyakazi 1,567** walikutwa na matatizo ya usikivu (*Hearing Loss*), **Wafanyakazi 43,987** walikutwa na matatizo ya uzito uliokithiri, **Wafanyakazi 6,564** walikutwa na uzito usiofikia kiwango, Wafanyakazi 56,890 walikutwa na matatizo ya shinikizo la damu(Blood pressure) na **wafanyakazi 25,878** walikutwa na matatizo ya uoni(poor vision). Aidha, taarifa iliainisha kuwa, jumla ya **Wafanyakazi 1,376** kati ya **Wafanyakazi 6,783** katika Viwanda vya rangi, viwanda vya betri, utengenezaji wa risasi pamoja na uchimbaji wa Uranium walifanyiwa vipimo maalum vya madini hatarishi ili kubaini athari za madini hayo kwenye damu na kutoa ushauri stahiki.

iv) **Mafunzo ya Usalama wa Wachimbaji wadogo na wajasiliamali**, ambapo taarifa iliainisha kuwa, jumla ya Maafisa 9,458 walipata mafunzo ya usalama na Afya mahali pa Kazi kwa mujibu wa Sheria, kati ya hao **Maafisa 6,250** walitoka Migodini na **Maafisa 3,208** walitoka viwandani ikilinganishwa na **Maafisa 7,320** waliolengwa. Mafunzo haya yalilenga Wanakamati wa Usalama na Afya katika Viwanda na Migodini pamoja na watoa huduma za kwanza.

v) **Uchunguzi wa ajali (Investigation of Occupational accidents)**, ambapo jumla ya **ajali 912** zitokanazo na kazi ziliripotiwa na kufanyiwa uchunguzi katika maeneo ya Viwandani na Migodini, ambapo ajali 30 kati ya hizo zilisababisha vifo sawa na **asilimia 3.3%** ya **ajali** zote na ajali 881 zilikuwa na majeruhi sawa na **asilimia 96.7%**. Hivyo, Kamati ilibaini kuwa, Sekta ya uzalishaji (Viwandani) ilisababisha **asilimia 88** ya **ajali** zote wakati Sekta ya Madini ilikuwa na **asilimia 12** ya **ajali** zote.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, jumla ya Waajiri wa Viwanda na **Migodi 1,623** kati ya Waajiri wa Viwanda na **Migodi 15,195** walichukuliwa hatua mbalimbali za kisheria kutokana na kutozingatia Sheria na Kanuni mbalimbali za Afya na Usalama katika maeneo yao ya kazi. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, zipo changamoto za uelewa mdogo wa masuala ya Usalama na Afya miongoni

mwa Wadau pamoja na ujio wa teknolojia mpya unaotolewa na ongezeko kubwa la Viwanda ukilinganisha na uwezo wa Wakala katika kukabiliana na changamoto hizo.

d) Hatua iliyofikiwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) katika Kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa kuzingatia Matakwa ya Sheria ya *The Public Service Social Security Fund Act (No.2 of 2018)*.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Januari, 2018 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria Na. 2 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (*The Public Service Social Security Fund Act*), ya mwaka 2018. Kutokana na Sheria hiyo, Mifuko minne(4) ya Pensheni ambayo ni PSPF, LAPF, PPF na GEPF ambapo Mfuko mmoja wa PSSSF umeundwa kwa ajili ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Aidha, Sheria hiyo ya PSSSF imefanya marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Sura ya 50 ili kuufanya Mfuko huo kuhudumia Wafanyakazi wa Sekta Binafsi pamoja na Sekta isiyu rasmi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ambayo inajukumu la kusimamia utekelezaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mfuko ya Hifadhi ya Jamii nchini (SSRA) iliomba taarifa ya utekelezaji kuhusu hatua zilizofikiwa katika kukeleza matakwa ya Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya Serikali iliyowasilishwa mbele ya Kamati na kubaini kuwa, toka Sheria hiyo ianze kutumika tarehe 1 Agosti, 2018 na kuanza kwa Mfuko wa PSSSF, Serikali imechukua **hatua mbalimbali ikiwemo ushirikishwaji wa wadau wakati wa uandaaji wa Muswada na wakati wa utungwaji wa Kanuni** kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hiyo.

Aidha, Kamati imebaini kuwa, taarifa ya Serikali inaainisha kwamba, idadi ya Wastaafu waliokuwa wanadai mafao ya mkupuo kwa Mfuko wa PSPF ilikuwa ni **Wastaafu 7, 924** wenye jumla ya **Shilingi Bilioni 738.43**, ambapo Mfuko

umeweka Mkakati wa kulipa madeni hayo kwa kuzingatia mtririko wa kifedha kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia Agosti, 2018. Kwamba, hadi mwezi Oktoba 2018 Mfuko umewalipa jumla ya Wastaafu 896 waliostaafu kati ya mwezi Julai hadi Agosti, 2017 katika awamu ya kwanza, na wale Watumishi waliostaafu hadi kufika Novemba, 2017 matayarisho ya malipo yao yamekamilika tarehe 8 Oktoba, 2018 ambayo ni malipo ya awamu ya pili ambapo jumla ya cheki/hundi 1,123 zilitolewa.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto ya sintofahamu ya waliokuwa wafanyakazi wa Mikataba wa Mifuko iliyounganishwa, ambao Serikali imekiri kuwa, ajira zao bado hazijahuishwa chini ya Mfumo huu mpya.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, hatua ya kuunganisha Mifuko inaweza kuwa na matokeo chanya endapo utekelezaji wake utafanywa kwa ufanisi kwa kuzingatia yafuatayo:-

- i) Kupunguza gharama za uendeshaji,
- ii) Kuwa na uwiano kati ya michango na mafao yatakayolipwa,
- iii) Kuimarisha uwiano baina ya Wanachama na Wastaafu,
- iv) Kuthaminisha pensheni ya kila mwezi kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wa wakati husika,
- v) Kuboresha huduma kwa wanachama wa Mfuko kwa kuwalipa mafao stahiki kwa wakati, na
- vi) Mifuko ya Pensheni kuwa na uwezo wa kulipa mafao kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

e) Ufanisi wa Matumizi ya TEHAMA katika kurahisisha utoaji wa huduma za Kisheria kwenye Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, Muhimili wa Mahakama ni chombo cha usimamizi wa utoaji haki kwa mujibu wa Ibara ya 107A (I)

ikisomwa pamoja na Ibara ya 107A (2)(e) na 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Hivyo, Mahakama imepewa mamlaka ya kusimamia na kutoa uamuzi wa mwisho katika masuala yote yahasuyo utoaji haki.

Kamati imebaini kuwa, Mahakama inatekeleza majukumu yake kupitia Mpango Mkakati wa Mahakama wa miaka mitano (5) 2015/2016 hadi 2019/2020, ambapo mpango huo umeainisha nguzo Kuu tatu ambazo ni:-

- i) Utawala Bora, Uwajibikaji na Usimamizi wa Rasilimali,
- ii) Upatikanaji haki kwa wakati, na
- iii) Kuimarisha Imani ya Wananchi na Ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Mahakama imepanga kuanzisha Mifumo ya TEHAMA kwa kuunganisha utekelezaji wa shughuli zake katika Mfumo jumuishi wa usimamizi wa Mashauri, Mifumo ambayo kwa sasa ipo katika hatua za upembuzi, ujenzi na baadaye majaribio kabla ya kuanza kutumika nchi nzima kwa utaratibu utakaowekwa.

Kamati ilibaini kuwa, Mifumo hiyo ya TEHAMA itajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

- i) Usajili wa mashauri kwa njia ya kielektroniki kwa ngazi zote za Mahakama kwa kuanzia na Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi na za Wilaya,
- ii) Utoaji taarifa ujumbe mfupi kwa njia ya simu (*sms notification*) kwa Wadaawa (*Parties*) tangu hatua ya usajili wa shauri na hatua zitakazo fuata,
- iii) Kutoa ripoti mbalimbali na takwimu za Mashauri,
- iv) Utoaji wa wito wa kuitwa Mahakamani kwa Wadaawa,

- v) Kufungua mashauri kwa njia ya mtandao,
- vi) Uratibu na Usimamizi wa Mwakili wa kujitegemea kama Maafisa wa Mahakama,
- vii) Upatikanaji wa taarifa za kiutawala za Mahakama zote nchini,
- viii) Kanzidata itakayotumika kuweka maamuzi mbalimbali yanayotolewa Mahakamani,
- ix) Usikilizaji wa Mashauri kwa njia ya Video,
- x) Kurekodi Mashauri,
- xi) Mteja kupata huduma kwa njia ya *Self Help Kiosk*, na
- xii) Maktaba Mtandao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa sasa mpango huu wa matumizi ya TEHAMA upo katika hatua za awali za utekelezaji. Hivyo, Mahakama imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- i) Kuunganisha Mahakama 170 na huduma ya internet kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano,
- ii) Kuwa na Maktaba ya mtandao (eLibrary) kwa lengo la kuhakikisha kuwa taarifa za kisheria (*Law Reports*) zinapatikana mtandaoni,
- iii) Kuendelea kuboresha miundombinu ya TEHAMA katika ngazi zote za Mahakama zikiwemo Mahakama za Mwanzo zilizoko Mjini (zenye miundombinu wezeshi),
- iv) Utoaji wa huduma za haki kwa Mfumo wa kielektroniki,
- v) Kufunga vifaa vya Mikutano ya Mtandao (*Video Conference*) katika Vituo vya Lushoto-IJA, Mahakama Kuu

Kanda ya Bukoba, Mahakama Kuu Kanda ya DSM na Gereza la Keko, na

vi) Kuunganisha Mfumo wa kielektroniki wa Mahakama-JSDS II na Mifumo mingine iliyoanzishwa na Serikali pamoja na Wadau wengine wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, endapo teknolojia hizi zikikamilika na kuanza kutumika zitakuwa na matokeo chanya yafuatayo:-

i) Kupunguza gharama na kuokoa muda kwa wateja wa Mahakama na Mahakama yenyewe,

ii) Kurahisisha utoaji ushahidi kwa njia ya Video,

iii) Kupunguza muda wakusikiliza mashauri na hivyo kupunguza mrundikano wa mashauri Mahakamani,

iv) Kumuwezesha Mteja kupata huduma kwa urahisi kupitia tovuti bila kuwasiliana na Maafisa wa Mahakama,

v) Kuimarisha utafiti na uandishi wa maamuzi ya Mahakama kupitia Maktaba Mtandao na njia nyinginezo za mawasiliano ya kimtandao, na

vi) Kusaidia kukokotoa gharama za kufungua shauri na taarifa mbalimbali za mwenendo wa shauri.

f) Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (5) ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kwa Tangazo la Serikali **Na.50** la Mwaka 2018 katika **Gazeti la Serikali Na.3** Toleo **Na.99** la tarehe 13 Februari, 2018, kwa lengo la kutekeleza majukumu Makuu Mawili (2), ambayo ni:-

i) Kusimamia na kuendesha kesi zote za Madai zinazoihusu Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine za Serikali kwa ujumla , katika Mahakama au Mabaraza ya Usuluhishi ndani na ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Kesi za Haki za Binadamu na za Kikatiba, na

ii) Kusimamia na kuendesha mashauri ya usuluhishi yanyohusu Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali, idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kazi ya kufanya uchambuzi wa kazi zitakazofanywa na Ofisi hii mpya, kupanga kazi hizo kwa kuzingatia vigezo vya utumishi wa Umma na kuzifafanua, ilipangwa ifanyike kuanzia mwezi Julai hadi Novemba, 2018 sambamba na kuwapanga Watumishi katika nafasi mbalimbali kwa ajili ya kuanza kuandaa nyaraka nyingine kulingana na muundo, majukumu na kazi walizopewa.

Maandalizi ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (5) wa utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, unategemea kuwa umekamilika na kuanza kutumika katika mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa kutegemea bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi hayo ya Mpango Mkakati, Kamati imebaini kuwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na mpango na bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, ambapo hadi Mwezi Oktoba 2018, Ofisi hii imeshughulikia **jumla ya mashauri 1,373** ya madai ambapo kati ya hayo **mashauri 198** ni mapya na **mashauri 1,175** ni ya zamani pia, Ofisi hii ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuokoa kiasi **cha Shilingi Bilioni 2.77** na **Dola za Marekani 576,000** katika kesi sita (6) zilizoshughulikiwa tangu kuanzishwa kwake.

g) Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilianzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **Ibra ya 36(1)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kwa **tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018**, kwenye **Gazeti la Serikali Na.3 Toleo Na.99** la tarehe 13 Februari, 2018.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye nafasi yake ipo kwa mujibu wa Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambapo, kabla ya Muundo huu mpya, Ofisi hiyo ilikuwa Divisheni ya Mashtaka ya Jinai chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, kwa mujibu wa Muundo huo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Afisa Masuuli wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya Serikali, Kamati ilibaini kuwa, Ofisi ya Mashataka ina majukumu Makuu matatu (3) ambayo ni:-

- i) Kusimamia na kuendesha mashauri yote ya Jinai kwa niaba ya Jamhuri,
- ii) Kuratibu na kusimamia upelelezi wa makosa ya Jinai, na
- iii) Kuwasimamia Waendesha Mashtaka wote, Mwakili wa Serikali na Watumishi wote walio chini ya Ofisi hiyo.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, bado Ofisi hii ya Taifa ya Mashtaka ipo kwenye hatua za awali za uchambuzi wa majukumu yatakayotekelezwa, kupanga na kufafanua kazi zitakazotekelezwa kwa kuzingatia Muundo mpya uliotolewa, kazi ambayo ilipangwa kukamilika ifikapo Novemba, 2018 kwa kuwapanga Watumishi katika wadhifa na nafasi mbalimbali kulingana na matakwa ya Muundo husika.

Hivyo, hatua ya kuandaa Mpango Mkakati pamoja na utekelezaji wake kwa kuzingatia Muundo wa Ofisi hii ya Taifa ya Mashtaka, itakamilika na kuanza kutekelezwa katika mwaka wa Fedha 2019/2020 kulingana na upatikanaji wa Fedha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa Mukstadha huo, Kamati ilibaini kuwa, kwa sasa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa mwaka huu wa Fedha 2018/2019.

h) Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu chini ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu umeainisha haki 23 katika Makundi manne (4) ya kipaumbele kwa lengo la kuimarisha ukuzaji na ulinzi wa Haki za Binadamu nchini. Makundi hayo ya Haki za Binadamu ni haya yafuatayo:-

i) Haki za Kiraia na Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, haki za kundi hili ni pamoja na haki ya kuishi, uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na kupata habari, fursa ya kupata haki, uendeshaji wa mashauri bila upendeleo, usawa mbele ya vyombo vya Sheria, haki ya uhuru na usalama wa watu na Bunge kupitia Mikataba ya uwekezaji. Ili kuboresha na kuimarisha Mfumo wa utoaji haki hizo nchini, Serikali imeimarisha Bajeti ya Mahakama kwa kutenga fedha za kutosha katika Mfuko wa Mahakama kwa lengo la kuimarisha Mfumo wa kusikiliza mashauri kwa njia ya kielektroniki, usajili wa mashauri, utoaji wa taarifa za kuitwa Mahakamani na matumizi ya TEHAMA.

Aidha, masuala mengine yaliyotekelezwa chini ya kundi hili, ni pamoja na kuwajengea uwezo Mahakimu, Majaji, Mawakili wa Serikali na Polisi kuhusu masuala mbalimbali ya haki za Binadamu ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 ambayo imewezesha

kuwepo Mfumo wa Wasaidizi wa kisheria katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

ii) **Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni,**

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali iliainisha kuwa, kundi hili linahusu haki ya kumiliki mali na fursa ya kupata Ardhi, haki ya Elimu na haki ya kupatiwa hali nzuri ya maisha, haki ya kupata chakula bora, maji safi na usalama na haki ya kufanya kazi. Haki nyingine za kundi hili ni haki ya kufaidi kwa kiwango cha juu cha ubora wa afya ya mwili na akili, haki ya kuwa na mazingira safi na bora kiafya na haki ya hifadhi ya jamii.

Katika kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya upatikanaji wa haki za kundi hili, taarifa iliainisha kuwa, Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza Sera ya Elimu bila malipo kuanzia elimu ya Msingi hadi Sekondari (Darasa la kwanza hadi Kidato cha Nne) pia kuifanyia Marekebisho Sheria ya Elimu Sura 353 kupitia Sheria Na.4 ya mwaka 2016 ambayo inazuia mtoto kukatisha masomo kwa sababu ya ndoa za utotoni.

Aidha, Serikali imeongeza upatikanaji maji safi na salama Vijijini ambapo idadi ya Wananchi wanaofaidika imeongezeka kutoka **Wananchi 15,200,000** kwa mwaka 2013 hadi **Wananchi 22, 951, 371** kwa mwaka 2017 sawa na **asilimia 72.58%**. Hii ni pamoja na kuanzisha jumla ya **program ndogo 5,438** za maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, **Vituo vipya 90** vya kuchunguza mwenendo wa rasilimali maji, vituo 633 vilimarishwa na visima virefu 1,100 vilichimbwa na kutambua jumla ya vyanzo vya **maji 114**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa haki afya, taarifa iliainisha kuwa, katika kujenga mazingira wezeshi kwa Wananchi kupata matibabu, Serikali imeanzisha **Vituo 6,155** pamoja na kuimarisha Maabara 4 za Kanda za Kifua Kikuu na kuwezesha **asilimia 90%** ya Wagonjwa wa Kifua Kikuu kutibiwa na kupona. Hii ni pamoja na Kampeni za ujenzi wa vyoo bora ambapo **Kaya 2,414, 094** zimepata vyoo bora na sehemu maalum za kunawa mikono.

iii) Haki za Makundi yenye Mahitaji Maalum,

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali iliainisha kuwa, kundi hili linahusu haki za makundi ya Wanawake, Watoto, Wazee, Watoto wanaokinzana na Sheria, Wafungwa, Watu wenye ulemavu, Watu waishio na VVU, Wakimbizi, Watafutao hifadhi ya kisiasa na Watu wasio na Taifa.

Katika kutekeleza mazingira wezeshi ya upatikanaji haki wa kundi hili, Serikali iliandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018-2021/2022 na tayari umeanza kutekelezwa katika Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Hii ni pamoja na kila Halmashauri kutenga **asilimia 2%** ya mapato yake ya ndani ili kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, pia kutoa huduma za kinga za Watu wenye ualbino ikiwemo kuwapatia *lotion* kwa lengo la kuwakinga na mionzi ya jua.

Mheshimiwa Spika, taarifa ilifafanua zaidi kuwa, hadi sasa kupitia RITA iliandaa na kuanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Usajili kwa Watoto chini ya Umri wa miaka mitano (5) unaotekelezwa katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Shinyanga, Geita, Lindi, Mtwara na Simiyu, ambapo hadi sasa zaidi ya **Watoto 2,634,192** wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa na hivyo kuongeza kiwango cha Watoto waliosajiliwa na kupata vyeti kutoka **asilimia 12.9%** mwaka 2013 hadi **asilimia 38%** mwaka 2017. Aidha, Serikali iliandaa Kanuni za Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 (*Juvenile Court Rules of 2016 and Juvenile Designated Courts, GN NO.314 of 9th December, 2016*) zenye kutoa Mwongozo wa kuendesha mashauri ya Watoto pamoja na kubainisha Mahakama za Mwanzo kuwa Mahakama za Watoto.

Pia, taarifa ilielezea kuwa, kutungwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, kuliwezesha Serikali kuanzisha Kanuni za Watu wenye ulemavu mwaka 2012 yenye kuainisha vyombo mbalimbali vya utekelezaji ikiwemo kuanzisha Baraza la Taifa la Watu wenye ulemavu pamoja na Kamati zake kwa ngazi za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali iliainisha zaidi kuwa, tayari imeanza na inaratibu utolewaji wa huduma ya matibabu bure kwa Wazee ikiwemo kuwapatia malazi kupitia Makambi ya Wazee, kuwapatia vitambulisho rasmi kwa ajili ya matibabu na kutoa chakula kwenye makambi rasmi ya Wazee. Hii ni pa moja na kuendelea kutoa Elimu kwa jamii kuhusu haki za ustawi wa Wazee kupitia vyombo vya habari na maadhimisho ya siku ya Wazee.

Aidha, taarifa ya Serikali iliainisha kuwa, Wizara ya Afya, Maendeeo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu utoaji wa Elimu kwa Jamii kuhusu UKIMWI na kuweka Mwongozo kuzielekeza Wizara na Taasisi za Serikali kutoa elimu na huduma kwa Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya ndani kupitia Jeshi la Magereza inaendelea kutekeleza jukumu la kurekebisha Wafungwa Magerezani kwa kupitia program mbalimbali za mafunzo darasani, dini, michezo, ushauri nasaha na stadi za kazi. Hii ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa program ya adhabu mbadala wa Kifungo Gerezani.

iv) Kujenga Uwezo wa Taasisi, Masuala yanayoibuka na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali iliainisha kuwa, kundi hili linahusu kujenga uwezo wa Taasisi chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na eneo la Haki za Binadamu na Biashara.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ilipelekea Serikali kuongeza Bajeti ya Tume kutoka **shilingi Bilioni 3.3** mwaka 2015/2016 hadi **Bilioni 3.7** mwaka 2016/2017 na **Bilioni 6.1** mwaka 2017/2018. Hii ni pamoja na kuimarisha Muundo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kuanzisha Ofisi Pemba na kupandisha hadhi ofisi ya Zanzibar kuwa ofisi ndogo ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, mchakato wa kuandaa Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara unaendelea.

Kama sehemu ya maandalizi ya mpango huo, taarifa ilifafanua kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamisheni ya Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu ilitoa mafunzo kwa maafisa wa Serikali wakiwemo Mwakili wa Serikali kuhusu Haki za Binadamu na Biashara, mwezi Agosti, mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, matokeo ya tathmini ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu kati ya mwaka 2016 hadi mwaka 2017, ulikuwa na mafanikio lakini kulijitokeza changamoto zifuatazo:-

(i) Mpango kazi ulikusudia kuimarisha haki za msingi kwa kuzingatia Mikataba ya Kimataifa pasipo kuweka vipaumbele kutokana na sera za nchi, hivyo maeneo mengi yamekwama kutekelezwa,

(ii) Uwepo wa bajeti finyu ya kuratibu shughuli za utekelezaji wa Mpango Kazi husika, na

(iii) Mpango Kazi haukuweza kufikia watu wote kwa wakati kutokana na changamoto ya fedha.

2.2.2 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria;

1.0.1 Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Miswada Mitatu ya Kisekta (3), Jumla ya Sheria zote zilizochambuliwa na kujadiliwa na Kamati zikiwemo Sheria zilizomo katika Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ni Sheria 41.

a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) Wa Mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018.*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulifanya marekebisho katika sheria 13 zifuatazo:-

(i) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27

- (ii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20,
- (iii) Sheria ya Kubadilishana Wafungwa, Sura ya 368,
- (iv) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1,
- (v) Sheria ya Ukomo, Sura ya 89,
- (vi) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171,
- (vii) Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254,
- (viii) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430,
- (ix) Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Utekelezaji wa Majukumu yake, Sura ya 268,
- (x) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329,
- (xi) Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19,
- (xii) Sheria ya Kuhusu Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256, na
- (xiii) Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni matokeo ya **Hati Idhini iliyochapishwa katika Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018**, ambapo, Serikali ilifanya Mabadiliko katika Mfumo wa Kisheria (*Legal Regime*) nchini yenye kuweka au kuanzisha Mfumo mpya wa uwakilishi na utetezi wa Serikali na Taasisi zake zote katika masuala ya Kisheria ndani na nje ya nchi.

Hivyo, kutokana na mabadiliko hayo, Mfumo wa Sekta ya Sheria nchini kupitia Ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zilihitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia mabadiliko hayo ya kimfumo kwa lengo la kuondoa

changamoto za kiutendaji miongoni mwa Taasisi husika kupitia Vifungu mbalimbali vya Sheria.

b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na.3 wa Mwaka 2018 [The Written Laws(Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill,2018];

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2018 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Sita (6) zifuatazo:

- (i) Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura ya 141,
- (ii) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33,
- (iii) Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216,
- (iv) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11,
- (v) Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49 na
- (vi) Sheria ya Takwimu, Sura ya 351.

Hivyo, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria hizo ili kuonda mapungufu ambayo yalibainika katika utekelezaji wa Sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo. Aidha, marekebisho hayo yalilenga kuziwezesha Sheria husika kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kiteknolojia, kisiasa na kiuchumi yaliyojitokeza na yenye athari katika utekelezaji wake.

c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2018 [The Written Laws(Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2018];

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulifanya Marekebisho katika Sheria Nne (4) ambazo ni:

(i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Sura ya 288,

(ii) Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225,

(iii) Sheria ya Pasipoti na Hati za Kusafiria, Sura ya 42, na

(iv) Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364.

d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 [The Political Parties(Amendment)Bill,2018]

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria hii yanaimarisha Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuipa Mamlaka zaidi ya kuratibu na kusimamia kwa ufanisi zaidi uanzishwaji na utekelezaji wa Majukumu ya Vyama vya Siasa nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za Nchi.

2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mkoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita na Wilayani Chato, kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2018. Hivyo, Miradi ifuatayo ilitembelewa na kukaguliwa:-

a) **Mradi Na.6314**-Ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga (**Shilingi Bilioni 4.4**), ambapo ujenzi umekamilika;

b) **Mradi Na.6310** -Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Geita (*District Court*) kwa teknolojia ya gharama nafuu ya Moladi (**Shilingi Milioni 644.40**); na

c) **Mradi Na.6310** -Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Simiyu (*District Court*) (**Shilingi Milioni 644.40**).

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukaguzi wa Miradi husika hapo juu, pia Kamati ilipokea taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa chini ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya tarehe 19 Machi, 2018, Mahakama imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Majengo Matano(5) kwa ujenzi wa kutumia teknolojia ya gharama nafuu (MOLADI) ambayo ni Mahakama za Wilaya ya Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama ya Mwanzo Kawe. **Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, Kamati haikuweza kutembelea na kukagua miradi hiyo kwa lengo la kujiridhisha hatua ya utekelezaji wake.**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Eflu (23, 236, 830,000/=)** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** sawa na **Asilimia 77.46%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Ndani na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Eflu (5, 236, 830,000/=)**, sawa na **Asilimia 22.54%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Laki Tano Hamsini na Sita Eflu (10,478, 556,000/=)** sawa na **asilimia 45.%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja na Tatu Eflu (9,261,003,000/=)** sawa na **asilimia 51%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za

Ndani na Fedha hizo zimepatikana kwa wakati. Aidha, Ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya *MOLADI* ni Mfumo wa gharama nafuu na unakamilisha ujenzi kwa haraka.

Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan Miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

2.2.4 Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi ambazo Kamati inazisimamia

1.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Mafungu 14 ya Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 **Fungu 26** la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais **lilitengewa Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa Kumi na Nne, Laki Sita na**

Nane Eflu (4, 914, 608, 000/) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018, Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Tano na Milioni Sitini na Tatu, Hamsini na Mbili Eflu, Mia Nne Themanini na Sita na Senti Arobaini na Nne (5, 063, 052, 486.44)** sawa na asilimia 103% ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ikiwa imeongezeka **asilimia 3%** zaidi ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho kilicho ongezeka ni kutokana na gharama za kuhamisha Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 **Fungu 31** la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Laki Tano Thelathini na Tano Eflu (8, 214,535,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018 Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tano Hamsini na Mbili, Laki Saba Hamsini na Moja Eflu, Mia Tisa Kumi na Tatu na Senti Ishirini na Saba (10,552,751, 913.27)** sawa na **asilimia 128.5%** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 28.5%** zaidi ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho kilichoongezeka ni kutokana na gharama za kuhamisha Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mafungu yote (**Fungu 26 na Fungu 31**).

b) Ofisi ya Waziri Mkuu;

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

- i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
- ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
- iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
- iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
- v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
- vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Saba, Milioni Tatu, Laki Saba na Tisa Eflu na Mia Tatu Thelathini na Sita (67,003,709,336 /=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Arobaini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Mbili na Ishirini na Moja Eflu, Mia Tatu Tisini na Tatu (43,342, 021,393)** sawa na asilimia 64.7% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu. Aidha, Fedha iliyoongezeka katika **Bajeti ya Fungu 61(Tume ya Taifa ya Uchaguzi)** hadi kupokea zaidi ya asilimia 100% ya fedha zilizoidhinishwa, ni kutokana na gharama za Chaguzi ndogo zilizohitaji kiasi hicho cha fedha ili kukamilisha chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisini na Tatu, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Eflu , Mia Saba Sitini na Tatu (93, 565, 372, 763)** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Eflu, Mia Saba Sitini na Tatu (61, 565, 372, 763)** sawa na **Asilimia 65.80%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha

za Nje na **Shilingi Bilioni Thelathini na Mbili (32, 000,000,000), sawa na Asilimia 34.20%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Arobaini na Sita, Milioni Mia Tano Thelathini na Mbili, Laki Tano Arobaini na Tano Eflu, Mia Tisa Sabini na Tisa (46, 532, 545, 979) sawa na asilimia 49.7%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Nje kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 jambo ambalo likiendelea linaweza kukwamisha utekelezaji wa maendeleo ya nchi hasa ukizingatia unyeti wa Ofisi hii. Hivyo, **Kamati inashauri Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya ndani ya nchi katika kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.**

c) **Wizara ya Katiba na Sheria;**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 .

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tatu, Milioni Mia Mbili Arobaini na Tatu na Sabini na Nane Eflu (143, 243, 078,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Wizara na Taasisi zake zilipokea **Shilingi Bilioni Themanini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Saba, Ishirini na Nane Eflu na Themanini**

na Tatu (86,977,028,083/=) sawa na asilimia 52% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Efu (23, 236, 830,000/=)** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** sawa na asilimia 77.46% ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Ndani na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Efu (5, 236, 830,000/=)**, sawa na asilimia 22.54% ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Laki Tano Hamsini na Sita Efu (10,478, 556,000/=)** sawa na asilimia 45. % ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja na Tatu Efu (9,261,003,000/=)** sawa na asilimia 51% ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upataikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilizyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara na Taasisi hizi na kulishauri Bunge lako Tukufu kuzipitisha bajeti zake pamoja na kutoa ushauri kuhusu namna bora ya

utatuzi wa changamoto zilizoonekana katika kila Taasisi husika kwa lengo la kuongeza ufanisi.

2.2.5 Ufinyu wa muda wa Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa fedha unaoisha. Ufinyu wa muda unakwamisha utekelezaji wa Kanuni hii. Siku za Kikanuni za kukagua Miradi ya Maendeleo ni siku saba ambazo kiuhalisia hazitoshi kukagua Miradi ya Maendeleo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda wa ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019, Kamati ilifanikiwa kutembelea Miradi ya Maendeleo michache inayohusu ujenzi wa Mahakama, kwenye eneo moja tu la Kanda ya Ziwa iliyopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

2.2.6 Semina na Mafunzo

1.1.1 Mheshimiwa Spika, katika Kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019, Kamati ilipatiwa Semina na mafunzo kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge, kwa ajili ya kujengea Kamati uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria hususan masuala ya msingi katika hatua za Uchambuzi wa Miswada. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-

a) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa *Legislative Support Program (LSP II)*;

b) Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN - Women) kwa kushirikiana na Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG);

- c) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA);
- d) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- e) Chama cha Mwakili Tanganyika (TLS);

Aidha, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali walitoa mafunzo/semina mbalimbali kuhusu masuala mbalimbali ya kisera, kisheria, Muundo na Majukumu ya Taasisi hizo kwa lengo la kuwaongezea uelewa Wajumbe. Taasisi hizo ni pamoja na:-

- a) Tume ya Utatuzi na Usuluhishi wa Migogoro kazini (CMA);
- b) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF);
- c) Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA);
- d) Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, na
- e) Mahakama kuu ya Tanzania.

1.1.2 Mheshimiwa Spika, kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo na uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisera na kisheria na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuishauri Serikali ipasavyo.

2.2.7 Changamoto za Mazingira wezeshi ya Watu wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto za uwekaji wa mazingira wezeshi kwa Watu wenye ulemavu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, wakati Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010 inatamka kuanzishwa kwa Baraza pamoja na Mfuko wa Watu wenye Ulemavu, bado kumekuwepo sintofahamu kuhusu utekelezaji wa matakwa hayo ya kisheria kwa lengo la kuwajengea mazingira wezeshi Watu wenye Ulemavu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019, Kamati iliweza kukutana na Makundi mbalimbali ya Watu wenye ulemavu kupitia semina mbalimbali na kupokea maoni na mapendekezo yao kuhusu changamoto mbalimbali wanazozipitia ikiwemo kukosekana kwa Baraza la Watu wenye Ulemavu na Mfuko wa kuwezesha masuala yao mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kuwa masuala haya ya Watu wenye Ulemavu yanaratibiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati imebaini kuwa, Bajeti ya Ofisi hiyo haina hata kasima (*Sub vote*) ya Watu wenye ulemavu, hali ambayo imekuwa ni hoja ya msingi miongoni mwa makundi mbalimbali ya Watu wenye Ulemavu hapa nchini.

Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa, ili kuweka mazingira wezeshi kwa Watu wenye Ulemavu, wakati umefika ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie kikamilifu utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu na Kanuni zake, kwa kuainisha masuala ya Watu wenye Ulemavu kuwa sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 *Masuala ya Watu Wenye Ulemavu*

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Watu wenye ulemavu ni sehemu ya Jamii ya Watanzania na hivyo wanahitaji kuwekewa mazingira wezeshi ili waweze kujikwamua kwa maendeleo endelevu;

NA KWA KUWA, Serikali inatambua na imezingatia haki mbalimbali za Watu wenye Ulemavu kupitia Sheria na Mikataba ya Kimataifa,

HIVYO BASI; Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- a) Kuanzisha na kutangaza Wajumbe wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu,
- b) Kuanzisha na kutenga fedha za Kifungu(Kassima) ya Masuala ya Watu wenye Ulemvau,
- c) Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemvau kama ilivyoanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, na
- d) Kuweka usimamizi mzuri wa Fedha za Watu wenye Ulemavu kwa kuhakikisha fedha hizo zinatengwa kwa kila Halmashauri na zina wafikia walengwa kwa wakati.

3.2 Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana A;

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya Vijana nchini,

NA KWA KUWA, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zenye kuathiri ufanisi wa Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana,

HIVYO BASI, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

- a) Kungeza Usimamizi wa fedha za Mfuko kwa lengo la kuimarisha SACCOS zilizopo na kudhibiti SACCOS hewa za Vijana ambazo hukopeshwa na kupotea na fedha za Serikali. Hii ni pamoja na OWM kuwa na ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Rais –TAMISEMI ambao ndiyo wenye dhamana na Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila Halmshauri inawajibika kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana na kusimamia marejesho kwa wakati,

b) Kupanue uwigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kuanza kutoa Mikopo kwa makundi mbalimbali ya Vijana nje ya SACCOS kwa kuwa siyo Vijana wote ni marafiki wa SACCOS kutokana na masharti magumu ya uendeshaji wa baadhi ya SACCOS nchini hatua ambayo huwa kizuizi kwa Vijana wengi kuzifikia fursa za Fedha. Hii ni pamoja na Vikundi vya Vijana vilivyosajiliwa na vyenye mipango ya miradi yenye lengo la kuongeza ajira, CBOs na Makampuni yaliyosajiliwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya Kati na Mikubwa ya kutoa ajira nyingi kwa Vijana, na

c) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, waandae ziara ya kikazi ambapo Kamati itatembelea na kukagua Vikundi/SACCOS za Vijana ambazo zimenufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Kamati iweze kujionea hali halisi na kuishauri Serikali ipasavyo.

3.3 Ufanisi Zaidi kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwepo changamoto za kiutendaji kwa baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu,

NA KWA KUWA; changamoto hizo ni vyema zikatafutiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi zaidi kwa Taasisi hizo;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri yafuatayo:-

a) **Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)** ujipange na kuwa na Mkakati ambao utahakikisha unakwenda sambamba na ongezeko kubwa la Waajiri wapya kutokana na kuongezeka kwa uanzishwaji wa Viwanda nchini pamoja na mahitaji ya matumizi ya TEHAMA katika kuwahudumia wadau wengi kwa wakati na kwa ufanisi zaidi. Hii inatokana na ukweli kuwa, hadi kufikia mwezi Septemba, 2018 kulikuwa na Jumla ya biashara zilizosajiliwa (*Registered Business*

Entities and institutions) 28,625 nchini ambazo zingestahili kujisajili katika Mfuko kwa mujibu wa Sheria.

b) Mamlaka ya Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) iongeze Mikakati ya usajili na usimamizi wa Afya na Usalama katika maeneo ya kazi kulingana na ongezeko la Viwanda nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Wafanyakazi kulingana na vipaumbele vya Wakala huo kwa wakati husika.

c) Serikali ione umuhimu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya wale Wafanyakazi wa Mikataba ambao Mikataba yao ilikuwa bado inaendelea kwenye Mifuko ya Pensheni iliyounganishwa lakini hawajaweza kuendelea na ajira zao.

3.4 Usimamizi wa utoaji haki nchini

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA; ni jukumu la Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya Sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati,

NA KWA KUWA; usimamizi wa utoaji wa haki nchini unategemea sana ufanisi wa Taasisi husika zenye dhamana hiyo;

HIVYO BASI; Kamati inashauri Taasisi husika zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

a) Mahakama iendeleo kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake iliyojiwekea wa kuhakikisha kila Hakimu na Jaji anashughulikia na kukamilisha idadi ya Mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya Wananchi kwa chombo hiki cha utoaji wa haki nchini.

b) Serikali iandae na kutekeleza Mkakati Endelevu wa kuwajengea uwezo Mwakili wa Serikali kutoka Taasisi mbalimbali za Umma, hasa uwezo wa kufanya majadiliano,

uandishi na uchambuzi wa Mikataba ya kiuwekezaji na uwezo wa kuelewa na kutetea maslahi ya nchi katika Mahakama/Mabaraza ya ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itaiwezesha Serikali kuwa na Rasilimali Watu wenye uwezo wa kulinda na kutetea maslahi ya nchi katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi. Aidha, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zihakikishe zinaendelea kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje katika kutafuta nafasi za kuwajengea uwezo na uzoefu Mawakili wa Serikali kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaaluma vinavyohitajika kwa wakati husika.

c) Serikali iajiri idadi ya Watumishi wa kutosha chini ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Serikali iandae na kutekeleza mpango endelevu wa kuwajengea uwezo Mawakili/Wanasheria na Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili waweze kusimamia na kuendesha mashauri ya haki jinai kwa ufanisi zaidi.

d) Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge iandae na kuratibu mafunzo kwa Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili Wajumbe wawe na uelewa wa pamoja kuhusu majukumu ya Tume na mipaka yake kwa lengo la kuishauri Serikali ipasavyo. Hii ni pamoja na Wizara husika kuona umuhimu wa kuishirikisha Kamati katika hatua za awali za uandaaji Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu nchini ili Kamati ipate fursa ya kutoa mawazo na hivyo kwenda sambamba wakati wa utekelezaji.

e) Serikali iendeleo na jitihada zake za kuchukua hatua madhubuti katika udhibiti wa uvunjaji wa haki za Makundi maalum kama vile Watu wenye Ulemavu wa ngozi, Wazee, Wasichana wanaosafirishwa nje ya nchi kwa biashara haramu lakini kwa mgongo wa kwenda kufanya kazi za nyumbani pamoja udharirishwaji wa haki za watoto wa mitaani kwenye vituo vya mabasi vya Mikoa na maeneo mengine nchini.

f) Serikali iandae na kutekeleza Mpango Mkakati chini ya Magereza ambao utahakikisha Wafungwa wenye ndoa wanawekewa mazingira yatakayohakikisha wanapata haki ya kutembelewa na wenzi wao na kupata haki ya tendo la ndoa kwa kuzingatia utaratibu utakowekwa na mamlaka husika. Hatua hii itapunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali magerezani hasa UKIMWI.

g) Serikali iendelee kuboresha Bajeti ya Fungu 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

3.5 Ufanisi katika mwenendo wa Bajeti za Serikali;

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa, kumekuwepo ongezeko la upatikanaji wa Fedha za ndani ukilinganisha na upatikanaji usioridhisha wa Fedha za Nje, kwa mwenendo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha 2017/2018,

NA KWA KUWA; hatua hii ya kutumia fedha za ndani kuendesha mipango ya nchi inapunguza utegemezi wa kiuchumi na ni ya uhakika zaidi,

HIVYO BASI; Kamati inashauri kuwa:-

a) Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika;

b) Serikali kupitia vyombo husika, ibuni vyanzo vipya vya mapato vyenye uhakika na endelevu, na

c) Elimu ya kulipa Kodi iendelee kutolewa kwa Wananchi ili kila Mtanzania aone umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

3.6 *Semina na mafunzo kwa Kamati*

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Programu ya utekelezaji wa Mradi wa LSP (II) chini ya UNDP, imekuwa msaada mkubwa sana katika kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hii kuhusu masuala mbalimba katika uchambuzi wa Miswada ya Sheria,

NA KWA KUWA, Kamati hii ina jukumu la Kuchambua na kujadili Miswada mingi ya Sheria za Marekebisho ya Sheria mbalimbali ambazo zinagusa Sekta mbalimbali nchini,

NA KWA KUWA; bado mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge na Sekretarieti ili kupanua wigo wa uelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao;

HIVYO BASI; Kamati inashauri kwamba:-

a) Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na **Waratibu wa Mradi wa LSP(II)** waone umuhimu wa kuandaa na kuratibu mafunzo maalum ya Kamati hii ndani na nje ya nchi kuhusu masuala ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria na Bajeti za Serikali (*Bills and Budget Scrutiny*) kwa lengo la kuongeza weledi kwa Wajumbe wa Kamati hii na Sekretarieti yake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mradi huu wa LSP uwe endelevu kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo yenye tija kwa kuongeza ufanisi wa Wabunge na Sekretarieti yake katika kusimamia utendaji wa Serikali na Taasisi zake.

b) Wizara na Taasisi za Serikali zenye maeneo yanayofanyiwa marekebisho ya Sheria kuendelea kutoa mafunzo kwa Kamati ili kuendelea kujenga uwezo na uelewa wa Kamati katika maeneo husika.

3.7 *Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati*

Mheshimiwa Spika;

KWA KUWA, Bunge lina dhamana kubwa ya kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

NA KWA KUWA, katika kutimiza jukumu hili Bunge hutumia Kamati zake ambazo hutoa ushauri, Mapendekezo na maelekezo mbalimbali kwa Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali ya Kamati na kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri na mapendekezo hayo kila inapotakiwa kufanya hivyo.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mliutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Mwaka Mmoja uliopita.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Shukrani za Pekee ziwaendee Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. January Makamba (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Manaibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Antony Mavunde (Mb) na Mhe. Ikupa Alex (Mb), Mhe. Mussa Ramadhan Sima (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati pale

alipohitajika kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha hoja za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria.

Aidha, Kamati inawashukuru sana Wanasheria wote na Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada mbalimbali. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhiti kwa Idara ya Ushauri wa Masuala ya Sheria ya Bunge (CPLC) kwa namna bora walivyoshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019. Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao:-

- i. Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) chini ya Mradi wake wa *Legislative Support Program (UNDP - LSP)*;
- ii. Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG),
- iii. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*)-LHRC,
- iv. *Stallion Attorneys*,
- v. Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (*Tanganyika Law society*)-TLS,
- vi. *Zanzibar Law Society*,
- vii. *Centre for Good Governance and Democracy in Tanzania*(CEGODETA)
- viii. Tanzania Women Lawyers Association-TAWLA
- ix. Tanzania Women Crossparty Platform (ULINGO)

- x. TWaweza
- xi. Alliance for Development Organisation
- xii. Jukwaa la Katiba Tanzania(JUKATA),
- xiii. *Tanzania Network of Legal Aid Providers-TANLAP,*
- xiv. Youth Partnership Countrywide (YPC)-Pwani,
- xv. Women Wake UP (WOWAP)-Dodoma,
- xvi. Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA)-Dar es Salaam,
- xvii. NGONEDO-Dodoma,
- xviii. ICISO-Iringa,
- xix. PLAJC-Dodoma,
- xx. Zanzibar Youth Forum (ZYF)-Zanzibar, na
- xxi. Mtandao wa Wanawake na Katiba,
- xxii. African Centre for International Affairs(ACIA),
- xxiii. Tanzania Citizens Information Bureau (TCIB), na
- xxiv. Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. **Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb -**Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foun, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
- 8.Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb-Mjumbe
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Jacqueline K. Ngonyani Msongozi, Mb- Mjumbe;
17. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Tundu Antiphias Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Dkt. Suzan Kolimba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Sanga, Katibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagia, Ndg. Dunford Mpelumbe, Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima pamoja na Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD), kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya

Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli ilizotekeleza kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii .

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

8 FEBRUARI, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Mtemi Chenge, dakika 15. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inahusu majukumu ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa na Serikali hapa Bungeni kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imeainisha utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge. Aidha, taarifa imebainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu sheria ndogo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019; katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari,

2019, yaani katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya sheria ndogo 704 ikilinganishwa na sheria ndogo 404 zilizowasilishwa Bungeni na Serikali katika kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya uchambuzi wa sheria ndogo, Kamati ilibaini jumla ya sheria ndogo 395 kati ya 704 ambazo ni sawa na asilimia 56.1 zilihitaji kufanyiwa uchambuzi ili kujiridhisha iwapo zinakidhi matakwa ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyingine za nchi. Aidha, katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini jumla ya sheria ndogo 93, kati ya hizo 395 ambazo ni kama asilimia 23.5 zilikuwa na dosari mbalimbali, ambapo Kamati ilitoa maoni na mapendekezo ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo; katika uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa, Kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na baadhi yake ni kama zifuatazo:-

(i) Sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi;

(ii) Sheria ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali (kutorejea kanuni sahihi, kurejea kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa kanuni na maudhui ya jedwali kutofautiana na vifungu);

(iii) Sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria (*drafting principles*);

(iv) Sheria ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu; na

(v) Sheria ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (*unreasonable provisions*) kinyume na kutungwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika mchakato mzima wa utungaji wa sheria ndogo ambazo zinachangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Uchache wa Wanasheria wenye taaluma ya uandishi wa sheria katika Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uhaba wa wataalam hao unasababisha sheria ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (*Chief Parliamentary Draftsman*) kwa sababu idara hiyo siyo tu kwamba ina wataalam wachache, lakini pia ina kazi nyingi sana;

(ii) Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili neno kwa neno (*copying and pasting*) sheria ndogo kutoka katika halmashauri nyingine bila kufanya marekebisho ya msingi na hivyo kusababisha kunakili sheria ndogo zisizoendana na uhalisia wa madhumuni na sababu za kutungwa kwake;

(iii) Baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa mamlaka waliyopewa na Bunge ya kutunga sheria ndogo kuweka masharti ambayo aidha yalikataliwa au kupingwa na Kamati za Kudumu za Bunge wakati wa uchambuzi wa Muswada wa Sheria inayokasimu mamlaka hayo. Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa na jukumu kubwa la kushughulikia dosari za masharti yaliyomo ndani ya sheria ndogo ambayo yangeweza kupatiwa uhalali wake kwa hayo masharti kuwekwa katika sheria husika.

(iv) Baadhi ya Mamlaka zilizokasimiwa mamlaka ya kutunga sheria ndogo, zimekuwa zikitunga sheria ndogo zinazopoka mamlaka ya vyombo vingine vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Mfano, baadhi ya Kanuni za Wizara kuwa na vifungu ambavyo utekelezaji wake unaingiliana na Mamlaka ya Mahakama au kanuni kumpa Waziri majukumu

mapana ambayo yanaingiliana na mamlaka ya Waziri mwingine.

(v) Baadhi ya Mamlaka zilizokasimiwa mamlaka ya kutunga sheria zimekuwa zikitunga sheria ndogo pasipo kuona umuhimu wa kushirikisha wadau ambao ndio walengwa wa sheria ndogo hizo. Hali hii imeleta changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge upo katika ukurasa wa 8–20 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge, Serikali imetekeleza ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu upo katika ukurasa wa 20 – 36 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ilichambua jumla ya sheria ndogo 513 zilizowasilishwa Mezani na Serikali. Baada ya uchambuzi huo wa sheria ndogo hizo Kamati ilibaini jumla ya sheria ndogo 76 kati ya 513 kuwa zilikuwa na upungufu. Kufuatia dosari hizo zilizobainika, Kamati ilikutana na Serikali ambapo Serikali ilikubali kufanya marekebisho katika sheria ndogo husika kama inavyoonekana katika jedwali la uchambuzi liliioambatanishwa na taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati; katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na

Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge yamefafanuliwa kwa kirefu katika jedwali la uchambuzi ambalo limeambatishwa na taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyoainishwa yachukuliwe na Bunge kama sehemu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa na Serikali katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge na hatimaye kufanikisha uwasilishwaji wa taarifa hii katika Bunge lako Tukufu. Naomba majina ya Wajumbe wa Kamati hiyo yote yatambuliwe kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake kwa wakati na kwa uratibu mzuri wa uwasilishaji wa Jedwali la Uchambuzi kwa Wizara husika ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda wote imekuwa ikiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati na kukubali utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa maeneo ambayo yana dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Kamati, Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Mkuta Masoli, Ndugu Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndugu Paul Chima kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA
NDOGO KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI
CHA KUENZIAJANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari,*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya awali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inahusu majukumu ya uchambuzi wa Sheria Ndogo yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019.

Taarifa hii imeainisha utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge. Aidha Taarifa imebainisha matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo hizo .

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii vilevile inafafanua kuhusu njia mbalimbali zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati sanjari na mapendekezo ya Kamati kuhusu namna bora ambavyo Bunge linaweza kuisimamia Serikali katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

1.2 Majukumu ya Kamati na Msingi wa Utekelezaji Wake

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinabainisha majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kuwa ni kuchambua

Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Malengo ya masharti haya ya kikanuni ni kulipatia Bunge Mamlaka ya Udhubiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo kwa vyombo vingine (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ambavyo Bunge limekasimu kwake mamlaka ya kutunga Sheria kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) imeweka masharti maalum yanayotoa mamlaka kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya udhubiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoshauri na kuisimamia Serikali. Hii pia ni kwa sababu Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania. Shughuli hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula
- b) Ufugaji
- c) Uvuvi
- d) Biashara za mama lishe
- e) Biashara ya usafiri wa “bodaboda”
- f) Uchimbaji wa madini
- g) Utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii

1.3 Njia Zinazotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria hiyo inatakiwa kuwasilishwa Bungeni (*laid before the*

National Assembly) ndani ya siku sita (6) ya Vikao vya Bunge (*six sitting days*) katika Mkutano husika. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1). Matakwa haya ya Sheria yanapewa nguvu kupitia Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayosomeka kama ifuatavyo:-

“37. - (2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri ...”

Baada ya hatua hiyo, Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa mamlaka inayopatikana katika Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo ambazo hutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni ni kama zifuatazo:-

- a) Amri (*Orders*)
- b) Matamko (*Proclamations*)
- c) Kanuni za Taasisi (*Rules*)
- d) Kanuni za Mahakama (*Rules of Court*)
- e) Kanuni za Wizara (*Regulations*)
- f) Matangazo ya Serikali (*Notices*)
- g) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By - Laws*)
- h) Hati Idhini (*Instruments*)

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo hizi hutungwa na vyombo mbalimbali vya Serikali ambavyo vimekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (8) ya

Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

a) Kuandaa Orodha ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika kila Mkutano wa Bunge;

b) Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa;

c) Kuandaa Jedwali la Uchambuzi wa Kamati (*Matrix*) linalobainisha matokeo ya Uchambuzi wa Kamati na kuliwasilisha Serikalini ili iandae majibu ya hoja zilizoibuliwa kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni;

d) Kukutana na Wizara husika (*relevant Ministries*) ili kupokea majibu ya Serikali kutokana na Uchambuzi wa Kamati;

e) Kuwasilisha Bungeni Taarifa Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati na kutoa maoni na mapendekezo ili Bunge liridhie kwa Azimio la Bunge (*Parliamentary Resolution*) kwa ajili ya Utekelezaji wa Serikali;

f) Kufanya mafunzo na semina kuhusiana na Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo na namna ya uchambuzi wa Sheria Ndogo

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA KUENZIA JANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019

2.1 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Januari 2019 katika **Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa**

Kumi na Tatu wa Bunge, Serikali iliwasilisha Bungeni Jumla ya Sheria Ndogo Mia Saba na Nne (704) ikilinganishwa na Sheria Ndogo Mia Nne na Nne (404) zilizowasilishwa katika kipindi cha Mwaka 2017 – 2018, hivyo kwa mwaka 2018 – 2019 kumekuwa na ongezeko la Sheria Ndogo Mia Tatu (300) ambazo ni sawa na asilimia 74.2 ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa 2017 - 2018.

Katika kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo, Kamati ilibaini jumla ya Sheria Ndogo 395 kati ya 704 ambazo ni sawa na asilimia 56.11 zilizhitaji kufanyiwa uchambuzi ili kujiridhisha iwapo zinakidhi matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi. Aidha katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini jumla ya Sheria Ndogo Tisini na Tatu (93) kati ya Mia Tatu Tisini na Tano (395) ambazo ni sawa na asilimia 23. 5 zilikuwa na dosari mbalimbali, ambapo Kamati ilitoa Maoni na Mapendekezo ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo ni Kamati ya Sekta Mtambuka, Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari au masharti yake kuhitaji ufafanuzi wa kina kuhusu maudhui yake, ziligusa Wizara zifuatazo:-

- a) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
- b) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
- c) Wizara ya Fedha na Mipango;
- d) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
- e) Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji;
- f) Wizara ya Madini;
- g) Wizara ya Katiba na Sheria
- h) Ofisi ya Waziri Mkuu;

- i) Wizara ya Maji na Umwagiliaji;
- j) Ofisi ya Rais (TAMISEMI);
- k) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
- l) Wizara ya Nishati;
- m) Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
- n) Wizara ya Kilimo.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa, Kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na zifuatazo ni baadhi yake:-

- a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi;
- b) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu);
- c) Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (*Drafting Principles*);
- d) Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu; na
- e) Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (*unreasonable provisions*).

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika Mchakato

mzima wa Utungaji wa Sheria Ndogo ambazo zinachangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo zilifanyiwa uchambuzi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

a) Uchache wa wanasheria wenye taaluma ya uandishi wa sheria (*legislative drafters*) katika Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uhaba wa wataalamu hao unasababisha Sheria Ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (*Chief Parliamentary Draftsman*) kwa sababu naye siyo tu kwamba ana wataalamu wachache, lakini pia ana kazi nyingi.

b) Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno (*copying and pasting*) bila kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili Sheria Ndogo zisizoendana na uhalisia wa sababu na madhumuni ya kutungwa kwake.

c) Baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa mamlaka waliyopewa na Bunge ya kutunga Sheria Ndogo kuweka masharti ambayo aidha yalikataliwa au kupingwa na Kamati za Kudumu za Bunge wakati wa uchambuzi wa Muswada wa Sheria inayotoa madaraka (*Principal Act*). Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa na jukumu kubwa la kushughulikia dosari za masharti yaliyomo ndani ya Sheria Ndogo ambayo yangeweza kupatiwa uhalali kwa kuyaweka masharti hayo katika Sheria Mama.

d) Baadhi ya Mamlaka zilizokasimiwa Mamlaka ya Kutunga Sheria Ndogo, zimekuwa zikitunga Sheria Ndogo zinazopoka Mamlaka ya vyombo vingine vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria za Nchi ya kusimamia Mamlaka hizo. Mfano baadhi ya Kanuni za Wizara kuwa na vifungu ambavyo utekelezaji wake unaingiliana Mamlaka ya Mahakama. Pili Kanuni kuweka majukumu kwa Waziri anayosimamia na ambayo yanaingiliana na Mamlaka ya Waziri mwingine.

e) Baadhi ya Mamlaka zilizokasimiwa Mamlaka ya Kutunga Sheria Ndogo, zimekuwa zikitunga Sheria Ndogo pasipo kuona umuhimu wa kushirikisha wadau ambao ndio walengwa wa Sheria Ndogo husika. Hali hii imeleta changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya Sheria Ndogo.

2.3 Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge Serikali imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

2.3.1 Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo hamsini (50) ambazo ziligusa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Madini, hata hivyo baada ya uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa ni jumla ya Sheria Ndogo tano (5) tu ndizo zilikuwa na hoja 13 za kiuchambuzi. Hoja hizo zilikuwa ni tatu (3) kwa Wizara ya Fedha na hoja Kumi (10) kwa Wizara ya Madini, ambapo Kamati ilitoa maoni na mapendekezo ili kuondoa dosari hizo zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya kulitaarifu Bunge lako tukufu naomba nionyeshe baadhi ya dosari zilizoibuliwa na Kamati na baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika uchambuzi uliofanyika katika Sheria Ndogo ya ***The Oil and Gas (Revenues Management) Regulations, 2017*** ambayo imetungwa chini Sheria ya ***The Oil and Gas Revenues Management Act, Sura ya 328***. Kamati ilibaini Sheria Ndogo hii iliyo chini ya Wizara ya Fedha na kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi. Uchambuzi wa Kamati

ulibaini kuwa **Kanuni ya 4(2) (b)** ya Kanuni hizi inampa Waziri wa Fedha jukumu la kushiriki katika majadiliano ya Mikataba ya Kugawana Mapato (*Production Sharing Agreements*) katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa Kanuni hii imemuongezea Waziri wa Fedha Majukumu mapya ambayo hayatajwi katika **Kifungu cha 4** cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*The Oil and Gas Revenues Management Act*), Sura ya 328. Kwa mujibu wa **Kifungu cha 5 na 47** vya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 majukumu yanayoainishwa na Kanuni husika yanapaswa kutekelezwa na Waziri wa Nishati, TPDC na PURA kwa niaba ya Serikali. Majukumu haya hayaingiliani na yale ya Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*The Oil and Gas Revenues Management Act*).

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kwamba, **Kanuni ya 4 (2) (b)** ya Kanuni hizi inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*Intepretation of Laws Act*) Sura ya 1 ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ya **Kanuni ya 4(2) (b)** ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Sura 328.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Madini, pamoja na Sheria Ndogo nyingine Kamati pia ilifanyia uchambuzi wa Sheria Ndogo ya **The Mining (Local Content) Regulations, 2018**, ambayo imetungwa chini Sheria ya *The Mining Act*, Sura ya 123. Kamati ilibaini Sheria Ndogo hiyo ina vifungu vinavyokwenda kinyume na Sheria Mama. Dosari ilionekana katika **Kanuni ya 3** inayotoa tafsiri ya neno **Kampuni ya mzawa/wazawa (Indigenous Tanzanian Company)** kuwa ni ile inayomilikiwa kwa asilimia 51 na Mtanzania/Watanzania na ina asilimia 80 ya watanzania katika nafasi za watendaji wa juu.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati yalikuwa kwamba, tafsiri inayotolewa katika Kanuni hii haipo katika katika Sheria ya Makampuni Sura, 212 ambayo ndiyo Sheria Mama inayosimamia masuala yote ya Makampuni Nchini. Kamati iliona kwamba utaratibu wa kuanzisha tafsiri mpya ya maneno ni vema kuanzia katika Sheria Mama au Sheria nyingine ya Nchi ambayo ni mahususi kwa jambo fulani. Lengo la kufanya hivyo ni kuondoa uwezekano kuwa na maneno mbalimbali yanayofanana yenye tafsiri zinazo tofautiana.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati inachambua Kanuni ya *Local Content* katika sekta ya Madini, hususan The ***Mining (Local Content) Regulations, 2018 (GN. 3/2018)***, Kamati ilibaini kwamba tafsiri ya maneno "***Indigenous Tanzania Company***" na "***Indigenous Tanzanian Bank***" - ie. "***a bank that has one hundred percent Tanzanian or majority Tanzanian shareholding***" iliyotumika katika Kanuni hizo ina ukakasi. Pamoja na nia njema ya Wizara ya Madini ya kuweka tafsiri hizo, utekelezaji wake una changamoto na unaweza ukawa na matokeo hasi kwa kampuni kama ***Puma Energy Tanzania*** ambapo Serikali inamiliki asilimia hamsini (50%) ya hisa zote na kwa benki ya ***NBC Limited*** ambapo Serikali inamiliki asilimia kumi na tano (15%) ya hisa zote.

Sheria Ndogo hiyo haitambui umiliki wa hisa katika benki ya NBC na katika kampuni ya Puma kuwa ni umiliki wa watanzania na hivyo kuzikosesha kampuni hizo fursa ya kushiriki kiuchumi katika sekta ya madini. Halikadhalika benki na taasisi za fedha nyingi zilizosajiliwa hapa nchini ambazo hazimilikiwi na watanzania kwa asilimia mia moja au kwa hisa nyingi zitakosa fursa ya kushiriki kwenye sekta ya madini. Kamati haiamini kwamba haya ndio yalikuwa madhumuni ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa Kamati mnamo tarehe 27 na 28 Machi, 2018 uliohusisha Sheria Ndogo Tano (5) ambazo baadhi zimetolewa mfano hapo

juu. Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Nishati ili Kupokea majibu kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge.

Katika Majadiliano hayo na Kamati, Wizara ziliwasilisha majibu yao ambapo zilikubaliana na hoja zote kumi na Tatu (13) zilizoibuliwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo Tano (5). Wizara hizo zimeendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho.

2.3.2 Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge mnamo tarehe 9 Aprili, 2018 Serikali iliwasilisha mezani Sheria Ndogo Mia Moja Ishirini na Moja (121) zilizogusa Wizara mbalimbali. Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo, na baada ya uchambuzi, Kamati ilibainisha jumla ya Sheria Ndogo Tisa (9) zilikuwa na hoja ishirini na saba (27) za kiuchambuzi. Hoja hizo zilikuwa ni Tisa (9) kwa Wizara ya Ujenzi, hoja Moja (1) kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, hoja Mbili (2) kwa Wizara ya Nishati, hoja Tisa (9) kwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hoja Tatu (3) kwa Wizara ya Katiba na Sheria ambapo Kamati ilitoa maoni na mapendekezo ili kuondoa dosari hizo zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya kulitaarifu Bunge lako tukufu naomba nioneshe baadhi ya dosari zilizoibuliwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Sheria Ndogo ya *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* ambazo zimetungwa chini *The Urban Planning Act, Sura ya 355*, zilikuwa na maudhui yanayokiuka Katiba ya Nchi. Kamati ilibaini katika **Kanuni ya 5(2)** ambayo inaweka sharti la lazima kwa Mahakama mara baada ya kutoa uamuzi, kuwasilisha

nakala tatu za hukumu kwa Mamlaka ya Mipango Miji zinazoainisha sababu za kufikia maamuzi yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa utaratibu uliowekwa na Kanuni hii unaingilia mamlaka ya Mahakama ambayo inajiendesha kwa mujibu wa **Ibara ya 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977** na taratibu za Kimahakama zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa chombo kinachoweza kuamuru Mahakama kufanya jambo lolote kwa uamuzi iliyotoa ni Mahakama iliyo juu yake na si chombo au taasisi nyingine nje ya Mfumo wa Mahakama (*Judicial Hierarchy*).

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 kinaelekeza kuwa, Sheria Ndogo hazipaswi kuwa na vifungu vinavyokinzana na Sheria Mama iliyoianzisha au Sheria nyingine ya Nchi na ikitokea inakuwa na Vifungu vinavyokinzana, vifungu hivyo vitahesabika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia Kanuni ya *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* zinazoanzishwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*, Sura ya 355 ina masharti yanayokinzana na yale yaliyowekwa na Sheria nyingine ya nchi. **Kanuni ya 4 (b) (ii) (iii)** ya Kanuni hii, inaweka sharti kwamba mtu anayetaka kukata rufaa dhidi ya Mamlaka ya Mipango Miji, atapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji, orodha ya nyaraka anazotarajia kutumia katika rufaa yake pamoja na nyaraka ambazo hakuwahi kuziwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji katika hatua ya usikilizaji wa shauri la awali dhidi ya Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa utaratibu huo si sahihi kwa kuwa, katika hatua hii mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi wa aina yoyote kwa mrufaniwa mpaka pale ambapo kesi yake itakapokuwa imefikishwa mahakamani. Aidha katika hatua ya rufaa mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi mpya mpaka pale tu mahakama itakapona kuna haja ya kufanya hivyo ili kufikia maamuzi kama

inavyoonyeshwa katika **O. XXXIX R. 27** ya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, Sura 33 (*The Civil Procedure Code, Cap 33*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kwamba, kukinzana kwa Kanuni na Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi kama inavyoonekana katika Kanuni za *The Urban Planning (Appeals), Regulations*, 2018 ni kinyume na masharti ya **Kifungu cha 36 (1)** na **Kifungu cha 39(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo kamati ilikuwa na maoni kwamba, utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, unaifanya **Kanuni ya 4 (b) (ii) (iii)** ya *The Urban Planning (Appeals) Regulations*, 2018 kuhesabika kuwa ni batili kutokana na kukinzana na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa **Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, Sura 33** (*The Civil Procedure Code, Cap 33*).

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika na Kamati kuweka masharti yanayokinza na Sheria Mama ni *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini *The Urban Planning Act, Sura ya 355*. Uchambuzi wa Kamati umebaini dosari katika **Kanuni ya 3** ambayo inatoa tafsiri ya neno " *Vehicle* " ikihusisha vitu kama mkokoteni wa kuvutwa na ng'ombe, baiskeli ya matairi mawili, baiskeli ya matairi matatu. Tafsiri hii ni kinyume na ile inayotolewa na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 ambayo haijabainisha vifaa hivyo kuwa ni sehemu ya vyombo vya moto. Halikadhalika masuala ya vyombo vya moto kwa namna yoyote ile hayahusiani na maudhui ya Kanuni hii inayohusu masuala ya mipango miji.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kwamba, kuweka katika Sheria Ndogo maneno tofauti na yale yaliyotumika katika Sheria nyingine za nchi ni kinyume na **Kifungu cha 36(1)** na **Kifungu cha 39 (1)** cha Sheria ya Tafsiri za Sheria ambacho kinaeleza kwamba, maneno yatakayotumika katika Sheria Ndogo yanapaswa kuwa na maana sawa na yale yaliyotumika katika Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Kamati ilibaini dosari mbalimbali za kiuandishi katika Majedwali ikiwa ni pamoja na kutorejea Kanuni sahihi zinazoanzisha Majedwali husika kurejea Kanuni ambazo hazipo na Maudhui ya Jedwali kuwa tofauti na vifungu vya Kanuni.

Mheshimiwa Spika, dosari za uandishi wa Majedwali zilibainika pia Sheria Ndogo za *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* zilizotungwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act, Sura ya 355*. Kamati ilibaini dosari katika **Fomu Na 18 na Na. 19** katika **Jedwali la Nne**. Fomu hizo zinarejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 77(1) (r)** ambayo haipo katika Sheria Ndogo hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1, majedwali ni sehemu ya Sheria na husaidia kufafanua zaidi maudhui ya kifungu husika katika Sheria. Hivyo kwa Kanuni hizo zilizoonyeshwa kutoweka rejea sahihi za vifungu katika Majedwali husika, si tu zitasababisha changamoto ya usomaji bali pia zinafanya Majedwali hayo kukosa uhalali wa kuwepo katika Kanuni kwa kuwa hayajaanzishwa na vifungu sahihi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa Kamati mnamo tarehe 27 na 28 Machi, 2018. Kamati ilikutana Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Madini ili Kupokea majibu kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge. Katika Majadiliano hayo, Wizara zote mbili ziliwasilisha majibu yao ambapo zilikubaliana na hoja zote saba 13 zilizoibuliwa na Kamati na hivyo kuendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na kutangaza marekebisho hayo katika Gezati la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Aidha kuanzia tarehe 27 - 30 Agosti na 11 Septemba, 2018 Kamati ilikutana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Habari, Utamaduni,

Sanaa na Michezo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda na Wizara ya Katiba na Sheria ili Kupokea majibu kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge uliohusisha Sheria Ndogo Tisa (9) ambazo baadhi yake zimetolewa mfano hapo juu.

Katika Majadiliano hayo, Wizara zote Sita ziliwasilisha majibu yao ambapo zilikubaliana na hoja zote Ishirini na Saba (27) zilizoibuliwa na Kamati na hivyo kuendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na kutangaza marekebisho hayo katika Gezati la Serikali.

2.3.3 Utekelezaji wa Mapendekezo na Maoni yatokanayo na Uchambuzi wa Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 Iliyowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Bunge la Kumi na Moja Serikali iliwasilisha Mezani Sheria Ndogo mbalimbali ikiwemo **Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa, 2017 (GN Na. 43/2018)**. Mnamo tarehe 11 Septemba, 2018 Kamati ilikutana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) – ili kujibu hoja za kiuchambuzi zilizojitokeza katika Kanuni hizo, ambapo Mheshimiwa Waziri alikiri uwepo wa dosari nyingi katika Sheria Ndogo hiyo. Hivyo aliomba muda wa kuipitia upya ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuiwasilisha tena Kanuni hiyo mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 23 Januari, 2019 katika vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Kamati ilikutana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kupokea majibu ya utekelezaji wa hoja zilizojitokeza katika Uchambuzi wa Kanuni ya BASATA iliyowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge. Kabla ya kubainisha majibu ya Wizara, ni vema kulitaarifu Bunge kuhusu dosari zilizobainika katika Kanuni za BASATA:-

2.3.3.1 Sheria Ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.

Mheshimiwa Spika, katika Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 zilizotungwa chini ya **Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204**, Kamati ilibaini kuwa Kanuni zimewekewa masharti yasiyo na uhalisia. **Jedwali la Pili** la Kanuni hizi linatoa sharti kwa Kampuni kulipa ada ya shilingi milioni Tano iwapo litamtumia msanii kutangaza aina fulani ya bidhaa, halikadhalika Kanuni inaelekeza utaratibu wa malipo ya ada hiyo ambapo itatozwa kwa kila tangazo litakalorushwa hewani.

Mheshimiwa Spika, Masharti ya Kanuni hii si halisia kwa kuwa, yamewekwa kwa jumla pasipo kuzingatia mapato ya Kampuni husika inayotangaza biashara hiyo pamoja na mikataba iliyoingiwa kati ya Kampuni hiyo na msanii husika. Hali hii inaweza kuchangia kuzorotesha ustawi wa Kampuni ndogo ambazo zinatangaza bidhaa zake kwa lengo la kuongeza soko la bidhaa zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia **Kanuni ya 60 (1) (2) (3)** zinaweka masharti ambayo utekelezaji wake unaweza kuwa na changamoto kwa upande wa msanii pia Baraza la Sanaa la Taifa. Kanuni hizo zimeweka sharti kwamba, msanii anayetaka kufanya onesho nje ya nchi kuwa ni lazima aombe kibali kutoka BASATA na baada ya onesho msanii atapaswa kuwasilisha taarifa ya onesho hilo kwa BASATA, iwapo atashindwa kutekeleza hilo itakuwa ni sababu ya kunyimwa kibali cha kufanya maonesho nje ya nchi. Masharti ya Kanuni hii yanaweza kuchelewesha au kukwamisha shughuli za wasanii kutokana na hatua za vibali hasa pale ambapo Baraza lithitaji kufanya mawasiliano na waandaaji walio nje ya nchi. Aidha Kanuni haiweki bayana ni jinsi gani BASATA itajiridhisha na maudhui ya taarifa iliyowasilishwa na msanii kama ni halali na inalenga kueleza ukweli wa kile kilichofanywa na msanii nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo limebainika kuwa na dosari ni **Kanuni ya 64** ambayo imeainisha adhabu kwa wasajiliwa wa Baraza au mtu yeyote atakaye bainika kuvunja au kukiuka masharti ya Kanuni. Kamati inaona adhabu hizi ni kubwa na hazina uhalisia iwapo mtu atakiuka masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi. Mfano wa adhabu hizo ni Msajiliwa au mtu yeyote Kutozwa faini ya papo kwa hapo isiyopungua shilingi 1,000, 000/-; Kufungiwa kazi husika na kutozwa faini ya papo kwa hapo isiyopungua shilingi milioni tatu (Tshs. 3,000,000/=) au; Kuzuiwa kujishughulisha na kazi za sanaa maisha kwa kubainika kulingana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Spika, vilevile uandishi wa **Kanuni ya 64** haujaweka bayana kila kosa na adhabu inayostahili kuchukuliwa kwa mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi, badala yake adhabu zote zimewekwa kwa ujumla na zinaweza kutolewa kwa pamoja. Kamati inaona kwamba, ni vema uandishi wa Kanuni hii pamoja na masuala mengine uainishe adhabu kwa kosa mahususi badala ya adhabu zote kuwekwa sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Taarifa ya Baraza la Sanaa la Taifa, inaonyesha kuwa zaidi ya watanzania milioni Kumi (10) wanajishughulisha na kazi mbalimbali za sanaa, ambapo wamekua wanajipatia kipato ili kuendesha maisha yao ya kila siku. Hivyo Kamati iliona kuwa, adhabu zilizowekwa na Kanuni ikiwepo ile ya kumfungia maisha msajiliwa kujishughulisha na shughuli ya sanaa, itapelekea vijana wengi kushindwa kuendesha maisha yao ya kila siku na inaweza kusababisha vijana wengi kuingia katika makundi ya utumiaji wa madawa au hata kushiriki katika vitendo vingine vya uhalifu ili kuendesha maisha yao.

2.3.3.2 Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi uliofanywa na Kamati, ilibainika kwamba Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 imeweka Kanuni inayokinzana na Masharti ya Sheria Mama.

Sehemu ya Pili ya Kanuni hizi inazungumzia kuhusu utaratibu wa kuanziasha Kamati mbalimbali, mfano **Kanuni ya 6** inaeleza kwamba Baraza linaweza kuunda kamati na kamati ndogo za Mikoa na Wilaya ili kurahisisha utekelezaji wa kazi za Baraza kwa ujumla wake, ambapo Kamati zitakuwa ni Kamati ya Utendaji, Kamati ya Maendeleo ya Sanaa; na Kamati ya fedha, Mipango na Uchumi. Utaratibu huu unaowekwa na Kanuni hizi unakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama chini ya Kifungu cha 14 ambacho kinaweka utaratibu kwamba kutakuwa na Kamati za Baraza la Sanaa la Taifa linaweza kuanzaisha Kamati na kuzipatia majukumu pamoja na mipaka ya utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini eneo lingine linaloonesha kuwa **Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018** zimekiuka Masharti na Maudhui ya **Sheria ya Baraza la Sanaa, Na. 23 ya 1984. Jedwali la Pili** la Kanuni hizi pamoja na masuala mengine, limeainisha gharama mbalimbali zinazopaswa kulipwa kwa ajili ya vibali vya kumbi za maonesho ya sanaa na burudani. Utaratibu na malipo ya vibali vya kumbi za sanaa na burudani si moja ya majukumu ya Baraza la Sanaa la Taifa yaliyoainishwa kwa mujibu wa **Kifungu cha 4 cha Sheria ya Baraza la Sanaa, Na. 23 ya 1984** ambayo ndio imetoa Mamlaka ya kutungwa kwa **Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018**.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa kuweka utaratibu wa kusimamia vibali vya kumbi za sanaa na burudani sio tu ni kwenda kinyume na Sheria Mama, pia inafanya watoa huduma za kumbi hizo kuingia gharama mara mbili kwa kuwa Halmashauri nazo zimekuwa zikitoza ushuru mbalimbali kupitia huduma hizo. Hii inaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za kukodi kumbi za maonyesho ya sanaa na burudani.

Mheshimiwa Spika, aidha uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba maudhi ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 zimeingiza zaidi suala la udhibiti jambo ambalo

halielezwi na Sheria Mama kuwa ni sehemu ya majukumu ya Baraza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Kanuni hii inakwenda kinyume na **Kifungu cha 36 (1)** na **Kifungu cha 39 (1)** cha **Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1** vinavyoeleza bayana kuwa, vifungu vya Sheria Ndogo havipaswi kutofautiana na vile vya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi. Halikadhalika maneno yatakayotumika katika Sheria Ndogo yanapaswa kubeba maana ile ile iliyotumika katika Sheria Mama iliyozanzisha Sheria Ndogo husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dosari hizo zilizoainishwa hapo juu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeifahamisha Kamati kwamba, imepeleka mapendekezo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Barua yenye **Kumb. Na. DA. 31/339/01/88** ili kufanyia marekebisho ya **Sheria ya Baraza la Sanaa, Na. 23 ya 1984** katika maeneo yanayohusu adhabu kwa wasanii, majedwali kupishana na vifungu, tozo za kumbi za burudani, ada za matangazo ya biashara na uhibitaji wa vibali vya wasanii kwenda kufanya maonesho nje ya nchi.

Hatua ya kufanya marekebisho katika Kanuni za Baraza la Sanaa ni ya mpito ili kuondoa changamoto zilizobainika katika Kanuni kwasasa. Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa Sera ya Utamaduni ambayo itapelekea kuandikwa upya kwa Sheria ya BASATA ambayo itakuwa na ushirikishaji mpana wa wadau wote wa kazi za sanaa.

2.4 **Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge**

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii pia inahusisha uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge. Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo pia umetekelezwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, hata hivyo taarifa zake hazikuwasilishwa Bungeni kama ilivyokuwa kwa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani katika Mkutano wa Kumi na

Kumi na Moja, ambazo taarifa yake liliwasilishwa Bungeni mnamo tarehe 13 Septemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba niwasilishe uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge ili bunge liweze kuazimia maoni na mapendekezo ya Kamati.

2.4.1 **Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Mbili**

Mheshimiwa Spika, Katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge Serikali iliwasilishe Mezani Sheria Mia Tatu Thelathini na Nne (334). Sheria Ndogo hizo ziligawanyika katika mchanganuo ufuatao:-

- a) Miongozo (*Guidelines*) - 14;
- b) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By- Laws*) – 143;
- c) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 64;
- d) Kanuni za Taasisi (*Rules*) – 17;
- e) Amri (*Orders*) – 23;
- f) Matangazo (*Notices*) – 72; na
- g) Hati Rasmi (*Instruments*) – 1.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa Sheria Ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo hamsini (50). Baada ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Sheria hizo kama inavyoonekana katika **Jedwali la Uchambuzi** lililoambatishwa. Kwa ajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

2.4.1.1 Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na vyombo mbalimbali vilivyokasimiwa jukumu la kutunga Sheria Ndogo zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au Sheria Nyingine za Nchi. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo iliyobainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi ni *The Tanzania Communications Regulatory Authority (Complaints Committee) Rules, 2018 (GN Na. 203/2018)* ambazo zimetungwa chini Sheria ya *The Tanzania Communications Regulatory Authority Act Na. 12/ 2013*. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, **Kanuni ya 21 (1) (2)** inatoa haki ya kukata rufaa kwenda Baraza la Usuluhishi (*Fair Competition Commission*) kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Hata hivyo Kanuni ya 21 (2) imeainisha sababu tatu za rufaa ambazo mrufani atapaswa kuwasilisha katika Baraza la Usuluhishi.

Uandishi wa **Kanuni ya 21(2)** ni kinyume na **Kifungu cha 42 (3)** Sheria Mama ya *The Tanzania Communications Regulatory Authority Act, Na.12 / 2003* ambayo imeainisha sababu Nne za rufaa ikiwemo sababu inayoonesha kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania haikuwa na uwezo wa kuamua shauri. Kimsingi sababu hiyo ya rufaa haipo katika Sheria Ndogo ya *The Tanzania Communications Regulatory Authority (Complaints Committee) Rules, 2018*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Kanuni hii kutokuweka sababu ya rufaa kwamba, **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania haikuwa na uwezo wa kuamua shauri**, sio tu imepunguza wigo wa sababu za rufaa ambazo mrufani anaweza kutumia kwenda katika baraza la

Usuluhishi, bali pia inaweza kusababisha Mamlaka kuamua mashauri ambayo haina uwezo nayo (*powers to determine*) na maamuzi hayo kutoweza kupingwa mahali popote.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwa, Kanuni ya *The Tanzania Communications Regulatory Authority (Complaints Committee) Rules, 2018* chini ya **Kanuni ya 21(3)** inatamka kuwa uamuzi wa Baraza la usuluhishi utakuwa ni wa mwisho. Kamati inaona kwamba, Masharti ya Kanuni hii hayakupaswa kuwa sehemu ya Kanuni hizi, kwa kuwa masuala haya yalipaswa kuwa katika Sheria ya *The Fair Competition Act*, na Kanuni zake zinazoiainisha hatua zinazoweza kufuatwa na mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza la Usuluhishi.

Kamati inaona kwamba, masuala yanayohusu Baraza la usuluhishi yanaangukia chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na uwekezaji ambayo ndio inasimamia Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya ushindani na si Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo dosari katika Kanuni ya 21(1) na 21(3) ya Kanuni hizi zinaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya *The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas Operations) Rules, 2018 (GN. Na. 376/2018)* ambayo imetungwa chini Sheria ya *The Petroleum Act, Sura 392* na kubaini kuwa ina kifungu kinachokwenda kinyume na Sheria Mama ya *The Petroleum Act, Sura 392*. Kamati imebaini dosari katika **Kanuni ya 5** ya Sheria Ndogo hii, ambayo inatamka kwamba mtu yeyote atakayejenga miundombinu ya gesi pasipo kupata kibali cha EWURA kuwa atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini au kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozi miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, adhabu inayotolewa na Kanuni hii imeweka ukomo wa juu wa adhabu ya Kifungo kuwa ni miaka mitano kwa mtu aliyetenda kosa hilo. Adhabu hii, ni tofauti na ile iliyowekwa na **Kifungu cha 127 (2) cha Sheria ya Petroli, 2015 Sura 392 (Sheria Mama)** ambacho hakiweki ukomo wa juu wa adhabu kwamba kifungo kisizidi muda wa miaka mitano, badala yake imeacha utashi huo kwa watoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kamati inaona kwamba, uandishi wa kuweka ukomo wa juu wa adhabu katika Kanuni ya 5 ni mzuri kwa kuwa unaondoa uwezekano wa watoa maamuzi kutumia vibaya utashi (*discretion*) waliopewa katika kutoa maamuzi. Hata hivyo, licha ya maudhui mazuri ya Kanuni hiyo, ukweli unabaki kuwa, Kanuni hiyo inatofautiana na **Kifungu cha 127(2)** cha Sheria Mama ambacho hakiweki ukomo wa juu wa adhabu ya kifungo kuwa ni miaka mitano.

Kamati iliona kwamba, kutofautiana kwa Kanuni ya *The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas Operations) Rules, 2018* na Sheria Mama ya *The Petroleum Act, Sura 392* ni kinyume na **Kifungu cha 36 (1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachobainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Magulio) za Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, 2018 (GN Na. 351/2018)** ambayo imetungwa chini Sheria ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290** na kubaini kuwa ina kifungu kinachokwenda kinyume na Sheria nyingine za Nchi. Kamati ilibaini kuwa **Kifungu cha 15 (2)** cha Sheria Ndogo hizi, kinatoa Mamlaka kwa Mkuu wa Soko kwa kushirikiana na Kamati ya Wadau kufunga Soko kwa sababu za dharura baada ya kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika.

Kamati iliona kuwa utaratibu uliowekwa na Kifungu hiki cha Sheria Ndogo hii hautoi haki ya kupata taarifa kwa Jamii

husika (Umma) pamoja na watu wanaofanya biashara katika maeneo hayo kuhusu mpango wa kufunga Soko au Gulio husika, ambao kimsingi ndio wanufaika wa Masoko/ Magulio hayo. Ni vema Sheria Ndogo ikabainisha pia wajibu wa utoaji wa taarifa kwa umma ili waweze kufahamu kuhusu kufungwa kwa soko kwa kuwa wao ni wanufaika wa huduma inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yaliyotolewa kuhusu Maudhui ya **Kifungu cha 15 (2)** cha Sheria Ndogo, Kamati iliona kwamba Kifungu hiki kinakinzana na matakwa ya **Kifungu cha 5** cha **Sheria ya Kupata Habari (*The Access to Information Act, 2016*)**, 2016 ikisomwa pamoja na **Ibara ya 18 (2)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977** ambazo zinazungumzia kuhusu suala la haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini ambayo yanahusiana na maisha na shughuli za wananchi, halikadhalika masuala muhimu yanayohusu jamii. Hivyo ni vema Sheria Ndogo hii kuandikwa vizuri kwa kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine za Nchi.

2.4.1.2 Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali kutofautiana na Vifungu vinavyo yaanzisha)

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Kamati ilibaini pia baadhi ya Sheria Ndogo kuwa na Makosa ya uandishi katika Majedwali, kwa mfano Sheria Ndogo ya ***The Tax Revenue Appeals Tribunal, Rules 2018 (GN Na. 222/2018)***, ambayo imetungwa chini Sheria ya ***The Tax Revenue Appeals Act, Sura 408***.

Kama zilivyo sheria nyingine, sheria hii pia ina Majedwali ambayo yanaweka ufafanuzi wa Kanuni mbalimbali katika Sheria Ndogo hii. Hata hivyo Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha Majedwali. Kwa mfano, **Fomu Na. TRT. 3** iliyopo katika Jedwali la Kwanza inafanya rejea ya kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 9 (3)** ambayo kimsingi

haipo katika Sheria Ndogo hizi. Kamati imeona kwamba rejea sahihi yenye maudhui yanayoendana na **Fomu Na. TRT. 3** yanaainishwa chini ya **Kanuni ya 10 (2)**.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini dosari mbalimbali katika uandishi wa Majedwali katika **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Magulio) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, 2018 (GN Na. 330/2018)** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290**. Mfano, Sheria Ndogo hii imeonesha kwamba Jedwali la Kwanza linaanzishiwa chini ya **Kifungu cha 5 (1)**, hata hivyo baada ya uchambuzi imebainika kuwa rejea ya Kifungu haina usahihi, kwa kuwa kifungu hicho kinazungumzia kuhusu wajibu wa Halmashauri na si masuala yaliyoainishwa katika Jedwali yanayohusiana na ushuru. Kamati imeona kwamba, kurejea sahihi ya kuanzisha Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo ni **Kifungu cha 4** ambacho ni mahsusii kuhusu masuala ya Ushuru ambayo ndiyo yanaainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati pia ulibaini **Sheria Ndogo ya The Fair Competition, Rules 2018 (GN Na. 344/2018)** ambazo zimetungwa chini ya **The Fair Competition Act, Sura 285** ina dosari nyingi za uandishi wa Majedwali. Mfano wa dosari hizo ni katika **Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizi ambalo liliandikwa pasipo kuweka rejea ya Kanuni inayolianshiza. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, maudhui ya Jedwali la Kwanza yanaendana na yale yaliyopo katika Kanuni ya 8 ya Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kwamba ni vema uandishi wa Majedwali katika sheria uzingatie kurejea Kanuni sahihi zinazoanzisha Majedwali husika, kwa kuwa Majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni husika katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika.

2.4.1.3 Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uchapaji na kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria (*Drafting Principles*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini jumla ya Sheria Ndogo mbili zina dosari za kiuchapaji na uandishi. Mfano ni **Sheria Ndogo za (Ushuru za Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, 2018 (GN Na. 346/2018)** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290**, Sheria Ndogo imebainika kuwa na makosa ya kiuandishi ambapo inaonekana ina Majina ya Halmashauri mbili yaani, moja ni **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Muleba** na jina lingine ni **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Pangani**.

Mheshimiwa Spika, Aidha Kamati ilibaini pia, Sheria Ndogo ya ***The Railway (Safety Standards of Infrastructure and Rolling Stock) Regulations, 2018 (GN. Na. 401/2018)*** ambazo zinaanzishwa chini ya ***The Railway Act, (Na. 10/2017)*** ina Majina ya Kanuni mbili tofauti, moja ni Kanuni ya ***The Social Security Regulatory Authority (Annual Levy), 2018*** na jina lingine ni ***The Railway (Safety Standards of Infrastructure and Rolling Stock) Regulations, 2018***. Kamati ilibaini kuwa pamoja na kuwa dosari ya kuweka majina mawili, Sheria Kanuni hizi zimetungwa na kusainiwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mwenye Mamlaka na ***The Railway (Safety Standards of Infrastructure and Rolling Stock) Regulations, 2018***.

Mheshimiwa Spika, dosari ya Sheria Ndogo kutofuata misingi ya uandishi imebainika pia katika Kanuni za ***The Public Health (Water Borne, Water Washed and Other Water Related Diseases Prevention) Regulations, 2018 (GN Na. 175/2018)*** zilizotungwa chini ya Sheria ya ***The Public Health Act, Sura 99***. Vifungu vyote vya Sheria Ndogo hii vimeandikwa pasipo kuwekewa maelezo ya pembeni ya Kifungu (*Marginal notes*), hali ambayo inachangia changamoto katika usomaji mzuri wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, dosari za kiuandishi zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati, zinaweza

kusababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake.

2.4.1.4 Sheria Ndogo kuweka Vifungu visivyo na Uhalisia (Unrealistic Provisions)

Mheshimiwa Spika, katika utungaji wa Sheria pamoja na masuala mengine huzingatia uwekaji wa vifungu ambavyo utekelezaji wake unakuwa na uhalisia na kutokuwa kandamizi kwa watumiaji wa Sheria Ndogo husika. Uchambuzi wa Kamati umebaini Sheria Ndogo moja ina vifungu visivyo na uhalisia. Mfano, sehemu ya Saba ya **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, 2018 (GN Na. 235/2018)** zilizoanzishwa chini ya Sheria ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290** inaweka viwango vya ushuru wa kupakua na kushusha mizigo sokoni, ambapo muhusika atapaswa kulipa Tshs. 50,000/- kwa kila tani ya mazao atakayoshusha ikiwemo matunda ya aina zote yatakayoshushwa katika eneo la soko na maeneo mengine ya Halmashauri.

Aidha Sehemu hii ya **Saba ya Jedwali la Kwanza** inaweka viwango vya ushuru wa bidhaa za viwandani zitapakiwa au kupakuliwa sokoni kuwa zitatozwa kiwango Tshs. 2,000/- kwa kila katoni itakayopakiwa au kupakuliwa katika eneo la soko na maeneo mengine ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, viwango vya ushuru vilivyowekwa kwa ushushaji wa tani za mazao yakiwemo matunda pamoja na katoni za bidhaa mbalimbali za viwandani vinaweza kukosa uhalisia kwa baadhi ya bidhaa zinazotozwa. Hii ni kwasababu faida inayopatikana kutokana na kuuzwa kwa aina fulani ya katoni za bidhaa za viwandani ni ndogo kuliko kiwango cha ushuru wa Tshs. 2,000/- kinachotozwa kwa kila katoni kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa vipindi tofauti Serikali imeonesha jitihada za dhati zenye lengo la kukwamua

wakulima na wafanyabiashara kwa kuondoa tozo mbalimbali ambazo ni kero. Hivyo Kamati inaona kwamba, Sheria Ndogo hii inaweza irekebishe vifungu ambavyo utekelezaji wake unaweza kuwa na changamoto wakati wa utozaji wa ushuru. Hali hii ya utozaji wa viwango vya ushuru vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo vinaweza kusababisha wafanyabiashara kutoleta aina fulani za bidhaa katika masoko na hivyo kupelekea upungufu wa bidhaa hizo.

2.4.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, Katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge Serikali iliwasilisha Mezani Sheria Mia Moja Sabini na Tisa (179). Sheria Ndogo hizo ziligawanyika katika mchangano ufuatao:-

- a) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) – 70;
- b) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 10;
- c) Kanuni za Taasisi (*Rules*) – 3;
- d) Amri (*Orders*) – 50; na
- e) Matangazo (*Notices*) – 46

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Ishirini na Sita (26), ambapo imetoa Maoni na Mapendekezo kwa lengo la kuboresha maudhui ya Sheria hizo kama inavyoonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa ajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, naomba kunainisha baadhi ya dosari kama ifuatavyo:-

2.4.1.5 Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini Sheria Ndogo kuweka vifungu vinavyokinzana na Sheria Mama. Mfano wa Sheria Ndogo hizo ni Sheria ya ***The Petroleum (Natural Gas) (Processing) Rules, 2018*** iliyotungwa chini ya Sheria ya Petroli yaani ***The Petroleum Act, Sura 392. Kanuni ya 43 (2)*** ya Sheria Ndogo inaweka adhabu kwa mtu atakayejenga miundombinu ya Gesi pasipo kupata kibali cha EWURA atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja. Hata hivyo adhabu inayotolewa na Kanuni hii ni tofauti na ile inayotolewa na **Kifungu cha 127 (2)** cha **Sheria ya Petroli** ambacho kinaeleza adhabu isipungue miaka miwili na pia hakiweki ukomo wa juu wa adhabu wa kifungu kwa muda wa miaka mitano.

Kamati inaona kwamba, dosari hii ni kinyume na **Kifungu cha 36 (1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya ***The Commission Of Human Rights And Good Governance (Appointments Procedure For Commissioners) Regulations, 2018*** ambayo imetungwa ***The Commission For Human Rights And Good Governance Act 391***. Kamati imebaini kuwa Kanuni ya **2** ya Sheria Ndogo hii inakwenda kinyume Sheria Mama kwa kutoa Tafsiri ya maneno **Chairman** na **Vice - Chairman** ambayo yanakosa msingi wa Kikatiba na Kisheria kwa kuwa haifanyi rejea ya **Ibara ya 129(2) (a)-(b)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na **Kifungu cha 7 (1) (a)** cha **Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura 391**. Kamati naona kwamba, ni vema tafsiri ya maneno hayo ingezingatia rejea ya tafsiri ya maneno Kamishna na Makamishna Wasaidizi iliyorejea Katiba ya nchi na Sheria Mama kwa kuwa maneno husika ni zao la sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo Tatu (3) zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambazo ni *The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Registration, Branding, Labeling and Sealing) Regulations, 2018*, *The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Registration of Animal Feed Resources Products) Regulations, 2018* na *The Grazing Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resources) Regulations 2018*.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Kanuni hizi zina dosari hasa ile ya kukinzana na Sheria Mama ya *The Grazing-Land and Animal Feed Resources Act, Sura 180*. Mfano katika Sheria Ndogo ya *The Grazing Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resources) Regulations 2018* ambapo **Kanuni ya 20** inatoa adhabu kuhusu mtu atakayekiuka masharti ya yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi kuwa ikithibitika atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au adhabu zote kwa pamoja. Adhabu hii haipo kwa mujibu wa adhabu zinazotolewa na Sheria Mama. Dosari hii ni kunyume na **Kifungu cha 36(1)** ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 inayotaka Sheria Ndogo kutokinzana na Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 22 Januari, 2019 Kamati ilikutana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kupokea majibu kutokana na dosari zilizoibuka katika Kanuni hizo. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi alifafanua kwamba kuna Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Mama ya *The Grazing-Land and Animal Feed Resources Act, Sura 180* ambayo hayajawasilishwa Bungeni. Marekebisho hayo yamebeba mambo mengi yaliyojitokeza katika Kanuni hizi. Kutokana na ushauri wa Kamati, Waziri aliiambia Kamati kwamba, anasitisha matumizi ya Kanuni hizi mpaka pale marekebisho ya Sheria Mama yatakapowasilishwa na Kupitishwa na Bunge.

2.4.1.6 Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini **Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala, 2018** ambayo imetungwa chini ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290** ina dosari nyingi za uandishi wa Majedwali. Mfano **Jedwali la Saba** linafaya rejea ya **Kifungu cha 4 (2)** ambacho hakipo, hata hivyo rejea sahihi iliyopaswa kurejewa **Kifungu cha 7(3) (i)**. Aidha **Jedwali la Nane** pia makosa ya rejea ya Kifungu kinachoanzisha Jedwali hilo. Sheria Ndogo inafanya rejea ya **Kifungu cha 4 (3)** kuanzisha Jedwali hilo, kimsingi kifungu hicho hakipo katika Sheria hizi, Kamati inaona kuwa rejea sahihi iliyapaswa kuwa ni **Kifungu cha 7(4)**.

Mheshimiwa Spika, Ni vema uandishi wa Majedwali katika Sheria Ndogo uzingatie kurejea sahihi ya Kanuni zinazoanzisha Majedwali husika, kwa kuwa Majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni husika katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa Sheria husika.

2.4.1.7 Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (*Drafting Principles*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini baadhi ya Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika vifungu. Mfano ni **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, 2018** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 290**. Vifungu vya 10, 11 na 12 vimebainika kutoweka mpangilio mzuri wa maelezo ya vifungu (***Marginal Notes***) ambapo maelezo ya **Kifungu cha 11** yamewekwa katika **Kifungu cha 10** na yale ya **Kifungu**

cha 12 kuhusu kufuta Sheria ya mwaka 2014 yamewekwa katika **Kifungu cha 11** kinachohusu kufifilisha kosa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini **Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Kondoa, 2018** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288** imeweka vifungu visivyo na masharti mahsusi (*Specific*). **Kifungu cha 4** kinaeleza kuwa Halmashauri itaamua ni kiasi gani cha mifugo kinapaswa kufugwa katika maeneo mbalimbali. Aidha **Kifungu cha 5 (e)** cha Sheria Ndogo kinaweka katazo kuwa ni marufuku mfugaji kufuga mifugo mingi katika eneo dogo.

Mheshimiwa Spika, Kimsingi kutoweka idadi ya mifugo inayotakiwa na ukubwa wa eneo kwa kulinganisha na idadi ya mifugo. Maudhui ya Vifungu hivi yanaweza kutekelezwa vibaya na wasimamizi ya Sheria Ndogo hii.

Kamati ina maoni kwamba, ni vema **Halmashauri ya Mji wa Kondoa** na Halmashauri nyingine nchini zenye Sheria zilizo na masharti kama haya zizingatie agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alilolitoa tarehe 15 Januari, 2019, ambapo pamoja na masuala mengine, ameziagiza Mamlaka husika kubainisha maeneo ya hifadhi za wanayamapori na misitu ambayo hayana wanyamapori na misitu ili yagawiwe kwa wakulima na wafugaji kwa kuwa wanapata taabu ya maeneo ya kufugia na kuzalisha mazao.

Hivyo basi, ni vema kuondoa vifungu vinavyoendelea kuwanyima haki wafugaji na badala yake wajielekeze katika maagizo ya Mhe. Rais kwa kuwasiliana na Mamlaka husika zilizopewa jukumu hilo ili kuondoa changamoto zinazowakabili Wakulima na Wafugaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati imebaini baadhi ya Sheria Ndogo kuweka vifungu visivyo wazi na mahususi (*Specific*). Mfano ni **Kifungu cha 5(3)** cha **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, 2018** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha za**

Serikali za Mitaa, 290 kinatoa sharti kuwa, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga machimbo yoyote ya madini ya ujenzi kama itaona kufanya hivyo ni **kwa maslahi ya Halmashauri na umma kwa ujumla**.

Kifungu hiki hakijaweka bayana aina ya maslahi ya Umma yanayokusudiwa katika Sheria hii na wala sheria haitoi tafsiri ya mantiki ya Maslahi ya Umma, ili kuepuka matumizi mabaya ya Mamlaka hayo wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. Aidha Kifungu hakijaweka sharti la halmashauri kutoa taarifa kwa mchimbaji wa madini kabla ya kusitisha leseni husika, halikadhalika kifungu hakijaonyesha sharti la fidia kwa mtu anayesitishiwa leseni yake kwa kigezo cha kuwepo kwa maslahi ya umma ili kufidia gharama za alizowekeza katika machimbo husika.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi unahitaji mtaji mkubwa ambapo wachimbaji hupata mitaji kupitia mikopo kutoka Taasisi mbalimbali za fedha ili kufanikisha shughuli hizo. Hivyo kitendo cha Halmashauri kufuta leseni pasipo kuonyesha hatua na taratibu za ufutaji wa leseni husika kunaweza kusababisha hasara kubwa kwa wawekezaji waliofutiwa leseni. Kamati ina maoni kuwa ni vema kifungu hiki kikafanyiwa marekebisho ili kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini **Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala, 2018** imeweka Kifungu kuhusu malipo ya faini pasipo kuanisha kiwango stahiki.

Kifungu cha 6 (2) kinatamka kuwa, Mfugo wowote utakao kamatwa ukizurura ovyo utatozwa faini na gharama nyingine zitakazojitokeza kama itakavyoamriwa na Halmashauri. Sheria Ndogo hizi kutoainisha wazi viwango vya faini vitakavyolipwa kunaweza kukwamisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi hasa kutokana na matumizi mabaya ya kifungu hiki kutokana na kukosa uwazi wa viwango vya faini.

Mheshimiwa Spika, Aidha utaratibu uliowekwa na Kifungu hiki umekuwa ukileta changamoto kubwa hapa nchini, ambapo mifugo hukamatwa na wafugaji kujikuta wanatozwa faini kubwa na zisizo na uhalisia kwa kadri ambavyo halmashauri zinaona inafaa. Hali hii imepelekea wafugaji kujikuta wakishindwa kulipa viwango hivyo vya faini na kupelekea mifugo yao kupigwa mnada.

Aidha kwa minajili ya uandishi wa Sheria, utaratibu huu wa utozaji wa viwango vya ushuru ni Kinyume na masharti ya **Kifungu cha 43 (2) (a)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 kinachotamka kwamba iwapo Sheria Ndogo inaweka viwango vya ada au tozo, vinapaswa kuwa mahsusii/maalum (*Specific*).

2.4.1.8 Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu

Mheshimiwa Spika, katika Sheria Ndogo ya *The Commission Of Human Rights And Good Governance (Appointments Procedure For Commissioners) Regulations, 2018* ambayo imetungwa *The Commission For Human Rights And Good Governance Act 391*. Kamati ilibaini **Kanuni ya 7(1)** ya Kanuni inatoa sharti kuwa, hatua ya kuutangazia umma orodha ya Majina ya walioomba nafasi za Ukamishna itaruhusu umma/Wananchi kuwasilisha maoni yao kwa Katibu wa Kamati ya Uteuzi dhidi Majina husika. Aidha, **Kanuni ya 7(2)** inatamka kuwa Kamati ya Uteuzi inaweza kukubaliana na Maoni ya Wananchi/Umma na kuyafanyia kazi kwa namna itakavyoona inafaa.

Maoni ya Kamati ni kuwa, Kanuni hii haiainishi utaratibu na vigezo vitakavyotumika kukataa au kukubali maoni ya Wananchi na wala haitoi utaratibu utakaowezesha Mwombaji wa Ukamishna aliyetajwa au kutolewa maoni hasi dhidi yake kupata haki ya kujitetea kabla ya Kamati ya Uteuzi kufanya maamuzi, hivyo ni vyema Kanuni ingeinisha na kuzingatia haki ya kujitetea kwa mujibu ya **Ibara ya 13(6) (a)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977**.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

- a) Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Bungeni tangu Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge ambazo zimebainika kuwa na makosa ya kiandishi na kiuchapaji ili kuondoa dosari hizo na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali kufikia Mkutano wa Kumi na Tano Bunge.
- b) Kamati inashauri Mamlaka zilizokasimiwa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kuhakikisha vifungu vya sheria mbalimbali za Halmashauri vyenye maudhui yanayofanana viwe na uandishi wa mtiririko wa maudhui unaofanana kwa kuzingatia mazingira ya utekelezaji wa Sheria hizo.
- c) Kamati inashauri Mamlaka zinazopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo zishirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hatua za uandaaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.
- d) Kamati inaishauri Serikali iendelee na programu za utoaji wa mafunzo ya uandishi wa sheria kwa Maafisa Sheria. Mafunzo hayo yatasaidi kupunguza makosa ya uandishi katika Sheria Ndogo kabla ya Sheria Ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.
- e) Kamati inashauri kuwa, Mamlaka/ Taasisi zilizokasimiwa Mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo zishirikishe wadau katika hatua za mwanzo za uandaaji wa Sheria Ndogo. Lengo ni kupunguza au kuondoa changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo husika.
- f) Kamati inashauri Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo kuepuka mtindo wa kunakili (***Copy and Pasting***) Sheria. Kwa kufanya hivyo itasaidia makosa yaliyo katika Sheria Ndogo yanayotumika katika eneo moja la utawala

kutohamishiwa katika Sheria Ndogo inayoenda kutumikaeneo jingine.

g) Kamati inashauri Taasisi/Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo kuacha kutunga Kanuni ambazo zinaweka vifungu vinavyonyang'anya majukumu ya Vyombo/Mamlaka nyingine za nchi.

3.1 Maoni na Mapendekezo kwa Serikali Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yameandaliwa kwa muhtsari kuzingatia matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Kumi na Tatu wa Bunge na yamefafanuliwa kwa kirefu katika Jedwali la Uchambuzi ambalo limeambatishwa na Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

3.1.1 Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

3.1.2 Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi;

NA KWA KUWA, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi;

NA KWA KUWA, kukinzana huko kunaharamisha Kanuni husika kwa kiwango ilichokinzana na Sheria Mama;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, zifanye marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi.

3.1.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria (*Drafting Principles*)

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kwamba baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

NA KWA KUWA, dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

3.1.4 Masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

NA KWA KUWA, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasio na uhalisia zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

3.1.5 Kukiuka Misingi ya Haki za Binadamu

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika Sheria Ndogo kuwa na dosari ya kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu;

NA KWA KUWA, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kubinya haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na vyombo vyenye Mamlaka ya kutoa maamuzi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambayo Sheria Ndogo yake imebainika kuwa na dosari za kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu, ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
4. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb
5. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
6. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb
7. Mhe. John John Mnyika, Mb
8. Mhe. Halima James Mdee, Mb
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
10. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb
11. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb
13. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb
14. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb
15. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb
16. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
18. Mhe. Mary Deo Muro, Mb
19. Mhe. Easther Lukago Midimu, Mb
20. Mhe. Catherine Nyakao Ruge, Mb

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (Sheria Ndogo) kwa wakati, pia uratibu mzuri wa uwasilishaji wa Jedwali la Uchambuzi kwa Wizara husika ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda wote imekuwa ikiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele

ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika Sheria Ndogo. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

- a) Mhe. Jenista Mhagama (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu;**
- b) Mhe. William Lukuvi (Mb) – **Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;**
- c) Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) - **Waziri wa Maji na Umwagiliaji;**
- d) Mhe. Selemani Jaffo (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya (TAMISEMI);**
- e) Mhe. Umy Mwalimu (Mb) – **Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;**
- f) Mhe. Dkt. Philip Mpango (Mb) – **Waziri wa Fedha na Mipango;**
- g) Mhe. Dkt Harrison Mwakyembe (Mb) – **Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**
- h) Mhe. Charles Mwijage (Mb) – **Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji;**
- i) Mhe. Luhaga Mpina (Mb) – **Waziri wa Mifugo na Uvuvi;**
- j) Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Mb) – **Waziri wa Nishati;**
- k) Mhe. Eng. Isack Kamwelwe (Mb) – **Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;**
- l) Mhe. Dr. Charles Tizeba (Mb) – **Waziri wa Kilimo;**

m) Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) – **Katiba na Sheria**; na

n) Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb) – **Naibu Waziri wa Madini**;

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili, na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO
8 Februari, 2019

MWENYEKITI: Waheshimiwa sasa tunaanza kuchangia, tunaanza na Mheshimiwa Kahigi, atafuata Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Lema ajiandae.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Kamati yangu ya Katiba na Sheria. Naipongeza Kamati yangu ya Katiba na Sheria kwa ushauri wao mzuri walioutoa, naiomba Serikali ipokee mapendekezo yao na iyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Kamati yangu ya Katiba na Sheria tumeshauri bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria inapotolewa katika Bunge itolewe kwa muda muafaka ili iweze kufanya kazi maana vijijini huko mahakama za wilaya ni chache na mahakama za mwanzo nyingi zimechoka kwa kuwa ni za muda mrefu, zina nyufa. Tunaomba wawe wanapewa hilo fungu ili waweze kujenga mahakama maana wananchi wanatembea mwendo mrefu kwenda kwenye kesi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeshauri Majaji, Mahakimu wa ngazi za chini waweze kupewa mafunzo, waweze kufanya kazi zao kwa weledi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tumeshauri, Mahakama Kuu hawana mashine maalum, watu wakienda pale wanakwenda kwa kupapaswa wakiwa wanaingia ndani, hiyo na yenyewe ni hatari, ni vizuri na wenyewe wawekewe mashine maalum wasiwe wanaingia hivihivi maana kwenye viwanja vya ndege, sehemu zingine hata na makanisani mahali pengine wana mashine za kuangalia wale watu wanaoingia mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tumeshauri kwenye magereza, kuna wafungwa ambao wamekaa muda mrefu ambao wana wenzi wao, kama ni wanaume wameacha wake zao nje, kama ni wanawake wameacha waume zao nje, ni haki yao kutimiza tendo la ndoa. Tumeshauri mkakati ufanyike watengenezewe

sehemu wawe wanakutana maana mtu kukaa miaka kama sita, saba mbegu za uzazi zinaweza zikaharibika, lakini kama wakitengenezewa sehemu ni vizuri na wenyewe wakaweza kukutana, tendo la ndoa ni haki yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tumeshauri katika Kamati yangu, upande wa mahakama, Majaji na Mawakili wanapaswa wapewe weledi wa hali ya juu sana, wapewe semina ili waweze kufanya kazi zao vizuri, pale Mawakili wanapotetea wateja wao waweze kutetea kwa umahiri sana, bila kuwapa kozi za maana wanaweza wakafanya mambo ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo machache, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, jandae Mheshimiwa Lema.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja za Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nishukuru na kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati, ama kweli ripoti hii wameitendea haki. Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza jemedari wetu, Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoiongoza nchi na kwa namna anavyoonesha mwelekeo, wapi tunataka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo; lazima niweke kumbukumbu sawasawa, lazima tukumbuke kwamba, mimi sio mtu wa kuweza kunukuu vifungu vya Biblia au *Quran* lakini zipo sehemu ambazo watu wanasema, kwamba mdomo unaumba, lakini sio hivyo tu, kuna kauli nyingine unaambiwa kwamba sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ni zao la dua za Watanzania. Sikuwepo kwenye Bunge lililopita lakini nilikuwa nasikiliza ni namna gani Wabunge walivyokuwa wanaomba kwamba tunataka Rais mwenye msimamo, tunataka Rais anayekwenda kusimamia rasilimali za Taifa hili. Kwa sababu Mwenyezi Mungu anasikia, kilio cha wengi ni kilio cha Mungu, ndiyo akatupatia zawadi tukapata Rais ambaye sasa ni kweli anakwenda kuyatekeleza hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ndugu zangu wanaobeza ni kwa sababu ya ubinadamu, kwamba binadamu ameumbwa ni mtu mwenye kusahau. Wameshasahau kwamba wao ndio waliopendelea wakamwomba Mwenyezi Mungu tupate Rais wa namna hiyo, kwa hiyo nilikuwa naweka kumbukumbu sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wabunge tukumbuke moja ya majukumu yetu ni kutunga sheria. Sasa naomba nitoe ushauri kwa Wabunge; tunapokwenda kutunga sheria lazima tuwe makini kuhakikisha sheria hizi zinakwenda kufanya kazi ile ambayo tumeikusudia, lakini tunapokwenda kufanya kazi hii kwa kulipua matokeo yake tunakuwa wa kwanza kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kusikia hapa kuna mchangiaji mmoja alikuwa analalamikia Sheria ya Korosho, kwamba kuna Mkuu wa Wilaya amewakamata watu wanatoa korosho kutoka Msumbiji kuleta Tanzania, lakini wanasahau kwamba kosa lile sisi ndio tumelifanya kwa sababu kwenye Sheria yetu ya korosho ukiangalia tunakataza korosho kutoka nje kuingia Tanzania na sio korosho tu, kuna mazao mbalimbali tumekataza kwenye sheria zetu, kwamba hakuna mtu anayeruhusiwa kutoa mazao nje ya nchi yetu kuyaleta Tanzania. Sasa hawa watekelezaji wanakwenda kutekeleza hizi sharia, bado kwenye Bunge hilihili sisi tunaona kwamba wale wanafanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena kuna Mbunge mmoja alikuja akasema kwamba hii ni *shame*, ni jambo la aibu, kwamba eti kwa nini Msumbiji wanataka kuleta korosho, kuinua uchumi wetu, tuongeze pato letu tunawakataza, lakini anasahau kazi hiyo ameifanya yeye hapa Bungeni na ndiye aliyelipitisha jambo hili. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tunapoifanya kazi hii tuifanye kwa umakini, tujue kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi na makosa haya mara nyingi yanafanywa na sisi wenyewe. Kwa hiyo hilo ndilo jambo ambalo nimeona kwamba niweze kulisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nirejee kwenye utunzi wa sheria. Naomba kuanza na sheria ndogo, Mheshimiwa Mwenyekiti ametoa mapendekezo hapa na ametaja kasoro mbalimbali zinazotokana na utunzi wa sheria ndogo. Kuhusu jambo hili naomba niishauri Serikali, hapa tunasema hizi sheria ndogo, lakini sheria hizi ndizo ambazo ziko karibu na wananchi wetu, ndiko ambako wanakwenda kuzi-*practice* hizi sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba kwa Serikali ni lazima tuhakikishe kwamba, hawa Wanasheria tunaowapeleka kwenye halmashauri zetu ni Wanasheria waliobobea katika fani hii ya sheria. Vinginevyo tunapoacha kupeleka Wanasheria waliobobea kwenye halmashauri zetu tunakwenda kuziangusha halmashauri zetu na ndiyo maana tunapata hizi kasoro ambazo zinaletwa kwenye marekebisho ya sheria ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, kuna matatizo mengi sana kwenye halmashauri, kuna kesi nyingi sana kwenye halmashauri ambazo halmashauri zinashindwa kwa sababu tu hatuna Wanasheria wenye weledi, hatuna Wanasheria waliobobea na matokeo yake tunashindwa kwenye kesi mbalimbali matokeo yake halmashauri zetu zinaingia kwenye madeni mbalimbali, kulipa fidia na kulipa faini mbalimbali. Hii yote ni kutokana na uchache au weledi wa Wanasheria wetu. Kwa hiyo hapa mimi naishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki cha sheria kwenye halmashauri zetu

ili tuepukane na hizi adha ambazo tunaweza kuzipata kwenye halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nichangie kuhusiana na uhaba wa upatikanaji wa huduma ya sheria hasa kwenye ujenzi wa Mahakama. Halmashauri zetu nyingi hazina Mahakama; kwa mfano Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale ni halmashauri ambayo iko tangu mwaka 1975, lakini leo naongea 2019 hatuna jengo la Mahakama ya Wilaya. Si hivyo tu, Wilaya ya Liwale kwa mfano ina tarafa zaidi ya tatu na kata zaidi ya 20, lakini mpaka leo naongea kwenye Bunge hili tuna Mahakama moja tu ya mwanzo; hatuna Mahakama nyingine ya Mwanzo; na hiyo Mahakama yenyewe ya mwanzo ni Mahakama ambayo ilijengwa na wananchi; lakini mpaka leo liko tu jengo la tope na Mhudumu yuko mmoja tu, Hakimu ambaye ndiye Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa naweza kuishauri Serikali, kwamba ili tuweze kwenda na wakati na mnajua dunia sasa hivi dunia hii ni kama kijiji; kwa hiyo uhitaji wa Mahakama ni mkubwa sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali ipanue hii huduma ya Mahakama ili tuweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. Hili jambo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye Mahakama za Mwanzo; Mahakama nyingi za Mwanzo zina uhaba mkubwa sana wa wafanyakazi, hasa Mahakimu. Si hivyo tu, kwa sababu ya uchache tulionao kwenye Mahakama imepelekea sasa kuwe na vitendo vingi vya rushwa, ili mtu kesi yake labda iishe mapema, inabidi atoe rushwa. Si hivyo tu, ule upeke kwanza *exceptionalist* wa mtoa huduma ambaye yuko pale na kesi zile zilikuwa ni nyingi. Kwa hiyo inakuwa ni miongoni mwa vivutio vya kuweza kuendeleza hii rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naiomba Serikali, kuna sera inahusu wazee. Ukiingia kwenye huduma mbalimbali unakuta kuna mahali pameandikwa wazee kwanza, mpishe mzee, fanya hivi, lakini ukiangalia kwenye

Bunge hili hatujawahi kutunga sheria inayohusu wazee. Hawa wazee ambao wanambiwa wapishwe labda wawahi wazee ni wazee wa aina ipi? Sheria haijawatambua wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba itulee sheria ya wazee ili hawa wazee ambao tunawaongelea siku zote tuweze kuwatambua, na tukiweza kuwatambua ndipo tutaweza kuwatendea haki. Vilevile tukumbuke sisi wote humu ndani ni wazee watarajiwa. Kwa hiyo naomba niishauri Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, ilete hii Sheria ya Wazee ili hawa wazee waweze kutambuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niishauri Wizara ya Sheria na Katiba. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la ucheleweshwaji wa kesi Mahakamani. Jambo hili linakuwa linaongeza sana mlundikano wa mahabusu kwenye magereza zetu. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iongeze bidii ili wananchi hawa watendewe haki yao; kwa sababu haki iliyocheleweshwa ni sawa kabisa na mtu aliyekosa haki hiyo. Kwa hiyo naiomba Serikali iongeze watumishi kwenye Idara za Mahakama na vilevile kuongeza ofisi kwenye idara hizi za mahakama ili kesi mbalimbali ziweze kwenda kwa wakati na ziweze kwisha kwa wakati ili kupunguza mlundikano kwenye magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye huo huo utunzi wa sheria; mara nyingi nimeona Serikali ikileta sheria hapa ili zifanyiwe marekebisho; zile ambazo zimepitwa na wakati. Kwa mfano unakuta sheria inataja labla mtu akifanya *offence* fulani atapata adhabu ya kulipa 2,000 au 5,000. Hizi ni sheria ambapo zimepitwa na wakati. Kwa hiyo Serikali wamekuwa wakizileta hizi sheria hapa kuzifanyia *amendment* ili kuongeza hivi viwango kulingana na wakati tulionao. Hata hivyo bado tunasahau kuzifanyia marekebisho zile sheria ambazo zitawasaidia wananchi wetu. Mathalani kuna sheria inasema kwamba mwananchi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kengele ya pili, Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nafurahi kwamba leo Bunge lina utulivu wa kutosha na taarifa na miongozo pengine jana mlijadili mkasema haina maana sana. Jana nilikuwa natafakari sana, kwamba ndani ya Bunge hili Wabunge wote tuliopo sasa tukapewa fursa na Mwenyezi Mungu ya kuishi miaka 30 inayokuja mimi nitakuwa na miaka 72, wewe utakuwa na takribani miaka 100, pengine Mheshimiwa Jenista atakuwa na miaka mingi zaidi. Maana yake ni kwamba hata kama tutakuwa hai wengine watakuwa hawana nguvu kabisa za kulitumikia Taifa hili. Thamani yetu leo si kulinda Chama Tawala ni kulinda misingi ya haki katika Taifa na ndio wajibu wa kwanza wa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiishi kula leo, kuvaa leo, kuendesha gari leo, halafu usitafakari maisha ya wajukuu wako, ya vitukuu vyako baada ya maisha yako hapa duniani, si tu utakuwa ni Mbunge mkatili, utakuwa ni mzazi mkatili. Kama kuna kitu tunapaswa kukichunga Wabunge wote bila kuangalia itikadi yetu ni juu ya namna gani tunalisaidia Taifa kuheshimu Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huu ndio msingi tuliokubaliana kwamba kwa sasa tutaishi kwa madhumuni haya na kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote duniani, iwe ni Marekani, iwe ni Venezuela, iwe ni Kenya, ikianza kuishi nje ya utaratibu wa Katiba na sharia, Serikali hiyo inakuwa ni kikundi cha wahuni ila wamevaa suti, yoyote duniani. Namna pekee ya kuthibitisha umahiri wa Maprofesa, Madaktari, *form four* na watu wote wenye hekima, namna pekee ya kuthibitisha umahiri ni kuishinda hofu linapokuja suala muhimu la haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wangu mimi na mjukuu wangu mimi natarajia siku moja akutane na

Mahakama huru hata kama nitakuwa sipo, *same to mtoto* wa Mheshimiwa Jenista, *same to mtoto wako*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapona haki inachezewa, lakini inachezewa kwa kwa sababu inatupa *fever* ni sawa sawa na *chloroquine* imepakwa *chocolate*, utaila kwa muda utasikia radha ya *chocolate* baadaye utakutana na uchungu. Hakuna uovu ambao hautalipwa ni *nature*, ni *karma*. Kuna mambo leo yanawatokea watu wa CCM ambao huko nyuma walikuwa *untouchable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikutana na Manji siku moja Karimjee, nikamwambia kwamba kuna kipindi wewe ulikuwa *untouchable*. Leo kuna watu walikuwa hawaguswi katika katika Serikali hii, walikuwa ni wafanyabiashara wakubwa, walikuwa ni viongozi wakubwa, leo wako magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utawala unaoweza uka-*guarantee* usalama wa mtu isipokuwa haki, kwa sababu haki haina tu kipaumbele cha *system* ina kipaumbele cha Mwenyezi Mungu peke yake. Waheshimiwa Wabunge tunapokaa hapa Bungeni kujadili mambo ya msingi; jana nimeshangaa; kwamba suala la mkono wa sweta (govi) linaweza likatolewa na Bunge na TV ya Bunge likapelekwa mitaani halafu masuala mengine ya msingi ya kusaidia nchi kama vile michango ya Wabunge wa Upinzani inanyimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yetu siyo uhaini...

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawasaidia, leo tunaongea michango yetu si uhaini, michango yetu...

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa muongeeji, naheshimu mawazo yake lakini mkono sweta unachangia kwa asimilia 60 ya maambukizi ya UKIMWI, ukilinganisha na mtu aseyekuwa na mkono sweta. Kansa ya akina mama *carries* ni wanaume na mkono sweta unaongeza mara nyingi zaidi ukilinganisha mtu na mtu asiye na mkono sweta; na afya na uhai ndiyo haki ya kwanza kabisa ya Mtanzania kabla ya yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa hiyo.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, taarifa hiyo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea hiyo taarifa. Hiyo ni sehemu ya mfano wa jambo hilo, lakini yako mambo mengi, kwamba leo mawazo yetu ndani ya Bunge si mawazo ya kuiangusha CCM. Mimi leo mkitawala kwa haki, kwa upendo, kwa sheria na mkafuata Katiba, hata mkitawala milele sitakuwa na tatizo. Lengo letu si kuwatoa ninyi madarakani, lengo letu ni kuona ninyi mnatutawala kwa haki na ndiyo maana ya upinzani.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo chuki inajengwa, leo kiongozi mmoja m-*NEC* wa Chama cha Mapinduzi anahutubia anasema Mheshimiwa Lissu siku akitua ashambuliwe, Mheshimiwa Zitto ashambuliwe, leo Mheshimiwa Zitto yuko Bungeni, tumemwondoa juzi, Mheshimiwa Zitto juzi alikuwa anafuatiliwa usiku kwa kazi za Kibunge si za kuuliza madawa la kulevya, si za kubaka mtoto, kwa kazi za Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitekwa Makuyuni kwa kazi ya Kibunge, wakaua mtu mmoja polisi, kwamba wale ni watu waliokuwa wanakuja kuniteka mimi. Nikapelekwa jela kwenye ile kesi yangu dhidi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Nikiwa jela wale vijana

wakaletwa jela, wakapelekwa *dispensary* nikajifanya naumwa nikapelekwa *dispensary* nikaanza kuongea nao. Cha ajabu wale vijana waliokuwa jela walitolewa jela siku ya Jumapili na Mbunge, Mheshimiwa Jitu alikuja kuwachukua na gari siku ya Jumapili ambapo Mahakama wala Magereza haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo yanafanya tulipwe machozi, tunaguna, siyo mimi peke yangu ninayeguna, tumesikia juzi hapa Itigi, Mkurugenzi ameuu, ameingia ndani ya Kanisa la Sabato, ame-*shoot*, mzazi anasema ame-*shoot*, Mkurugenzi akasema ilikuwa ni kwa bahati mbaya. Tunaona taarifa ya polisi leo inasema Mkurugenzi yule hakuu, walioua ni Polisi wa Wanyamapori waliokuwa nje.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa kanuni yan 64 (1)(c); jambo ambalo analizungumzia Mheshimiwa Mbunge Godbless Lema wa Arusha Mjini ni jambo ambalo limetokea, vyombo vya ulinzi na usalama vinalifanyia kazi. Tuiachie Mahakama itakapofikia hatua ya kuamua tutajua nani amehusika; kwa sasa jambo hili linafanyiwa uchunguzi, si jambo jema, Bunge kuanza kulijadili na kuingilia shughuli za mhilimi mwingine. Kwa hiyo hoja yangu ni kwamba kulijadili jambo hili ni kinyume na taratibu za kanuni, aliache lifanyiwe kazi na maamuzi yatatolewa, tutajua nani na nani wamehusika katika jambo hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema ambalo haliko Mahakamani usilizungumzie...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema nisikilize mimi, kama jambo liko Mahakamani...

MHE. JOHN J. MNYIKA: (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti, hakisikika*)

MWENYEKITI: Nazungumza na Mheshimiwa Lema sizungumzi na wewe Mheshimiwa Mnyika, wala sizungumzi na Mheshimiwa Bobali, wala sizungumzi na nani, nazungumza na Mheshimiwa ambaye ndiye mwenye hoja na hizi ni kanuni zetu, lolote ambalo liko Mahakamani huwa hatulizungumzi humu ndani. Sasa na mimi nafuatilia, Mheshimiwa Lema endelea.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno tunaongea hapa kwanza hili suala haliko Mahakamani; lakini siku Bunge hili likafikiri hata jambo lililoko Mahakamani lakini lina mashaka ya damu ya mtu, Bunge hili haliwezi kulijadili tunainajisi *legitimacy* yetu kama Wabunge. Waheshimiwa Wabunge thamani ya mtu mmoja ni zaidi ya kilometa 10, 000 za lami, thamani ya mtu mmoja, hata kama ni kichaa, ni zaidi ya *SGR* ya kutoka Tanzania kupita nchi zote za *SADC*. Kazi ya kwanza ya serikali yoyote duniani ni ku-*protect human rights*. Kama huu si msingi wetu wa imani, kwamba maisha ya mtu mmoja yanaweza yakawa *considered* na vitu, thamani yetu ya kuishi haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanaendelea kufa, watu wanaendelea kupotea na yote hii ni Katiba. Inawezekana kabisa kuna nia njema ya Serikali, kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ni kumwambia ukweli kwa sababu ukweli ni nguvu. Leo tunavyoongeza kuna watu wanaoza mahabusu. Jamani mimi nikiongea habari ya mahabusu; pasu nimekutaka na Mheshimiwa Profesa Kabudi nimeongea naye; kuna watu wana kesi za *money laundering* wako mahabusu, Sh.300,000 mtu yuko jela miaka mitano. Kenya leo kila kesi ina dhamana isipokuwa kesi ya uhaini, Uganda leo kila kesi ina dhamana mpaka

kesi ya uhaini. Dhamana ni hoja kuu imewekwa kwenye Katiba hii ndiyo Mtobesya. (*Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kaka yangu, shemeji yangu, Mheshimiwa Lema kuwa hatumwelewi anachoongea. Hapo anasema nchi ifuate sheria na Katiba; Katiba yetu imeweka vyombo vitatu, Mahakama, Serikali na Bunge, hapo hapo anapiga makelele kuwa kuna watu wanaozoea jela wakati yale ni maamuzi ya Mahakama na Mahakama ni chombo kingine. Kwa hiyo awe *specific*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lema taarifa hiyo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lenye Wabunge zaidi ya watu 350, hutarajii kumkosa mtu kama huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, mimi napita Magereza zote, kuna kesi inayotumika vibaya, Profesa yuko hapa, ni Mwanasheria. *Money Laundering Act*; Waheshimiwa sikilizeni tuna miaka miwili kutoka humu ndani, haya mambo ninayowaambia sisemi kwa niaba ya CHADEMA nasema kwa niaba ya watu wote sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walioko Magereza leo wengi hawakuwa makada wa Chama cha CHADEMA. *Concern* yangu hapa nini, leo Mahakama ya Kikatiba ilinusa *section 148* ya *CPA* ambacho kilikuwa kinampa mamlaka *DPP* ya kuweka watu ndani kwa *certificates*. Mimi nimekaa ndani kwa *certificate*, watu wengi wakaa ndani. Sasa haya mambo leo yanaonekana ni CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kundi hili linaweza likaamua leo, tunaamua tu leo kwamba hatugombanii ubunge, tu naacha siasa halafu ninyi CCM mjae huko, *then what?* Halafu nini kifanyike? Yaani *assume* huku mmejaa, huko mmejaa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wenu, Mheshimiwa Rais wenu halafu *then what, then what?* Kimsingi ni sheria, kimsingi ni utaratibu. Ndiyo maana tunasema Waheshimiwa Wabunge turudi turudi kwenye *sense*. Nawaambia, kwa hali ilivyo leo na nisikilizeni mimi ninyi, Mawaziri mlioko kwenye Baraza hili na Makatibu Wakuu, kwa utaratibu wa sasa ninavyouona jandaeni, la sivyoo badilisheni sheria; jandaeni ninyi na hamtajua. Kwani, Waheshimiwa viongozi, kwani Magufuli ni CHADEMA, Magufuli si CHADEMA, ni *purely* CCM. Wakati Magufuli anashinda Urais.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Rais utamu-*address* kwa cheo chake tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani na namheshimu sana. Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Mtukufu Magufuli, siyo CHADEMA ni CCM na watu wote leo wamekuwa *responsible* na matatizo waliyofanya kwenye kazi zilizopita siyo CHADEMA, wengi ni Makada wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi, mtafanya mitimanyongo yote mnayoweza kufanya, mtafanya kila mnachoweza kufanya; tunaweza tusirudi Bungeni tena; mtasema tutamweka mtu wetu Profesa Kabudi huyu, atalinda utawala uliopita. Akina Kikwete walifikiri hivyo hivyo, utawala uliopita haulindwi. Walifikiri hivyo hivyo. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, bado dakika tano. Zangu ni 15.

MWENYEKITI: Ahsante. Tayari Mheshimiwa Lema. Ulianza na dakika sita. Sasa namwita Mheshimiwa Timotheo Mnzava, ajiandae Mheshimiwa Mollel.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nitumie nafasi hii kukupongeza wewe na viongozi wengine wote wa Bunge kwa namna mnavyotuongoza. Pia nitumie nafasi hii kuzipongeza sana Kamati zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa hizi za Kamati kwenye uchambuzi wao, ukasoma maoni na mapendekezo ya Kamati zote, unaona kabisa kwamba Wajumbe wa Kamati hizi wamelitendea haki Bunge lako Tukufu. Nimezisoma, kazi yao ni nzuri na ni wajibu wangu kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, lakini pia na ile ya Sheria Ndogo. Tunapokuja kwenye uwanja kama huu wa Sheria, kwa sisi tunaopenda nchi yetu pia lazima tutumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusaidia utekelezaji na usimamizi mzuri wa sheria ndani ya nchi yetu. *Speed*, kasi na moyo wa Mheshimiwa Rais kuendelea kuteua Majaji kwa wingi kama anavyofanya sasa hivi ni ishara kwamba Mheshimiwa Rais anataka kuusaidia Mhimili wa Mahakama ufanye kazi zake vizuri na utoe haki kwa wakati jambo ambalo ni wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ni vyema nichangie mambo machache. Kwa muda mrefu tumekuwa tukisikia na ndiyo msingi wa kuwa na Katiba na kuwa na Sheria, kwamba nchi yetu ni lazima iongozwe na iendeshwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Hata mchangiaji aliyetoka, kaka yangu Mheshimiwa Lema amesisitiza jambo hilo na ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kelele nyingi kwenye uhuru wa watu kutoa maoni, uhuru wa watu kushirikiana; na mambo mengine ya namna hiyo. Wote wanaozungumza, wanasema uhuru huu upo kwa mujibu wa Katiba, kwa hiyo, wanataka uhuru huu uheshimiwe. Hilo ni jambo zuri, nami naliunga mkono kabisa; na ndiyo mtazamo wangu, ndiyo msimamo wangu na ndiyo mawazo yangu kwamba kama Taifa, lazima tuheshimu uhuru na haki zilizotolewa kwenye Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukumbushane kwamba hata huu uhuru tunaotaka tuheshimu, tunaotaka ufuatiliwe, tunaotaka utekelezwe; haki za binadamu tunazotaka watu wapate; hakuna haki bila wajibu. Katiba hii hii ambayo inapigiwa kelele kwamba imetoa haki za binadamu, imetoa uhuru kwa watu kufanya mambo, imetoa na namna ya kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma vizuri Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kwamba ziko haki, uko wajibu, lakini ukienda kwenye Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa masharti, haiachi tu uhuru ukaenda unavyotaka, kila mtu afanye anavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba inatuambia kabisa, lazima kila mmoja kwenye kutekeleza na kutumia uhuru wake, ahakikishe haingilii uhuru wa mtu mwingine, ahakikishe hautumii katika namna ambayo inakwaza na kuumiza watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale ambao tunapigania haki, tuko sahihi kabisa, lakini lazima tukumbushane kwamba uhuru huu una mipaka. Ibara ya 30(2) inaipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria kutekeleza huo uhuru na hizo haki ambazo tunazo kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona kwa kuwa tunajadili taarifa za Kamati hizi ni vyema tukakumbushana jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo, kwenye ukurasa wa 36 kama sikosei, Kamati ya Sheria Ndogo imetoa maoni na mapendekezo mazuri sana kuhusu Sheria Ndogo ambazo zinatungwa kwenye nchi yetu; ukurasa wa 36 ile (a), (b), (c), (d) na (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Kamati kwa sababu ushauri waliutoa ni ushauri wa msingi, nami ninauunga mkono na ninaomba ukafanyiwe kazi. Nasema naipongeza Kamati hii kwa sababu gani? Ushauri waliutoa wenzetu kwenye Kamati, umetuonesha pia tofauti ya ile dhana waliyokuwa nayo watu wengine kwenye mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mawazo, dhana na maneno; wako watu ambao wanapinga, wanasema siyo sahihi kuendelea kuiachia Serikali, Taasisi mbalimbali za Serikali kutunga Kanuni. Wako wengine wanasema Kanuni mbalimbali zitungwe ziwekwe ndani ya sheria au zije zijadiliwe Bungeni. Ni dhana zinazungumzwa, lakini ukisoma ushauri huu wa Kamati, unaelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu imelipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria, ukisoma Ibara ya 64. Ukienda Ibara ya 97(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatoa mwanya, baada ya kutunga Sheria inaruhusu kutungwa kwa kutungwa kwa Kanuni na sheria nyingine ndogo ndogo zikiwemo Kanuni, zikiwemo *Orders* na vitu vingine vya namna hiyo. Kwa hiyo, kwanza, Kanuni kutungwa kwenye Wizara, kutungwa kwenye Taasisi mbalimbali za Umma, kutungwa kwenye vyombo mbalimbali, haikiuki Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hatuwezi kuacha Bunge likawa linatunga sheria zote, kanuni zote na *orders* zote. Tutakuwa nchi ya namna gani? Kazi zitafanyika namna gani? Bunge hili tunakutana kwa mwaka mara ngapi? Tunafanya kazi mara ngapi kwenye Bunge hili? Huwezi ukaacha kila sheria ikatungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mambo yaende vizuri, tutatunga Sheria ya Bunge, lakini sheria hiyo lazima itoe mwanya kwa Taasisi nyingine au Wizara au Idara kutunga kanuni ili mambo yaweze kwenda vizuri. Hata inapotokea kuna jambo la kurekebisha, pia ni rahisi kurekebisha kanuni kuliko utaratibu wa kurekebisha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya siyo maneno yangu tu peke yangu. Mwanasheria mmoja mbobezi anaitwa John Alder, ameandika Kitabu kinaitwa *“Constitutional and Administrative Law”, edition* ile ya saba. Kwenye kitabu chake ukurasa wa 147 anajaribu kueleza huo mkanganyiko na hayo mawazo ya watu, lakini mwisho ana-conclude akasema *“however, it is difficult to imagine a complex and highly regulated society that could function effectively if all laws had to be made by the Parliament itself.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema niliseme hili, kwa sababu maoni ya Kamati yamejielekeza vizuri, lakini najua yako mawazo ya watu ya namna hiyo. Mimi nadhani utaratibu uliopo ni mzuri, tuache utaratibu huu uendelee. Sheria zitungwe na kama inavyotukumbusha ile Sheria yetu ya *Interpretation of Laws*, ukisoma kuanzia *section* ya 36 inatoa utaratibu, hizi kanuni zitungweje? Ziweje? Zifuatane na kitu gani? Zizingatie vitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu uliopo uendele, lakini ushauri wa Kamati uzingatiwe ili kuweza kuboresha utaratibu huu wa kutengeneza Kanuni na Sheria nyingine ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lilitoka kuzungumzwa hapa muda siyo mrefu sana. Tunapokumbushana kuendesha nchi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu, lazima tukumbushane kama nilivyosema, haki na wajibu wa kila mmoja wetu. Sheria zetu na taratibu zetu haziruhusu mambo yaliyoko Mahakamani kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona imekuwa ni utaratibu wa kawaida na kwa masikitiko makubwa,

nimewahi kuona hata kwenye Bunge lako hili, mtu ana kesi Mahakamani, amepewa dhamana, amekiuka masharti ya dhamana, akafutiwa dhamana, ana kesi Mahakamani, ana-*challenge* uamuzi wa Mahakama kumfutia dhamana, mtu anakuja na jambo hili kulileta Bungeni. Tunakuja kufanya nini kwenye Bunge hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uko wazi. Mtu anasema kuna kesi ya Mashehe; ndiyo ipo kesi ya Mashehe lakini iko Mahakamani. Unataka tuilete Bungeni humu kufanya nini? Ni lazima sisi kama Wabunge tuwe watu wa kwanza kuheshimu sheria.

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tuwe watu wa kwanza kuheshimu misingi na taratibu na Katiba ya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnzava, ahsante.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja za Kamati. Ahsante.

MWENYEKITI: Mchangiaji wetu sasa hivi ni Mheshimiwa Dkt. Kolimba, jiandae Mheshimiwa Zainab Katimba.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Ulinitaja mimi.

MBUNGE FULANI: Hajaomba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kolimba.

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupewa nafasi ya

kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Moja kwa moja kama wenzagu waliotangulia, naomba niunge mkono taarifa zote mbili zilizotolewa mbele yetu na maoni na maazimio ya Kamati hizo zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoongea Mheshimiwa Timotheo, Mbunge, jirani yangu, narudi pale pale kwenye suala la uhuru. Tunapozungumzia suala la haki ya uhuru kwa raia yeyote wa Tanzania, tunazungumzia suala ambalo liko ndani ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo alipozungumzia kuhusu suala la haki na uhuru, pia alitukumbusha kwamba tunapodai uhuru lazima pia tujue kwamba tunatakiwa kuwa na wajibu. Ukimsikiliza mzungumzaji, Mheshimiwa Mbunge Lema, alipokuwa anazungumza alitukumbusha sisi wote kama Wabunge wa Upinzani na wa Chama Tawala kwamba tunapozungumza kwamba watu wengine wako Magarezani, maana yake ni kwamba tukumbuke kwamba nasi pia tutakwenda Magarezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hoja yake na dhana yake naitafsiri kwamba Mheshimiwa Lema anakubali kabisa utendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu inasimama kwenye haki na wajibu. Pale ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaposimamia suala la uhuru, haki na wajibu, maana yake ni kwamba pale inapona mwananchi au raia yeyote wa Tanzania anavunja sheria, ni lazima hatua za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba nakubaliana na Mheshimiwa Lema anapositiza kwamba sisi wote tuwajibike, tusimamie sheria, tuzifuate na tuzitekeleze. Sheria hizi ni msumeno, inaweza ikakata upande wowote na hatuwezi kusema kwamba pale wanapowekwa Magarezani labda wanachama wanaotokana na Chama cha Mapinduzi maana yake ni sahihi; lakini wanapoguswa

wanachama wanaotokana na vyama vingine maana yake sheria inavunjwa au Katiba inavunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba nizungumzie kuhusu utendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake. Tumeona katika Kamati, Wizara hii imejipanga vizuri na hasa kwa kuanzisha vile vyombo vipya ambavyo vimewekewa utaratibu. Kitu ambacho nimekipenda zaidi ni pale ambapo Taasisi mpya ambazo zimeanzishwa ndani ya Wizara hii ya Katiba na Sheria zinapoweka utaratibu wa mpango kazi wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kitendo cha Wizara ya Katiba na Sheria cha kuanzisha zile Mahakama za kielektroniki, nafikiri ni wazo zuri kwa sababu litakuwa linasaidia kupunguza msongamano wa uendeshaji wa mashtaka madogo madogo yaliyopo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndani ya Kamati, tumepata taarifa ya jinsi Wizara ya Katiba na Sheria ilivyojipanga vizuri katika kujenga *capacity* ya watumishi watakoajiriwa katika Taasisi hizi mpya na kule katika Wizara zao. Ninachoshauri, Wizara iweze kutumia nafasi waliyonayo ya kuhakikisha kwamba katika kila mwaka waweke mpangokazi wa kuhakikisha kwamba wanajenga uzoefu na ujuzi kwa wafanyakazi na watumishi watakoajiriwa na wale ambao wanafanya kazi katika Ofisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Wizara pia iweze kutumia vizuri zile *scholarships* ambazo zinatolewa na Mataifa mbalimbali rafiki ili kuwajengea uwezo na hasa *practice* katika Taasisi hizi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono ushauri uliotolewa pia na Kamati Ndogo ya Sheria Ndogo ya Bunge ambayo pia imejaribu kuangalia upungufu unatotokana na sheria ndogo ndogo zinazotungwa katika Taasisi, kwenye Wilaya au Ofisi za Kiserikali. Katika upungufu huo,

tunaungana nao kwamba utaratibu uwekwe vizuri, pale ambapo Taasisi au Ofisi zinapotunga hizi Kanuni, zihakikisha kwamba zinatengeneza mpangokazi wa kuhakikisha kwamba kabla hazijatolewa kwa matumizi, zinapitiwa vizuri na kuhakikisha kwamba hazikiuki masharti yaliyowekwa kwenye sheria na Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe kutoka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ya Bunge, nitaendelea kuishauri Serikali na kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao bila kuvunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kutoa mawazo kwamba pale ambapo sheria au sheria ndogo zinapotungwa, waweze kuwajulisha watumiaji, wadau wanaotumia hizo sheria ndogo ili waweze kuzitumia sheria hizi bila kuzivunja na kupata mataizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa taarifa hizi zote mbili. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Katimba, ajiandae Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Katimba, siyo wewe uliyekaa karibu na Mheshimiwa Shangazi? Hujaomba? Maana jina lako lipo hapa. Kama huchangii niambie tu huchangii, nitakutoa.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaomba kuchangia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel. Jiandae Mheshimiwa Oscar Mukasa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Kamati zote hizi mbili. Awali ya yote, naunga mkono Kamati zote mbili. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia na hatimaye kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabisa, naishukuru Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kweli niwapongeze sana kwa jitihada kubwa wanazofanya katika kuhakikisha makundi maalum na hasa kundi la watu wenye ulemavu ambalo leo hii nitapenda zaidi nilizungumzie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nisiisahau pia Wizara ya Katiba na Sheria, nawapongeza sana kwa jinsi ambavyo wamekuwa nao katika suala la Sseria kuzingatia masuala ya watu wenye ulemavu. Vilevile kwa kuwa katika ukurasa wa 25 wamezungumzia makundi maalum, wakiwemo pia watoto, nichukue nafasi hii pia kukemea mauaji yanayoendelea huko Mkoani Njombe hasa ya watoto na Mwenyezi Mungu pia awajalie familia ambazo zimepoteza watoto. Pia wale watoto waliotangulia mbele ya haki, basi Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa kuzungumzia suala zima la michezo kwa ajili ya watu wenye ulemavu; na nitapenda pia kunukuu Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Ibara ya 30 unaelekeza nchi wanachama kushirikisha watu wenye ulemavu kwenye michezo. Vilevile Sheria yetu ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 Sheria Na. 9 inatoa haki ya watu wenye ulemavu kushiriki kwenye michezo kupitia Kifungu cha 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Kimataifa inazungumzia *inclusive policy* ambayo Tanzania pia imekubali na imeridhia. Ni kweli nchini kwetu tumekuwa tukizungumzia masuala mbalimbali, hasa katika michezo, tunazungumzia kwa ujumla na hasa mpira na michezo mingine ambayo inawahusisha wenzetu ambao kwa namna moja au nyingine wako kamili kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu wenye ulemavu, kwa kweli Serikali bado imekuwa nyuma pamoja na kwamba tumeridhia hii sheria, bado michezo kwa watu wenye ulemavu haijapewa kipaumbele na wala haijatiwiwa

mkazo. Nasema hivyo, kwa sababu hakuna fungu lolote, hakuna mahali ambapo Serikali imejitoa katika kusaidia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; walikuja wenzetu ambao ni kutoka katika Chama cha Watu Wenye Ulemavu ambao wanahusika na michezo. Kwa bahati nzuri sana mwaka huu kuna mashindano yatafanyika hapa nchini kwetu mwezi wa Sita yatahusisha watu wenye ulemavu kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati. Jumla ya nchi 12 zitashiriki, lakini mpaka sasa bado wanahangaika hawajui wapi ambako kwa kweli wanaweza wakasaidiwa. Ni heshima kubwa kwa michezo hii kufanyika hapa nchini mwetu, lakini ningeiomba Serikali katika majibu yao watakapokuja kutueleza, watueleze kwamba katika hili wamejiandaje basi ili kufanikisha michezo hii, lakini kama tunavyofahamu michezo ni ajira, michezo ni afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia michezo hii inatukutanisha kwa pamoja walemavu kutoka sehemu mbalimbali. Kwa hiyo katika ile michezo inakuwa ni faraja kwetu pia, kwa hiyo niombe tu kwamba Serikali ione kwamba inatekeleza sera hizi katika kusaidia hawa watu wenye ulemavu kwenye michezo kwa sababu pia itawasaidia kuongeza kipato cha kwao wao binafsi pia na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili naomba sana Serikali waweze kuliona kwa sababu katika Kamati yetu ni kweli tunasimamia Ofisi ya Waziri Mkuu na kipekee mimi nawapongeza kwa sababu kuna jitihada kubwa sana ambazo zimefanyika na niseme tu kwa kweli kwa Mheshimiwa Rais wetu nampongeza sana kwa moyo wangu wa dhati kabisa, kwa jinsi ambavyo ameyapa kipaumbele masuala watu wenye ulemavu. Hilo kwa kweli tunajivunia na hata kwa Afrika Mashariki kitendo cha kuwa na Naibu Waziri katika Baraza la Mawaziri, hii ni faraja kubwa sana na ni mfano ambao hata wengine wenye ulemavu wakiona kwamba kwenye Baraza kuna mtu ambaye amefikia hatua hiyo, wanapata ile ari ya kusoma na kuweza kuwa na ndoto kwamba na wao siku moja watakuja kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, nampongeza sana kwa hili kwa kutambua na kuwapa umuhimu na niseme tu kwamba sasa hivi watu wenye ulemavu tumekuwa na heshima kubwa hata wazazi wale ambao walikuwa wanaona kwamba kuwa na mtoto mwenye ulemavu ni tatizo, sasa hivi wanaona kwamba kumbe akipata elimu na kwa kuzingatia kwamba sasa hivi elimu ni bure, kwa kweli hizi pongezi namwombea sana Mheshimiwa Rais wetu, Mwenyezi Mungu aweze kumpa maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kuzungumzia mwishoni mwa mwaka jana nilipata bahati ya kuhudhuria kama mdau katika Ofisi ya Waziri Mkuu, walikuwa wanaandaa mwongozo ambao utawezesha kuwa na Mfuko Maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu na hili nimelizungumzia sana katika Bunge hili, ni matarajio yangu kwamba Mheshimiwa dada yangu mpendwa Jenista kwamba kwa mwaka huu ni matarajio yangu kwamba kwa sababu katika Bunge na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu tuna fungu kwa ajili ya Bunge, tuna fungu kwa ajili ya vijana, tuna fungu kwa ajili ya masuala mengine, lakini hakuna fungu maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu kwa kweli nitakuwa mpinzani wa Mheshimiwa Waziri endapo hatokuja na fungu maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Matokeo yake kwamba sasa tumekuwa tukidandia tu katika haya mafungu mengine, vijana wanalo fungu lao na katika fungu hili mpaka katika mikoa yote wana ofisi zao. Sasa kama masuala haya tumeshayachukua na tumeshayapa kipaumbele ni muhimu sasa na hili pia wakati mwingine hata Naibu Waziri aweze kufanya kazi zake vizuri inakuwa ni busara zaidi akiwa na fungu lake, anajua kabisa kwamba hapa Mheshimiwa Waziri nitamshauri tufanye hivi, nitamshauri tuendeleze hivi, lakini pasipokuwa na fungu wakati mwingine unaweza ukaambiwa kwamba hakuna fedha kwa ajili ya masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dada yangu mpendwa namjua uwezo alionao, Mheshimiwa Jenista Mhagama namfahamu yeye ni mwanamke shupavu, ni mwanamke hodari amekuwa mfano bora na isitoshe kama mama basi hili atalibeba kwa hekima kubwa na ataliangalia pia kwa jicho la ziada kuhakikisha kwamba katika bajeti ya mwaka huu tunakuwa na fungu maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu na sio kudandia katika mafungu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia kuhusiana na watu wenye ulemavu, naendelea kupongeza kwa sababu naona mabadiliko makubwa na ndio maana naendelea kujivunia, mwaka jana tulipitisha sharia...

MWENYEKITI: Ahsante kengele ya pili.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa namna ya pekee namshukuru Mungu kwa nafasi hii na nawapongeza Wenyeviti wote wawili wa Kamati hizi kwa kazi nzuri kabisa. Kimsingi kwa kiwango kikubwa sana binafsi nakubaliana na mapendekezo yao lakini nina mambo machache ya kuchangia. Miongoni mwa mambo ambayo kwa upande wangu, naona ni mafanikio ya juu kabisa ya Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli toka imeanza, ni lile jambo la uchumi jumuishi. *World Economic Forum* ilitangaza Tanzania kwamba ndio nchi inayoongoza kwa kuwa na uchumi jumuishi kwa mwaka 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa kwamba ni uchumi ambao mbali ya kujali saizi yake au unafanyaje kazi, kwa uzuri kiasi gani, unajumuisha watu wengi wa makundi yote kwenye nchi husika, hili ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulileta kwenye muktadha wa leo, juzi tarehe sita nilimsikia Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli akisihi mahakama zetu mhimili wa mahakama, kwamba sasa wakati umefika wa kuanza kuhakikisha kwamba sheria zetu sasa zinaandikwa na kufanyiwa kazi kwenye mahakama kwa lugha ya Kiswahili. Kwa nini naona hilo ni jambo zuri, mtafiti mmoja amefanya utafiti mwaka 2014 hapa Tanzania anasema miongoni mwa Watanzania milioni 54, asilimia 90 wanaongea Kiswahili na asilimia nne wanaongea Kiingereza nne tu na waliosalia ndio wanaongea zile lugha za kienyeji kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria yetu ya Tafsiri za Sheria kifungu cha 84 kina vifungu vitatu, cha kwanza kinasema *the language of the laws of Tanzania shall be written in English or Swahili*, kwamba itakuwa kwa Kiingereza ama Kiswahili na pale ambapo hizo *version* mbili zinagongana, ile *version* ambayo ndio *original* sheria ilitengenezwa kabla ya kutafsiriwa ndio itatumika, lakini pale ambapo zilitungwa zote kwa pamoja Kiingereza kitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo swali langu ni kwa nini tunapambana kujiondoa kwenye utegemezi wa mambo ya kiuchumi na mengine lakini hatutaki kuondoka kwenye utegemezi wa mambo ambayo yanatupa nafasi ya wananchi wetu kushiriki vizuri pale wanapotaka haki zao, kushiriki vizuri pale ambapo wanatakiwa kujieleza, kushiriki vizuri pale ambapo hata kama anasimamiwa na Wakili mahakamani, pamoja na kwamba hana uwezo wa kufanya tafsiri ya kisheria, lakini angalau awe na fursa ya kuelewa Wakili wake anasema nini mwenendo wa Wakili wake unakwendaje kwa maana ya hoja. Hiyo inakuwa ni sehemu ya kupata ile haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 71 ya Katiba ni mfano ambapo kifungu kile kinatoa masharti ya ni namna gani mtu atapoteza nafasi ya Ubunge. Kuna tofauti kwenye *version* ya Katiba ya Kiingereza na ya Kiswahili, ambapo kifungu ambacho kinasema kwamba yoyote ambaye

samahani niangalie kidogo hapa, kifungu (e)lwapo Mbunge atachaguliwa ama kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais ni moja ya masharti ya ibara hiyo kwamba atapoteza Ubunge, lakini *version* ya Kiingereza ya ibara hiyo inaongea kitu kingine. Kwa hiyo suala hili limeshatokea mahakamani, ukatokea mtafaruku, sio mtafaruku wa maana ya kukosea nini kinasema pale, lakini mtafaruku wa maana kwamba kilichoandikwa upande huu ni tofauti kabisa na kilicho upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakamani wanatoa haki ya Katiba ya Kiswahili kwamba ndio iwe ya kwanza kufanyiwa rejea kabla ya ile ya Kiingereza kwa sababu Katiba yetu ilitungwa kwa Kiingereza kama *version* ya kwanza kabla ya kutafsiriwa. Ushauri wangu niombe Serikali hebu tufanye mabadiliko tulete hadhi ya lugha yetu, lakini na fursa ya watu kushiriki kwenye haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika ukurasa wa 41 wa ripoti ya Kamati ya Katiba na Sheria, wanasema moja ya mapendekezo yao ni usimamizi wa utoaji haki nchini kwamba ni jambo la muhimu sana na wameeleza pale. Nimewahi kushuhudia Biharamulo miongoni mwa mahabusu ambao wamewekwa gerezeni pale kwa muda mrefu kabisa, nilipata fursa siku moja nikaingia gerezeni pale, nikazungumza na baadhi yao kila mmoja akasema jambo lake. Nikagundua kwamba kulikuwa na mambo ambayo mengine hata sikuwahi kudhani kama yako dunia hii, lakini nikachukua fursa nikamwomba Waziri wa Sheria wakati huo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe alifanya kazi nzuri sana akaja na *DPP* pale wakasikiliza watu kwa siku moja tu, kuna mahabusu 40 waliondoka mle gerezeni kwa sababu ukaaji wao mle ulikuwa kwa kweli huko kinyume cha sharia, wengine hata zile hati za kuwafutia mashtaka zimeshatolewa miezi sita iliyotangulia lakini watu wako mle. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwe na utaratibu mbali na hii ambayo Mbunge anaweza kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria na *DPP* kwenda, tuweke

utaratibu wa kimfumo wa kuhakikisha tunaweza tukafanya *checks and balances* za mambo kama haya kwa sababu kuna watu wako kule chini hana mahali pa kusemea, anaminywa haki yake, anakaa miaka miwili, mitatu bila sababu ya msingi na ushahidi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe nilikwenda nae katika Gereza la Biharamulo, waliondoka watu 40 kwa yeye na *DPP* kukaa na kuwasikiliza watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Kamati ya Sheria Ndogo, katika ukurasa wa sita yapo mambo ambayo wanalalamika, wanasema kumekuwa kuna tatizo la sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyinginezo za nchi, lakini kuna matatizo ya sheria ndogo kuwa na makosa ya uandishi, matatizo ya sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi, kwa mfano *hansard* zinaonesha wamewahi kupata *report* ambayo sheria mama inasema kosa fulani adhabu yake ni shilingi 100,000, sheria ndogo kule imekwenda imefanya kitu kwenye muktadha ule unasema 300,000 kwa sababu ya makosa ya uandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo unaweza kuona ni kosa la uandishi kwenye karatasi, lakini huko kwenye *field* haya mambo yanaumiza watu. Tunaomba tujue namna gani Wizara inayohusika watachukua hatua kwa sababu kumbukumbu za Bunge zinaonekana kwa Kamati hii haya ni malalamiko ambayo yamekuwa yanajirudia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru na naunga mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Najma Giga.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nitachangia katika taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria katika maeneo machache, lakini la kwanza nitaanza ni katika suala la kuwajengea uwezo kiuchumi vijana ambalo linafanyika kwa kutumia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Naomba nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada ambazo zinafanyika katika kuwawezesha hawa vijana ambao ndiyo inapunguza kasi ya changamoto ya ajira katika nchi yetu. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya kwamba sehemu hii mwaka 2015/2016 zimetolewa bilioni moja; 2017/2018 zimetolewa bilioni 2.7; na naamini baadae wataendelea kutoa zaidi na zaidi, hii ni nia njema. Tatizo ndiyo hilo changamoto imeonekana, naomba niiseme ili iweze kufanyiwa kazi na Serikali, ni usimamizi wa hivi vikundi vya vijana ambao wanapewa hizo fedha, yaani hizi SACCOS. Kwa kweli imeonekana kwamba hizi fedha zimetolewa kwa lengo jema, lakini vikundi ambavyo vinapewa vinaonekana kwamba vinatumia hizo fedha kinyume cha malengo waliyojiwekea, hiyo ni changamoto. Pia inaonekana kwamba hizo fedha pia zinatolewa bila kuelewa kama hicho kikundi kweli kipo ama hakipo. Kwa hiyo wito wangu ni kwamba Serikali iweze kuzisimamia au kuzishinikiza halmashauri zetu ziweze kusimamia hivi vikundi vya vijana ili lengo jema kabisa la Serikali ambalo limekusudiwa liweze kufanikiwa. Hiyo ni sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni suala la ufinyu wa ukomo wa bajeti kwa baadhi ya taasisi zinazosimamiwa na Kamati ya Katiba na Sheria ambayo ni miradi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika sehemu ya Bunge, Kazi, Vijana na Ajira na Wenye ulemavu. Hii imeonekana kwamba miradi mingi inategemea fedha za nje, hii ni changamoto. Kutegemea fedha za nje ni changamoto na kwa nini nasema hivyo? Nasema kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshaligundua hilo kama ninavyoliona mimi na Watanzania wengi naomba waelewe hivyo. Fedha za ndani ni muhimu, kwa hiyo ili tuweze kupata fedha za ndani lazima wananchi tuhimizwe kukusanya kodi kwa wakati, tulipie, tuwe watiifu, tutengeneze miradi mingine kupitia Serikali yetu ili tuongeze vyanzo vya mapato ya ndani ya nchi yetu na hili jambo linafanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuongeze jitahada ya kuunga mkono Serikali kuongeza mapato ya ndani ya nchi. Misaada ina madhara, Waheshimiwa pamoja na Watanzania naomba tuelewe hivyo, ukiona unasaidiwa, basi kuna lengo fulani linatakiwa huko. Kwa hiyo sasa hii tuikwepe kwa njia yoyote na napongeza sana kwa kweli jitihada za Mheshimiwa Rais ameliona hilo na ameligungua na ndio maana anakwepa hii misaada ya nje kwa gharama yoyote. Kwa hiyo na sisi tumuunge mkono tuendelee kupigania fedha zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo kubwa ambalo nimeona pia ni upande wa magereza, naomba nizungumzie kwa upana wake. Lengo la kuweka magereza ni kuwapa mafunzo wale wanaofanya makosa ya aina mbalimbali ili wakitoka nje uraiiani waachane na hayo, wafanye mambo mema ili wawe kama raia wa kawaida waweze kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo naomba nielezee hapa kwa undani, ni jinsi ambavyo magereza yetu pamoja na mahabusu zinavyokusanya wafungwa wa aina tofauti; mwizi wa kuku, mbakaji, muuaji, jambazi sugu, wote wako pamoja wanafungwa pamoja. Si hivyo tu, mwenye miaka 18 ambaye anajulikana huyu sasa ni mtu mzima na kuendelea hadi kufika 30 humo humo ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokusudia hapa ni hivi, tunawaweka kule ili wapate mafunzo, wakija uraiiani wawe watu wema, badala yake mule ndani watoto wetu ambao ni vijana kuanzia miaka 18 ni kijana tunavyosema kwa mujibu wa sharia, wanatoka mule ndani wamebakwa, wamelawitiwa, wanarudi uraiiani wameisha hawana nguvu kazi ya vijana, kwa hiyo hilo nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufanye mpango maalum wa magereza yetu kupitia Serikali ili tuone utaratibu maalum hawa wabakaji sugu wawekwe tofauti na watu wengine, wanania uchungu mimi wanawaharibu watoto

wetu vijana. Pia hawa wauaji, majambazi sugu nao wanafundishana vitendo viovu, wanaweza wakawafundisha vijana wetu mambo ambayo yatawajengea uwezo, wakitoka huku nje badala ya kuwa mwizi wa kuku anakua muuaji, kwa hilo jamani naomba sana Serikali itafakari kwa kina kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi na hukumu zinazotolewa mahakamani, hata ukija kwenye hiyo *money laundering* yaani utakatishaji wa fedha, inawezekana yule mtu ambaye amefungwa kwa kutakatisha hizo 300,000, hizo 300,000 zimepatikana labda pengine kwa mafunzo ya ugaidi, kwa mafunzo ya uuaji, kwa hiyo anaweza akafungwa hata miaka sita, hata miaka 10 hata zaidi *there is no problem*. Kwa hiyo hiyo mimi sina pingamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba upande mwingine nimalizie kwenye *challenge* ambayo tunayo kwenye mazingira wezeshi ambayo wenzangu wamezungumza na mimi nitumie fursa hii kupongeza uongozi mzima wa Bunge naona jengo letu linakarabatiwa kwa hiyo kutakuwa na *lift* karibuni na itakuwa ni mazingira wezeshi kabisa kwa wenzetu wenye ulamavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kwamba sasa Serikali iweze kuona mpango mzuri wa kutekeleza sheria ya mwaka 2010 ili Baraza hili sasa la Watu Wenye Ulemavu liweze kuanzishwa lakini pia na Mfuko wa Maendeleo ambao umekusudiwa kwenye sheria hii uweze kuanzishwa na kuweza kuwasaidia kwa umakini hao wenzetu wenye ulemavu. Suala la mwisho katika upande wa watu wenye ulemavu ni kwamba, halmashauri zetu ziweze kushughulikiwa kwa ukamilifu kuona kwamba ile asilimia mbili inawafikia walengwa kwa wakati mahususi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo natumia fursa hii kukubali hoja hii ya Kamati ya Katiba na Sheria kwa maana ya taarifa nzima kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais, sina pingamizi, mambo yanakwenda vizuri, changamoto ndogo ndogo naamini zitafanyiwa kazi, lakini

kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu nao pia nitumie fursa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Mifuko ya *WCF, OSHA* na Taasisi zote zinafanya kazi kuwawezesha wafanyakazi wetu katika hali nzuri kufanya kazi, pia malipo ya fidia nayo yanafanya kazi kwa uzuri, kwa hiyo nitumie fursa hiyo, kama kuna changamoto ndogo ndogo tuzirekebishe. Kwa ujumla wake natumia fursa hii kukubali hoja zote za Kamati kama zilivyo, lakini na kuipongeza Serikali kwa kadri ambavyo wanajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha, jioni tutaanza na Mheshimiwa Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Selasini.

Waheshimiwa kama mtakumbuka kuna agizo la Mheshimiwa Spika alilolitoa kwa Wabunge wote wenye kero za ardhi wanaagizwa kuonana na Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi saa saba mchana leo katika ukumbi wa Msekwa. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Tunaendelea na majadiliano na nilishamtaja Mheshimiwa Kubenea ajiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Selasini.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Sehemu ya Utangulizi ambayo inasema: “Kwa kuwa sisi Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, undugu na amani. Na kwa kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo Serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi, na pia wenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenukuu msingi huu wa Katiba nikirejea kesi mbalimbali ambazo zimepelekwa Mahakamani na zimecheleweshwa kwa makusudi kabisa. Moja ya kesi ambayo nataka niitolee mfano ni ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye alifungwa na Mahakama ya Mkoa wa Mbeya, akakata rufaa kwenda Mahakama Kuu na aliomba awe nje kwa dhamana wakati shauri lake linasikilizwa lakini Mheshimiwa Mbilinyi alikaa gerezani kwa kipindi chote cha kifungo chake hadi pale alipotoka baada ya kupata msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu inasema Mahakama itende haki bila kuangalia sura ya mtu lakini wapo watu ambao wamekosa haki zao kwa makusudi kabisa kwa utaratibu ambao Mahakama imeshindwa kuwapa haki hizo. Taarifa zilizopo ni kwamba Jaji aliyekuwa *Incharge* kwenye kesi ya Mheshimiwa Mbilinyi alikiri kwamba alishinikizwa kuendelea na shauri lake kulipeleka mbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kubenea haya maneno unaweza ukayathibitisha?

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENE ULEMAVU): Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENE ULEMAVU): Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64(1)(e). Namheshimu sana Mheshimiwa Kubenea lakini naomba tu nimsaidie kanuni hii haituruhusu kabisa kuzungumzia miendeno ya shughuli za watoa haki wakiwemo Majaji, Mahakimu, Mheshimiwa Rais mwenyewe, Mheshimiwa Spika lakini hata sisi wenyewe Wabunge tumewekwa katika kanuni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea anaweza kabisa akaendelea kuchangia mchango wake vizuri lakini nadhani si sahihi sana akianza kuzungumzia mienendo na hasa katika utoaji wa haki wa hawa waliotajwa kwenye kifungu hiki cha (e). Nadhani hata sisi Bunge lako litakuwa linaingilia kazi za mihimili mingine. Nadhani tu Mheshimiwa Kubenea atambue kanuni hii na aendeleo na mchango wake. Narudia kusema kwamba kwa kweli tuache kuzungumzia hawa watoaji wa haki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nakubaliana na wewe na nilianza kuingilia kati. Mheshimiwa Kubenea kaa kwanza. Ni lazima tujue humu ndani tunakwenda kwa Kanuni na kuzungumzia mihimili mingine kesi iwe imekwisha au hajjakwisha siyo sahihi. Tafuta maneno sahihi ya kuzungumza na unayo mengi ya kuzungumza, kwa hiyo, mambo ya Mahakama na haki za Mahakama siyo sahihi sababu hata tukikwambia uthibitishaye haya maneno mtu alishinikizwa sijui ushahidi huo utauotoa wapi. Kwa hiyo, ili kujiepusha na madhara ya mbele endelea na mchango wako kwa mujibu wa Kanuni na hoja iliyokuwepo mbele yako.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bunge hili lilipokea Muswada wa *Mobile Court*, uliletwa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, Serikali katika mvutano wa adhabu ambazo zilikuwa zimependekezwa katika Mahakama hiyo ikaondoa ule Muswada. Hata hivyo, juzi wakati wa uzinduzi wa Siku ya Sheria tumesikia kwamba Mahakama imezindua *Mobile Court*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mashaka ya Wabunge yalikuwa *Mobile Court* ina gharama kubwa sana. Gari moja lilikadiriwa kuwa na thamani kati ya shilingi milioni 200 mpaka milioni 490. Tukasema gharama za kuendesha *Mobile Court* ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ni kubwa kuliko tukiamua kujenga Mahakama za Kata. Pia tukasema katika baadhi ya maeneo gari hili haliwezi kufika na tukatoa mfano kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kule juu milimani, gari hili la *Mobile Court* haliwezi likafika. Lingine lilikuwa ni eneo la maamuzi yenyewe na hasa katika eneo la *fine* ambazo zitaenda kutozwa kule na haki ya watu kupewa wakili na kusikilizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Muswada unaletwa Bungeni tayari tenda au magari yalishaagizwa kutoka nje. Kwa hiyo, Bunge lilikuwa linatumika kuhalalisha kitu ambacho tayari kilikuwa kimeshafanyika.

TAARIFA

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji. Yeye mwenyewe ametoka kuzungumza hapa kwamba huu Muswada ulikuwa *withdrawn* haukuletwa Bungeni. Sasa anasema Muswada wakati unaletwa tayari gharama za hayo magari zilikuwa zinashughulikiwa, sasa sijui Muswada gani anauzungumzia kwa sababu haukuletwa hapa Bungeni.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana kaka yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Mwakasaka, nikizungumzia Kamati ya Bunge nazungumzia Bunge Dogo. Nimesema Muswada ulikuja kwenye Kamati ya Katiba na Sheria na ukaondolewa na Serikali, sasa sijui, aah, naomba niendelee tu.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza, kama alikuwa hafahamu, moja kati ya faida za *Mobile Court* ni kuharakisha na kurahisisha usikilizaji wa mashauri. Hii inasaidia kutatua changamoto ambayo alianza kulalamika yeye mwenyewe kwamba mashauri yamekuwa yakichelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo, Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, alikuwa anazungumza hapa juzi akasema sisi Wabunge tuwe wavumilivu, tuwe tunasikiliza na wenzetu, usikilize kile ambacho pengine wewe hutaki kukisikia. Huyu mwenyewe hapo nje alikuwa analalamika na wenzake wawili na wenzake watasimama sasa hivi kwamba Rais Magufuli hasikilizi watu, sasa wewe unapata wapi *moral authority* ya kuniambia mimi. Kwa hiyo, taarifa yake nimeikataa.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TIMOTHE P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1) kwamba, Mbunge hatatoa taarifa ambazo hazina ukweli ndani ya Bunge lako. Mbunge anayezungumza anasema tulikuwa tukilalamika mahali, kwangu jambo hili si la kweli, naomba alithibitishie Bunge lako hicho anachokisema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, Kanuni hiyo inataka wewe ndiyo uthibitishie. Mheshimiwa Kubenea endelea. (*Makofi*)

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ibara ya 74(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inazungumzia juu ya uwepo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo tunayo sasa imeundwa na kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Na.1 ya mwaka 85 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia muundo na mfumo wa Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu ujao na jinsi Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wanakatazwa na Katiba hii kwamba watu wanaojihusisha na vyama vya siasa (makada) wasiwe wasimamizi wa uchaguzi lakini ukiangalia huko chini muundo wa Tume, ukiacha pale juu unatutia mashaka kwamba tunaweza tukaenda kwenye uchaguzi mkuu wa 2020 tukiwa na amani na usalama. Niishauri Serikali na niiombe sana kwamba ifanye marekebisho ya Tume yetu ya Uchaguzi ili yale mambo ambayo yametokea Zanzibar mwaka 2001, yametokea Kenya na katika mataifa mengine yasije yakatupata na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina picha za Wakurugenzi wa Halmashauri ambao walikuwa makada wa CCM na walikuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Wengine asubuhi wanakuwa makada wa CCM na mchana wanaenda kusimamia uchaguzi, kinyume na Katiba yetu, kinyume na Sheria ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hatua ya Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Jecha Salim Jecha, kuamua tu binafsi kufuta uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kengele ya pili.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pareso unazungumza na Kiti au Makatibu? Mheshimiwa Kubenea dakika zake zilikuwa ni 10 na ninyi ndiyo mmempangia 10, alianza dakika na dakika 11 amesimamishwa dakika 11.

Tunaendelea na Mheshimiwa Getere ajiandae Mheshimiwa Selasini.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwanza kwa kuzishukuru Kamati zote mbili, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo. Vilevile niwapongeze Wajumbe wa Kamati hizo na Mawaziri walioshughulika na Kamati hizo kusaidia kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natazama vitu katika Kamati hizi na nimeona kuna jambo nataka nilizungumze la Kamati Ndogo kuhusu kile kipengele cha Kodi ya Majengo. Kipengele hiki cha kodi ya majengo wakati

kinatekelezwa katika maeneo yetu kimekuwa na vitisho vingi sana. Kwa hiyo, naomba wakati wanafanya ufuatiliaji wa kipengele waangalie kwa sababu huko vijijini kuna nyumba za nyasi na nyumba za bati, ilifika wakati ukijenga nyumba ya bati unadaiwa kodi, ikaonekana kama ni Kodi ya Kichwa hivi. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie vizuri kwenye kodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Taifa ni letu wote na kama kuna watu wana ndoto kwamba nchi hii ni ya Rais John Pombe Magufuli na chama chake na wako tayari kuiharibu kwa wakati wowote wanavyotaka kwa maslahi yao watakuwa wamekosea sana. Hotuba nyingi zinazokuja hapa hata ya ndugu yangu hapa Mheshimiwa Kubenea anauliza habari ya ma-*DED* kwamba ni makada wa CCM, lakini hapa tuna Wabunge zaidi ya 100 kwenye uchaguzi uliopita na wametangazwa na ma--*DED* hao wanaosema ma-*DED* wa CCM. Sasa *DED* amemtangaza kuwa ameshinda, amekuja Bungeni halafu anamsema ni mbaya, sielewi kinachoendelea huko mbele katika mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yanazungumzwa hapa. Nilikuwa natazama sana wakati Rais wa United State, Trump, alivyo-*tweet* juu ya *White House*, kuhusu ya Wazungu wale weupe wa South Africa kwamba anataka kuwalinda wale Wazungu kwa maana ya ardhi ya South Africa. Nikamtazama Julius Malema, nikamtazama Ramaphosa ambaye ni Rais, wote walikusanyika pamoja kutetea ardhi ya South Africa bila kujali upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimuona Malema alienda mbali zaidi anawaandaa wanachama wake anawaambia tuko tayari kufa kwa ajili ya ardhi yetu, hatuko tayari kutoa ardhi yetu kwa sababu ya umasikini wetu au kwa sababu hatuna uwezo wa kufanya jambo hili. Huyu ni mpinzani wa South Africa lakini nchi yetu leo hata tungezungumzia habari ya kugeuzwa kuwa wanawake tayari watu wanatetea. Mimi sielewi kama katika nchi hii hali ya hewa inavyoenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanazungumza *democracy* lakini wanashindwa kutofautisha *democracy and futures of democracy...*

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere, subiri kidogo, kuhusu utaratibu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(c). Mzungumzaji amesema kwamba hata kama wote tungegeuzwa wanawake, hii ni kauli ya kudhalilisha akina mama. Akina mama wa nchi hii wana haki sawa na akina baba na siyo viumbe dhaifu. Kwa sababu hiyo, nakuomba umtake afute hiyo kauli yake na tena tukizingatia Bunge hili lina Naibu Spika ambaye ni mwanamke. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Getere futa hilo neno.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa heshima ya Paroko nafuta hilo neno, tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine wakati fulani unaweza ukaongea hata ukachanganyikiwa kwa sababu leo kama tuna watu ambao ni Watanzania wanaodhani kwamba Rais au utawala wa nchi hii ambao tuliupata bila kumwaga damu na kuna watu walihangaika kuupata kwa kuzunguka tukapata uhuru, leo ni mwaka wa 48, wanadhani kwamba nchi za Ulaya, za Mabeberu wanaweza kuamrisha Watanzania wakampa mtu Urais kwa kupitia nchi za Ulaya, haya ni mambo ya ajabu na ya aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais aliyekuwa maarufu sana hapa duniani na Afrika, Nelson Mandela, alifungwa miaka 27. Alipotoka jela wala hakwenda Ulaya kutafuta Urais, alikaa kule kwake na wala alipotoka jela wala hakutafuta nani alimweka jela. Alikaa kwenye nchi yake akawaambia uhuru tunautafuta na uhuru akapewa na Wazungu waliomweka ndani miaka 27 akaishi nao, ni historia kubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mtu akikosewa dakika mbili, dakika tatu, imekuwa matatizo. Leo tuna Rais bora kabisa katika nchi za Afrika, ameandikwa humu ndani ukisoma, ana miaka mitatu lakini ameandikwa anafanya vizuri. Leo nchi yetu ni ya 10 kwenda kwenye uchumi bora katika nchi za Kiafrika. Sasa leo wanapita tu wanachafua nchi yetu ambayo ni yai letu la kulea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale wote ambao wana mawazo hayo warudi tufanye kazi ya ndani wasichanganye demokrasia na utekelezaji wa demokrasia. Kama kuna utekelezaji mtu anazungumza ni watu wanafungwa na kesi zinacheleweshwa, mmeona juzi Mheshimiwa Rais ameteua Majaji na anaendelea kuteua ili mambo ya kesi yaende vizuri na mambo mengine pia tunaendelea kuyatendea haki, mfano, uchaguzi tumechagua vizuri na tunaendelea kuchagua. Tunapozungumzia demokrasia maana yake nchi yetu inatekeleza demokrasia. Tumechagua Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji, Madiwani, Wabunge na Rais hiyo yote ni demokrasia, sasa demokrasia inayozungumzwa ni ipi, mimi sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wasilete hofu kwamba utendaji mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli watakosa vyeo, ukikosa cheo ni Mungu ameamua, siyo wewe sasa. Mungu akisema wewe huwezi kuwa Mbunge huwezi kuwa Mbunge. Kwa hiyo, tukubali kwamba nchi ni yetu tumsaidie Rais afanye kazi vizuri ili tuendeleo kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, chama ni chenu na Ilani ya Uchaguzi inayotekelezwa ni yenu, tufanye kila namna tumsaidie Rais afanye kazi yake vizuri. Pale ambapo tunahitaji kumshauri, tumshauri vizuri, pale tunapotakiwa kutenda, tutende vizuri. Tukianza kuwa tofauti maana yake ni kwamba chama chetu kinakwenda kufa, kwa sababu aliye na dhamana ya kusimamia Chama cha Mapinduzi kwa sasa ni Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Huyu ndiye mchezaji wetu wa Chama cha Mapinduzi, tukimyumbisha wakamkanyaga mguu ukavunjika maana yake chama chetu kinaenda kupata matatizo, kwa hiyo, lazima tumlinde kwa heshima zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru tumeupata, nchi yetu ipo, ina miaka 48 na ina sifa, ni nchi pekee duniani yenye Muungano. Nataka niwakumbushe watu, tusipokuwa watetezi wa mambo mazuri tuliyoyafanya, kama mwaka 1995 Muungano wetu ulivyotaka kuyumba, asingesimama imara Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius Nyerere, akaita Bunge na Halmashauri Kuu ya CCM na tukakubali kuendelea na Muungano leo Muungano usingekuwepo. Kama hatuwezi kuungana kutetea nchi yetu maana yake wote tunaweza kwenda kwenye matatizo. Nchi yetu ni ya amani na watu wetu hawakuzoea mabomu na timbwilitibwilli nyingi, kwa hiyo, tunaomba watu wawe na amani na tuombeane amani ili tuweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kusema kwamba tuko hapa Bungeni kwa ajili ya kumsaidia Rais. Hakuna Mbunge yeyote humu ndani ambaye lengo lake siyo kumsaidia Rais. Mawazo tunayotoa hapa lengo lake ni kusaidia ili nchi hii iweze kuongozwa vizuri. Kwa hiyo, Bunge lisipotoshwe kwamba

kuna watu ambao wako hapa wanafanya hujuma dhidi ya uongozi wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nilishauri Bunge na Taifa acheni Mheshimiwa Lissu afanye anachofanya kwa utashi wake. Tunapoteza muda na nguvu kujadili habari ya Mheshimiwa Lissu. Nguvu hizi tungezitumia wakati alipopigwa risasi kama Wabunge ingeonekana tumefanya jambo la busara sana lakini alivyopigwa risasi, alivyokuwa hospitali, alivyokuwa anahangaika na matibabu tulikaa kimya. Sasa hivi Mungu amemjalia pumzi acheni aseme. Kama kuna jambo ambalo atakosea atakuja ahojiwe mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa jambo la Uchaguzi Mkuu na Tume ya Uchaguzi. Pia Serikali wiki iliyopita ilijibu maswali kuhusu Tume ya Uchaguzi na maandalizi ya uchaguzi ujao kwamba imeanza taratibu za kuboresha daftari, hili ni jambo zuri. Mwenzangu amechangia juu ya kupitia hata Tume yenyewe na kuhakikisha kwamba watendaji wa Tume wanateuliwa watu huru na watakaosimamia uchaguzi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chaguzi katika nchi mbalimbali zimeleta fujo sana na zimesababisha mataifa mengi kuvurugika. Kwa hiyo, naikumbusha na kuiomba Serikali, uchaguzi wa 2020 ni wakufa na kupona, naomba sana maandalizi ambayo mmeamua kuanza kuyafanya yawe shirikishi, wananchi washirikishwe, vyama vishirikishwe na kila mdau ashirikishwe. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa taarifa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa kwamba uchaguzi wa 2020 siyo wa kufa na kupona bali ni CCM inakwenda kushinda kwa kishindo kutokana na kazi nzuri aliyofanya Rais wetu Dkt. John Joseph Magufuli. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, taarifa hiyo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleee. Uchaguzi Mkuu unatanguuliwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mwaka huu kila mmoja wetu alitegemea kwamba maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yangeshaanza kufanyika. Kama tunavyojuwa maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanaanza na kanuni na kuwashirikisha wadau. Naomba sana maandalizi yawe wazi, wadau wote washirikishwe, kwa sababu uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita ulikuwa na fujo za hapa na pale.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Mbunge wa Rombo kwamba ni kweli mwaka huu ni wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa na maandalizi yamekwishaanza. Kwa kawaida hili jambo kwa sababu ni kanuni zinashughulikiwa na wataalamu, Ofisi ya TAMISEMI huwa inafanya kazi hiyo, mapendekezo yanapokelewa na itapelekwa kwa vyama vya siasa na kutoa maoni ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, unazo dakika zako za kujibu hoja hii. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wamekuwa wanatukatia muda wetu na Kiti kimekuwa kikipunguza muda wetu. Hakuna mtu huku anachangia dakika kumi hata mmoja ni saba, nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wahusika washirikishe wadau na wadau ni vyama vya siasa na kadhalika, tuweze kuzipitia hizo kanuni ili uchaguzi uweze kwenda vizuri, tuweze kupata viongozi wa kutuongoza sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo haraka haraka nizungumzie kuhusu yanayotokea katika nchi. Tutafika mahali nchi hii tutaingia kwenye matatizo makubwa. Yapo mauaji na vifo ambavyo hadi sasa hakuna matokeo ya uchunguzi wake na nitataja baadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichinjwa Mwenyekiti wa CHADEMA wa Arumeru, hakuna taarifa mpaka sasa hivi; Ben Saanane hakuna taarifa; Azori Gwanda hakuna taarifa; David John wa Ananasifu hakuna taarifa; Simon Kangoye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo kupitia Chama cha Mapinduzi hakuna taarifa; Akwilina Akwilini, Kamanda wa Kanda Maalum anasema faili limefungwa wakati anasema alikamata askari sita ambao walituhumiwa kumpiga risasi; Petro Shemasi wa Itigi ambaye baba yake anasema alishuhudia Mkurugenzi akimlenga risasi ya kichwa, leo Polisi wanaanza kusuasua na kuweka mambo ili kulinda wauwaji; yupo Alphonse Mawazo na Lwena wa huko Kilombero. Siyo hao tu, wapo Watanzania wengi ambao wamekwishauwawa kwa sababu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi hii tunauwana hovyoy namna hii, tuna Polisi na vyombo vya dola lakini hakuna taarifa tunaona ni jambo la kawaida tu, tukumbuke kwamba familia za hawa waliouawa...

T A A R I F A

MHE. AMINA S. MOLLEL: Taarifa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Kaa chini bwana.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Aah!

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Amezungumzia kuhusiana na mauaji mbalimbali kama ambavyo ameelezea lakini napenda tu kumpa taarifa kwamba kule Kibiti waliuawa watu na hasa walikuwa wanalenga upande mmoja wa watu ambao kwa namna moja au nyingine wanahusiana na Chama cha Mapinduzi lakini Serikali iliweza kufanya vizuri na hatimaye imetokomezwa yale mauaji.

MWENYEKITI: Taarifa hiyo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja akiuawa, ni jambo kubwa sana katika nchi na unachoniambia wewe Mbunge wa CCM ni kwamba Serikali imeshindwa kuchunguza haya mauaji kwa sababu mimi sitetei wauaji wa Kibiti, sitetei wauaji wa sehemu nyingine yoyote, nachosema ni kwamba wajibu namba moja wa Serikali ni kumlinda raia na mali zake, wauaji waue Kibiti...

T A A R I F A

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, subiri kuna taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Mheshimiwa Selasini na kule Kilwa walipigwa Waislam Msikitini wakafa watu wawili mpaka leo uchunguzi haujapatikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema na kuiomba Serikali, mauaji ya holela katika nchi hii itafute namna ya kuyakomesha. Mimi sizungumzi habari ya kauawa wa CCM au CHADEMA. Nachosema tukiendelea na huu mchezo ni kwamba itafika mahali kisasi kitalipwa. Nasikitika yakizungumzwa mambo kama haya Wabunge wazima wanapiga makofi, wanacheka, wanabeza, wanatoa miongozo na nini kama vile hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi Wabunge wa CCM shaurini Serikali tutafute namna ya kukomesha haya mauaji kwa sababu leo hii ukinigusa mimi, mimi nina watoto, nina ukoo usitegemee kwamba watoto na ukoo wangu utachekelea tu hivi hivi, pengine ukiniua kuna *reaction* itatokea huko. Ndiyo maana nasema chonde chonde, Waziri wa Sheria kaka yangu Mheshimiwa Kabudi, kaa na vyombo kwa utulivu na amani kabisa, kaa na *DPP*, *IGP* na wengine wote hii ni aibu nimetaja watu karibu 20 wameuawa lakini hakuna uchunguzi, hakuna chochote, ni kama mbuzi tu. Hata hawa wa Kibiti waliokamatwa, nasema lazima washughulikiwe vinginevyo tukienda hivi, nchi hii itafika mahali kisasi kitatembea barabarani na haitakuwa jambo la maana. Rwanda ilianza kidogo kidogo hivi ikachochea na vyombo vya habari matokeo yake Rwanda ikalipuka, sisi hatuna tofauti na Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, limezungumzwa hapa jambo la walio mahabusu. Hoja hapa ni kwamba walio mahabusu wanaweza kutafutiwa njia nyingine. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Selasini. Nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Mollel, ajiandae Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba tunaishi kwenye dunia ambayo ina rasilimali za kudumu na zinaisha. Ili nchi iweze kuendelea ni lazima sheria zote ambazo zinatungwa katika Taifa zielekeze kuzisimamia rasilimali hizo na kuziweka katika *chain* ambayo izitafanya ziwe endelevu. Katika kuwekeza kwenye rasilimali ambazo zina tabia ya kuisha, fedha ambazo zitapatika ni lazima ziwekezwe ili zikiisha basi pato la Taifa liweze kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja sehemu ambazo ni muhimu sana kuwekeza, kwanza, kuwekeza kwenye *human capital* kwa maana ya rasilimali watu na ndiyo ambacho Serikali inafanya inawekeza sana kwenye elimu. Pili, kuwekeza kwenye *human made capital* kwa maana ya miundombinu ndiyo maana unaona Serikali inawekeza kwenye *Stiegler's Gorge*, treni, barabara, ndiyo kazi Serikali inafanya. Sehemu ya tatu ni kuwekeza kwenye *innovation* na *technology*, ugunduzi pamoja na teknolojia. Ugunduzi ninaozungumzia ni kuwekeza katika eneo litakalovumbua watu wenye uwezo wa kufikiri katika hali ya utupu, kukaa chini na kugundua. Leo Israel ni jagwa lakini kwa sababu watu wake wana uwezo wa kufikiri katika hali ya utupu, mimea inapewa dawa *specifically* siyo kurusha kama tunavyorusha sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tuna hizi rasilimali zinazohisha na tunataka kuwekeza huko tujue wenzetu katika mataifa mengine rasilimali zao zimekwisha. Wamefika mahali sasa wanatoka nje ya mataifa yao kwenda kutafuta maeneo ya kuwekeza ili waweze kuhakikisha usalama wa nchi yao kiuchumi. Ndiyo maana utakuta baadhi wanaweza kutumia vyama vya siasa au mtu mmoja mmoja kuvuruga baadhi ya mambo ambayo yanawazuia wao kuwekeza kwenye rasilimali za Taifa husika. Ndiyo maana utaona...

T A A R I F A

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe mzungumzaji taarifa kwamba siyo wageni wanaoharibu mipango yetu. Leo hii tunavyoongea Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro ametoa amri, ujenzi wa Hospitali ya Siha usimame na kilichojengwa kivunjwe kwa sababu ya matofali hafifu. Hii ni kwa sababu Mbunge anayeongea yupo pale lakini hasimamii hela za Serikali zinapotea. (*Makofi*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Selasini unajua vizuri ni yule rafiki yako wa pale Moshi ame-*supply* vitu *substandard*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sisi tulipokuwa upande ule wa Selasini, Selasini akituongoza kwa sababu walishaweka mkakati...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda umuelekeze mzungumzaji kwamba Wabunge tuna namna tunavyokuwa *addressed*, asimu-*address* Mbunge kama ana *address* mpiga debe.

MWENYEKITI: Ni sawa Wabunge mtaitana kwa heshima zenu, utasema Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Mbunge.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Paroko nimepokea hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa upande ule walianza na mkakati wa kuhakikisha wanazuia Serikali yetu isiwekeze kwenye maeneo haya ya kimkakati. Tukajipanga

namna ya kuzuia na kukwamisha Serikali ili isiwekeze katika eneo hilo. Mwenzetu Mheshimiwa Tundu Lissu akaonyesha kuwa kinara wa kuzuia hilo, yakatokea mambo mawili. Jambo la kwanza ikaonekana kwamba anatengeneza umaarufu binafsi lakini ya pili kwa sababu ni watu ambao wamepanga kuuza hili Taifa wakatuma watu wakampiga Tundu Lissu na kumuumiza... (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Ooh, ooh.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mollel, kuna kanuni inasemekana imevunjwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a), naomba Kiti chako kimitake athibitisha kwamba njama za kumdhuru Mheshimiwa Lissu zilifanywa na watu wa upande huu.

MBUNGE FULANI: Thibitisha wewe kwanza.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kuthibitisha. Namna ambayo nitathibitisha kwanza leo tu jioni hii nitatoka nje, isisemekane nimesema twende Mahakamani lakini CHADEMA wanilettee matumizi yao yote ya ruzuku na hela wanazotoa nje wanatumia kufadhili nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Daktari niliyewakilisha CHADEMA kwenye *postmortem* ya mabomu ya Arusha nilipotoka nikaiambia CHADEMA, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Selasini walikuwepo ni Mkutano wa Kanda, kwa sababu kilio chetu tunasema hatuamini Serikali kwenye kuchunguza kuna vitu nimeviiba huko ndani twendeni tupeleke kwa Mkemia Mkuu wa Afrika Kusini walikataa, waseme kwa nini walikataa na

walikuwa na ruzuku. Wanapinga suala la Mheshimiwa Tundu Lissu, Chacha Wangwe kilimtokea nini baada ya kutaka Uenyekiti? (*Makofi*)

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mollel kuna taarifa yako.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza, kwa sababu alikuwa ni Daktari aliyekuwa anachunguza kilichokuwa kimetokea na kwa bahati mbaya aliiba vitu fulani ambavyo alitaka kuwaonesha viongozi CHADEMA na baadaye aende nao South Africa ili wakajaribu kuangalia baadhi ya vitu. Kwa muktadha huo inaonesha kabisa kwamba si mwaminifu na alishindwa kufanya kazi yake kwa jinsi inavyotakiwa na...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mollel, taarifa!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu yuko CCM...

MWENYEKITI: Nimeshakuzuia, Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, anasahau kilio alichotoka kulia hapa Serikali isaidie, mimi nilikuwa kada mwaminifu, nikafanya kazi za chama lakini walinikwamisha wao, nikagundua kwamba wanajua kinachoendelea. Mnajua Mheshimiwa Zitto leo asingekuwa hai kwa kilichomtokea kama siyo Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kumlinda. (*Makofi*)

T A A R I F A

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ili ufanye uchunguzi wa jambo lolote ambalo limefanyika hapa nchini kwa kutumia vyombo vya nje ni lazima upate ruksa ya Serikali kwa sababu zipo taratibu za kufuata.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru aliyenijibu hapa ni mmojawapo wa wale waliokuwa wanatengeneza njama za kumng'oa Mbowe. Kwa hiyo, kuna uthibitisho dhahiri hapa kwamba huko kuna mafia wa kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze tu...

T A A R I F A

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, pale Igunga wakati wa Uchaguzi Mdogo sijui mwaka gani, kuna kijana yupo pale alimwagiwa tindikali na hao.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa kwa sababu tulikuwa pamoja na tulikimbia umafia kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kulikuwa na *plan* namba moja ya kuzuia Serikali isifanye kazi, katikati ya *plan* namba moja Lissu akapigwa risasi ili kuisisimua watu waivuruge Serikali yetu. *Plan* namba mbili ndiyo inaendelea Ulaya ambayo ni mwendelezo wa kufadhiliwa na wale watu wachafu. Mimi sisemi kuwa kuna nchi yoyote inafadhali ila ni watu wachafu ambao ni wezi wa rasilimali za kidunia. Tunataka kuwapa taarifa kuwa hakuna rasilimali ya Tanzania mtakayoweza kuipekea nje ilhali Watanzania wapo na leo tunawaambia ukweli. Tanzania haiuzwi kwa makubaliano ya ninyi kufika Ikulu, mkifika Ikulu mtasimamia nini? (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mollel, kengele ya pili. Tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Kamati hizi mbili; Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo katika kuweka mambo sawa juu ya sheria zetu na mambo yanayoendelea ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kabisa, naomba niruhusu nianze kwa kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili, Mheshimiwa Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo na Mheshimiwa Mchwengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Hakika kazi zao zinaonekana na binafsi napenda kuwaambia kuwa waendeleo kupambana hivyo hivyo kwa sababu sheria inataka wasimamizi wazuri kama wao na wanafanya kazi nzuri, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nishukuru na kupongeza sana sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa jinsi ilivyoendesha mchakato wa usimamizi wa utungaji kama si urekebishaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Hakika

mchakato ule ulikuwa mgumu kutokana na makundi mengi kuwa na *interest* katika jambo lile. Kwa kweli jinsi mchakato ulivyoendesha vyama na wadau walivyoweza kushirikishwa mpaka mwisho tumekuwa kupata marekebisho yaliyotokana na lile pendekezo la Serikali, kwa hakika ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia wanasiasa wenzangu kwamba siku zote tusitegeme kupata kitu kilichokamilika kwa asilimia mia moja isipokuwa kwa hii hii asilimia 90 tuliyopata tushukuru na pale kwenye upungufu basi twende katika taratibu za vyombo vya sheria ili kuweza kupata kilicho haki yetu au kile ambacho tunakiona kimekosewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, niendeleo kuzungumza na Mheshimiwa Waziri wa Sheria, mara zote tunapokutana kwenye Kamati ya Sheria Ndogo kilio chetu sisi kama Wanakamati kimekuwa ni dosari zinazojitokeza katika utungaji wa sheria. Makosa ya kiufundi katika uandishi, makosa ya kutotambua au kutoangalia sheria mama inasema nini, makosa ya kiuandishi kwa maana ya *copy and paste* na kusahau mamlaka, ni mambo ambayo yamekuwa yakiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa mawazo na maoni yetu katika mchango wetu kikao kilichopita kwamba Wizara yenu Profesa wangu, Mheshimiwa Kabudi ijikite zaidi kuangalia jinsi gani inatengeneza waandishi wazuri ambao watakuwa na weledi wa kutosha ili siku nyingine tutakapokuja tuwe na kazi ya kuelezea mazuri au upungufu wa kisheria na si ya kimuundo kama ambavyo tumekuwa tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Kamati yetu hatuna wataalamu wa kutunga sheria, hivyo Waziri kupitia ofisi yake anaweza kutusaidia kufanya kazi hii ya kuweka vizuri miundo ya kuangalia vizuri dosari zinazojitokeza ili tuendeleo kuwa wenye kufanya kazi ndogo ambayo imetuleta Bungeni. Bungeni hapa hatukuletwa kwa ajili ya kuangalia miundo tumeletwa kwa ajili ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, niendeleo kuishukuru Serikali katika kufanya kazi yake kubwa imeendelea kukamilisha miundombinu ya Mahakama. Pamoja na kazi nzuri ambayo imeendelea kufanywa hakuwezi kuwa na Mahakama kusipokuwa na nyumba na nyumba hiyo lazima watu wakutane ili haki ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zama hizo haki zilikuwa zinatolewa chini ya miti lakini katika dunia ya sasa Mahakama zetu zinahitaji majengo mazuri, teknolojia za kisasa pamoja na kuwa na miundombinu rafiki zaidi ili kusaidia ile shughuli ya kutoa haki iweze kufanyika. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ameendelea kulisimamia jambo hili lakini pia nimeona kupitia hotuba ya Kamati na taatifa mbalimbali za Wizara kwamba kuna Mahakama za Mwazo zaidi ya tano ambazo zimeshakamilika ikiwemo ile Mahakama ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watu wa Bagamoyo nitumie nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu watu wetu wakati mwingine walikuwa wakitamani wakae nje ya Mahakama kwa sababu ya kuogopa kuangukiwa na dari za majengo ya Mahakama hizo. Pamoja na hilo, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ameendelea kutoa mchango mkubwa sana katika tasnia ya sheria lakini pia kuonesha kwamba ni Profesa wa Sheria na kuendelea kusaidiana nao kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita Kamati yetu imeweza kuangalia na kutoa mapendekezo mbalimbali ya jinsi sheria zinavyoweza kukaa vizuri. Hata hivyo, bado upo upungufu ambao unaendelea kuonekana hasa katika sheria, kwa mfano, ile ya Baraza la Sanaa ambayo mapendekezo yake tumeyatoa na kupitia Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tulimpa taarifa. Binafsi nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa sababu alishafika mbele ya Kamati yetu na kueleza hatua ambazo zimeshachukuliwa na kwa kweli sisi kama Kamati tumeridhika. Namwomba Mheshimiwa Waziri aendeleo

kusimamia tasnia na wasanii wetu ili waendeleo kunufaika naye. Pamoja na hilo, yapo mapungufu ambayo tumeendelea kuyaeleza kama ya kiandishi na kimuundo ambayo yanatakiwa yawekwe sawa ili sheria ile iweze kuchukua nafasi ya utelelezaji na tusije tukapata mikwamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeelezwa jambo lingine juu ya kodi zetu kuwa si rafiki. Katika kitabu cha hotuba ya Wizara ya Sheria imeelezwa kwamba ipo baadhi ya migongano inayotokana na sheria ambazo zipo katika maeneo mengi, hasa katika sheria za vijijini kama zilivyoelezwa na Mheshimiwa Getere hapa, leo hii kuna baadhi ya vijiji ikionekana mtu amejenga nyumba ya bati basi kuna ushuru mkubwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri katika utaratibu ambao tumeshajipangia ni kwamba nchi hii kakuna mtu ambaye atatozwa kodi mara mbili. Ipo kodi tunayolipa tunapokwenda kununua mabati na *cement*, je, iweje leo hii tufike sehemu ya kulipa kodi nyingine ambazo ziko kinyume na utaratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si mwisho kwa umuhimu, ziko baadhi ya sheria ambazo zinahitaji sana marekebisho. Katika kitabu chetu cha hotuba ya Kamati ya Sheria Ndogo zimeelezwa na jinsi ambavyo zimeendelea kuonekana zinakinzana na sheria mama lakini pia zinakinzana na sheria nyingine zilizopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako.

MWENYEKITI: Baada ya mjadala.

Tunaendelea na Mheshimiwa Bobali, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Nitaongea kiungwana sana katika hoja zangu nitaziwasilisha na nakusudia kuzungumzia mambo mawili tu. Zanzibar ilipata uhuru tarehe 10 Disemba, 1963 lakini baada ya kupata Uhuru wananchi wa Zanzibar wakaona haitoshi...

T A A R I F A

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Anasema uongo.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Zanzibar ilipata Uhuru wake tarehe 12 Januari, 1964 na si kama inavyoelezwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali, taarifa hiyo.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Zanzibar ilipata Uhuru tarehe 10 Disemba, 1963 ikafanya Mapinduzi tarehe 12 Januari, 1964. Nazungumzia Uhuru, *independence and revolution are two different things. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mataifa ambayo wakati wanatawaliwa na Wakoloni walifanya mambo makubwa ya kuwaletea maendeleo ya kujenga barabara, miundombinu ya viwanja vya ndege kama vile South Africa na Angola lakini wananchi wa nchi hizo wakaona haitoshi kwa sababu hawakuwa huru. Kwa hiyo, kwa kuwa Mheshimiwa Profesa Kabudi yupo na yeye ni mtaalamu wa

historia na sheria anajua hili kwamba kitu kinachoitwa uhuru ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabudi wakati anafundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tulikuwa tunafuatilia sana hotuba zake nzuri, alikuwa anatufundisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulivyo pamoja na umuhimu wa Katiba Mpya. Mwenyezi Mungu amejalia sasa ndiyo umefungwa kengele, wewe ndiyo Waziri wa Katiba na Sheria wa nchi hii, ule mchakato wa Katiba Mpya umekwama wapi Mheshimiwa Profesa Kabudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa ma-*champion* wa nchi hii wa kuhakikisha kwamba nchi inapata uhuru ni wewe. Mheshimiwa Profesa Kabudi utaandika historia kubwa sana ikiwa yale uliyokuwa unayasema, unayapigania wakati uko nje na sasa wewe ndiyo Waziri wa Katiba na Sheria ukiweza kuyatekeleza utaacha historia kubwa sana kwenye nchi hii. Vinginevyo *the vice versa is true* kwamba kumbe ulichokuwa unakisema haukiamini kama utashindwa kutelekeleza ukitoka kwenye nafasi yako bila kuwa na Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo nilikuwa nataka niseme kwa sababu namuona Mheshimiwa Profesa Kabudi yupo hapa ili ajue kwamba ana dhima hiyo ya kuhakikisha nchi yetu inapata Katiba Mpya. (*Makofi*)

T A A R I F A

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa kabisa nasimama kumpa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Mbunge Hamidu Bobali kwamba Mheshimiwa Kabudi yeye ni Waziri wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hafanyi mambo kwa matakwa na utashi

wake. Nampa taarifa kwamba Chama cha Mapinduzi kipaumbele chake kwa sasa ni kujega Reli ya *Standard Gauge*, Bwawa la Umeme la *Stigler's Gorge*; na kuhakisha wafanyabiasha wadogo wadogo wananyakazi bila usumbufu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsate Mheshimiwa Bobali taarifa hiyo.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo kwa sababu siyo kila taarifa unaweza ukaijibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria, ukurasa wa 39 - 40 inazungumzia juu ya uwepo wa Mfuko wa Taifa wa Vijana ambao pia nimemsikia vizuri Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii akisema kwamba 2016/2017 ulitengewa shilingi bilioni 1 na 2017/2018 wakapewa shilingi bilioni 2. Mimi bado si muhenga, bado nipo kwenye kundi la vijana lakini Mfuko huu siujui. Mheshimiwa Mhagama hizi fedha mnapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati nayaunga mkono kwamba inatakiwa kwenda kufanya ufuatiliaji juu ya fedha za vijana zilipopelekwa. Nasema hivyo kwa sababu moja Mheshimiwa Mhagama, kuna Mfuko wa Uwezeshaji wa Rais na unajulikana na upo nchi nzima, hata ukija Lindi pale ofisi zao zipo. Huu Mfuko wa Vijana ulio chini ya Waziri Mkuu, mbona hatuufahamu?

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa

Mheshimiwa Bobali kwamba kama anahudhuria vizuri vikao vya Halmashauri taarifa za Mfuko huu zipo katika kila Halmashuri na katika Kamati tumeshapeleka taarifa ya migao ya fedha kwa ajili kusaidia vikundi vya vijana katika kila Halmashuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Bobali, ama aje ofisini apate taarifa za ziada, ama ashiriki vikao vya Halmashauri aulize atapewa taarifa zote za Mfuko huu. Si sahihi kusema kwamba Mfuko huu haujulikani, ni tofauti na ule wa asilimia 10 na huu mwingine pia. Kwa hiyo, tarifa zote zipo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bobali umekaribishwa ofisi kwa *Chief Whip*.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtoe wasiwasi, Halmashuri yetu ina Wabunge wawili, mimi na Mheshimiwa Nape. Wewe muulize tu, sijawahi kukosa kuhudhuria kikao chochote cha Baraza la Madiwani, hata vikao Kamati za Fedha, nikiwa Dodoma nawahi kwenda Lindi. Kwa hiyo, hatuna wasiwasi, tunahudhuria.

MWENYEKITI: Hata kipindi cha korosho?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Ndiyo, hata kipindi cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokisema ni kwamba ukifika Lindi leo ukimuuliza kijana Mfuko wa Uwezeshaji wa Rais unajulikana. Mimi sijaongea *from nowhere*, hiki ndicho kilichoandikwa na Kamati kwamba hizi fedha Kamati inaomba kwenda kuvifuatilia hivyo vikundi vilivyopewa fedha. Sasa mimi kuunga mkono hoja ya Kamati inakuwa kosa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema ni kwamba Kamati yenyewe wameweka wasiwasi kwamba kuna umuhimu wa kufuatilia. Mimi naunga mkono Mheshimiwa

Mchengerwa fuatilieni kwa sababu wanasema hapa kuna SACCOS zimekopeswa, mimi Mbunge kutoka...

T A A R I F A

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Bobali. Yeye amesema hajui hizi fedha ziko wapi sasa hivi anabadilisha anasema kwamba Kamati imeomba fedha hizi zikaangaliwe kule zilikopelekwa kama zimefika. Maana yake ni kwamba Kamati inakubali kwamba hizo fedha kule zimefika isipokuwa kinachosisitizwa na Kamati zifuatiliwe kuona kama zimefanya kazi iliyokusudiwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muungwana, nimelelewa kiungwana na naheshimu sana watu wote, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Musukuma ajiandae Mheshimiwa Salome.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa naunga mkono taarifa za Kamati zote mbili. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa uchapaji kazi na usimamizi wake wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya wanaotambua na kuthamini kazi anazofanya na Geita nadhani ni namba moja. Ukiangalia Geita ya leo na Geita ya mwaka mmoja tu uliopita kabla ya yeye kuamua kutekeleza sheria na kuisimamia ni vitu viwili tofauti. Wengine hata tukiona

wanavyomshambulia, tunaumia sana, lakini tunaomba aendelee kukaza buti kwa sababu msimamo wake ndiyo unaofanya hawa watu wapige kelele humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sisi tunaotoka vijijini tunaishukuru sana Serikali pamoja na Wizara. Mheshimiwa Kabudi, Mahakama inayotembea ni suluhisho kubwa sana kwa watu wa vijijini. Ukienda Jimbo la Geita Vijijini lenye watu takribani 600,000 lina Mahakama moja tu ya Mwanzo na yenyewe inapatikana pengine kilometa 150 ndiyo unaiona Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali. Ombi letu ni kwamba sasa Mheshimiwa Kabudi tumeona mmezindua juzi, tunatarajia baada ya muda mfupi, tutayaona haya magari yanakuja huko vijijini kuanza kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nilishauri Bunge lililopita kwamba makosa mengi, ukienda kwenye Magereza kuna mlundikano wa wafungwa na mahabusu lakini watu wengine wana makosa tu ya kuiba kuku. Watu wengine wana makosa ya kukamatwa uzururaji, hata faini yake pengine inakuwa shilingi 100,000/= lakini ameshakula ugali zaidi miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kabudi kwa uchapaji wake kazi hebu aangalie namna anavyoweza kufanya, makosa mengine tuwe tunamalizana nayo hata kwa viboko watu waendelee kuchapa kazi huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, sisi Wabunge ndio tunaotunga sheria. Pamoja na minyukano inayokuwa humu ndani, lakini sisi ndio tunaotunga sheria. Kwa hiyo, sheria inapotekelezwa, tusidhani tunapopitisha sheria, tunapitishia mbwa; tunapitishia binadamu tukiwemo na Wabunge. Kwa hiyo *sometimes* sheria inapotulenga sisi, lazima tukubali kutii sheria bila shuruti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia watu wengi wanasema; na bahati mbaya rafiki zetu wakizungumza, wanawahi *Canteen* hawamo humu ndani. Amezungumza Mheshimiwa Lema hapa, anasema alitekwa Makuyuni. Hivi mtu anatekwa halafu anapelekwa Kituo cha Polisi? Hicho ni kitu cha uhuni. Mimi mwenyewe nilikamatwa, siwezi kusema nilitekwa. Unakamatwa, unapelekwa Kituoni, unamaliza shida zako, unaachiwa. Ndiyo maana leo Mheshimiwa Lema yumo humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mwongozo wangu jana kwa Mheshimiwa Spika kuhusiana na suala la Mheshimiwa Tundu Lissu. Nimeona mitandaoni wananitukana, wananichamba, lakini sishangai. Bahati nzuri wengine tunaongea nao huko. Hili suala nililolizungumza jana kuna watu wanalifurahia kwa sababu michango inawaua na hawana kitu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nizungumze, katika Bunge hili hakuna mtu ambaye hatarajii kuugua; hata sisi, hata yeyote. Tunatambua kabisa kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu alipata matatizo. Wengine tunaomba kimya kimya, siyo lazima wote tupayuke kama nyie. Tumekuja kushtuka, mtu tunayemwombea ni mcheza sinema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi toka nimekuwa Bungeni hapa, hatujawahi kukaa Bungeni zaidi ya masaa matano *tuna-break*, tunarudi masaa matano, tunaahirisha Bunge. Naomba niwaambie kwa sababu tunazunguka zunguka na sisi ni wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua kutoka alikokuwa anatibiwa Mheshimiwa Tundu Lissu, ziara yake ya kwanza ameenda Uingereza. Kutoka Ubelgiji kwenda Uingereza ni masaa manne kwenye Ndege. Huyu ni mgonjwa. Kutoka Uingereza kwenda Marekani ni masaa 10 mpaka 11, huyu ni mgonjwa. Haya, kutoka Marekani kwenda Ujerumani, ni zaidi ya masaa 14, huyu mtu anaitwa

mgonjwa, haiwezekani. Hili lazima tuungane mkono. Nanyi mnaomtetea, nataka niwaambie ukweli, pamoja na

T A A R I F A

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia data zako za kutoka hapa na pale. Hivi kutoka Kenya mpaka Ubelgiji ni masaa mangapi? Mheshimiwa Lissu alikuwa haumwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilichokuwa nakisema; na wenzangu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Singida Mashariki walichagua Mbunge na wao ni wamoja wa watu ambao wanamwomba Mbunge wao apone, hawakuchagua mtu wa kula bata, wanayemwona kwenye TV na magazeti kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokisema hapa, sheria tulizitunga wenyewe. Nashangaa sana na Bunge lako, kwa nini hatutekelezi matakwa ya kanuni? Kama mtu amepona anaweza kusafiri masaa yote na kukaa kwenye hotuba kutukana Taifa...

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Musukuma pale, ajue kabisa kwamba jinsi ambavyo Mheshimiwa Tundu Lissu amezungumzwa ndani ya Bunge hili, ndivyo dunia nzima wanavyomzungumza. Kwa hiyo, aendelee kumzungumza tu, ni mtu maarufu sana katika dunia nii. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, endelea.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ndugu yangu Mheshimiwa Mwakajoka, najua wewe Timu Tundu Lissu, unadhani anakuona ili akupitishie jina. Ninakuomba utulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, wananchi wa Singida Mashariki hawana mwakilishi; na sheria inatutaka mtu akiwa mzima, asipohudhuria vikao vitatu, kuna hatua ya kuchukua na mliitunga wenyewe, inasubiri kutekelezwa wakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wasichukue *point* hapa. Humu humu ndani tunao Wabunge wenzetu wanaumwa, wala hamna mtu anawajadili. Tunaye Mheshimiwa Mkono...

TAARIFA

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Musukuma kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu sio mtu maarufu, ila ni dalali wa rasilimali za Tanzania na utu wa Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachokisema hapa, ni vizuri Mheshimiwa Spika akachukua hatua ya kuweza kutengua uteuzi wake ili wananchi wa Singida Mashariki waweze kupata mwakilishi wasiwe na mwakilishi anayewawakilisha kwenye TV.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, tunao watu wanaumwa hapa, lakini kwa sababu wananchi wao wamewatuma kufanya kazi, tunaye Mbunge wa Singida Magharibi hapa Manyoni, ni mgonjwa, anakuja na gongo lake humu ndani; tunaye Mheshimiwa Ridhiwani, tunao watu kibao. Hhaiwezekani mtu anayeweza kukaa kwenye ndege masaa 14 halafu akaachwa tukaendelea kumwona anakula mshanara. Watanzania wanatupima na wanatuona.

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa Musukuma, ahsante. Mheshimiwa Salome, jiandae Mheshimiwa Mlinga.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba hizi mbili za Katiba na Sheria na Kamati yangu ya Sheria ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo napenda kuongea mambo machache. Kwanza, napenda kuongelea misingi miwili ya Utawala Bora katika nchi yoyote inayoendeshwa Kidemokrasia. Misingi miwili nitakayoiongelea, wa kwanza ni mgawanyo wa madaraka, kwa maana ya *separation of power* na wa pili ni uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote inayotambua misingi hii miwili ya Utawala Bora, ni lazima, siyo tu itekeleza

misingi hii, lakini pia ionekane kwamba inatekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, hasa kwenye upande wa mgawanyo wa madaraka, Tanzania katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, tunayomihili mitatu, kwa maana ya Mahakama, Serikali na Bunge. Juzi tulikuwa na Siku Maalum ya Sheria hapa Tanzania. Katika siku hiyo Maalum, iliyofanyika karibu nchi nzima, kitu kinachotarajiwa kwenye siku ile, viongozi wa *Judiciary* wanategemewa kuitumia siku hiyo kama siku maalum kujadili changamoto na namna bora ya uendeshaji wa Mahakama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho nilikishuhudia kinaendelea, ni namna ambavyo *Judiciary* wanawapa nafasi watu wa *Executive* (Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa) kwenda kutangaza yale ambayo wanayafanya kwenye Serikali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko *forum* mbalimbali ambazo tunaweza kuzitumia kutangaza haya tunayotangaza, lakini siku ya Wanasheria Duniani Watanzania wangependa kusikia ni namna gani *Judiciary* wamejielekeza kupunguza mlundikano wa kesi zisizokwisha Mahakamani, ni namna gani wanapunguza mahabusu waliolundikana Magerezani, ni namna gani wanaongeza Mahakama, ni namna gani wanaongeza Mahakimu na Majaji, katika nchi hii, ili siyo tu haki itendeke, bali ionekane imetendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaona Majaji na ilitokea Iringa kule, picha moja inazunguka kwenye mitandao. Jaji na Mkuu wa Mkoa, Jaji ki-*hierarchy* ni mtu mkubwa sana. Sijui kama wamejawa na hofu, sielewi. Jaji anatembea pembeni, kwenye *Red Carpet* anatembea Mkuu wa Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali itekeleze mambo yake ya *Executive* na iache mhimili wa

Mahakama uweze kufanya kazi kwa uhuru, ufanye kazi kwa weledi na utashi. Kwa sababu pamoja na kuhubiri maeneo mbalimbali kwamba haki inatendeka, haipaswi...

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia hivi sasa. Majaji ama Mahakama, Siku yao ya Sheria siyo siku ya kwenda kueleza changamoto ama mafanikio. Wanao utaratibu wa siku hiyo. Wewe kama una changamoto, Mbunge sasa unaweza ukaja na hoja binafsi ama jambo lolote ambalo linakukera ukalileta Bungeni kama swali, kama hoja binafsi, ama...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi, hoja wala haikuwa hiyo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niishauri Serikali, iliwekwa misingi ya Utawala Bora, iliwekwa misingi ya Uwajibikaji, yote hiyo ni kutoa sintofahamu na kutoa ombwe kubwa ambalo lilikuwepo la kuonekana mihimili hii inaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa wale wanaosoma, Wanazuoni, huu mjadala ni mkubwa sana. Nawaomba sana, Serikali, Mahakama na Bunge, kuepusha maneno yanayojitokeza ya kuonyesha kwamba mihimili hii inatawaliwa na mhimili wa *Executive*. Hebu tuoneshe kwa vitendo kwamba tunaweza kujisimamia, kwamba tunaweza kutekeleza wajibu wetu kwa mujibu wa Katiba na Sheria na Katiba inatulinda kufanya hivyo.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Naibu Waziri wa Utawala Bora.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(1) kumpa taarifa mdogo wangu anayeongea kwamba nchi hii tangu tupate uhuru, inaongozwa kwa misingi ya utawala bora na haijawahi kuingiliwa katika mihimili hiyo mitatu. Naomba tunapozungumza humu ndani tuheshimu mamlaka kwa sababu hata Biblia inasema tutii walio kwenye mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye hoja ya pili kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi, ni lazima kila mtu awajibike kwenye eneo lake. Leo Mheshimiwa Selasini ameeleza vizuri kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Waziri wakati anajaribu kujibu, anasema jambo hili linafanyika kwa uwazi. Sisi ni Wabunge, ni Wawakilishi wa Wananchi, tunasimama hapa kutoa maoni na mapendekezo yetu ya namna bora ya kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nafikiri Mawaziri wangetumia fursa hii kusikiliza maoni yetu, kuyasimamia, kuyatekeleza kwa mustakabali wa Taifa hili kuliko kusimama kuwa *defensive*, kwa sababu haimsaidia mtu yoyote.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Chaguzi kwenye nchi hii ni moja kati ya kitu ambacho kinaweza kutuletea matatizo

ambayo yanaweza kuvunja amani. Tusipoandaa uchaguzi huu kwa kufuata taratibu za ushirikishwaji wa wadau...

T A A R I F A

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: *Yah, I know the lady is nice and very bright lady I know.* Ni mmojawapo wa akina dada wenye weledi sana.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba anazungumzia suala la uchaguzi huru, lakini nilitamani kumpa taarifa. Mpaka leo na nilipotoka huko sijajua ni utaratibu gani ulitumika kupata Viti Maalum, CHADEMA, lakini mpaka leo nilivyotoka huko sijui kuna Chama kiko huko, kuna mtu mwenye...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mollel. Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sisi Wabunge, moja kati ya jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunaisaidia nchi hii kuwapa uelewa mzuri wa yale tunayoyatunga humu ndani wananchi wetu, kuwasaidia kuwafikishia taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakuja kukutana hapa Bungeni tena mwezi wa Nne, tukitoka hapa ni mwezi wa Saba. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aweke uwazi wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili tunapotoka hapa, moja kati ya majukumu yetu iwe ni kwenda kuwaelimisha wananchi na kuwapa taarifa juu ya

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, anasema hiyo kazi inafanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndicho kinachofanya leo na kesho sisi Wabunge tutukanwe na kuonekana hatuna maana. Tunatoa ushauri, Serikali inaelewa kuliko sisi tunaowakilisha wananchi. Mwisho wa siku, ndiyo kauli zinapozuka mtaani, unazisikia zile; kama ile aliyosema CAG, sijui ameshaomba radhi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza. Moja kati ya kitu Mheshimiwa Rais alisema, ni lazima tufute tozo za kero kwa wananchi kwa sababu zinapunguza ufanisi na zinazuia wananchi kufanya shughuli za maendeleo. Juzi Mheshimiwa Rais ameanzisha kitu kinaitwa Vitambulisho kwa Wajasiriamali.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Sixtus, ataendelea Mheshimiwa Mliga.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia majukumu au kazi za Kamati hizi mbili zilizoko mbele yetu. Awali ya yote, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa jinsi walivyotuwasilishia kwa ufasaha sana kazi zao; lakini pili, kutuelezea changamoto na namna bora ya kuondokana na zile changamoto ili Bunge lako Tukufu lipate fursa nzuri ya kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mnajili wa kuchangia hoja yangu ya leo, itoshe tu kuongea mambo mawili ambayo yanatokana na mjadala wetu wa leo; lakini vile vile katika kuwekana sawa ili kama kuna jambo linapotosha humu ndani, wote tulielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mijadala imeendelea huku ndani ikielezea *separation of power, good governance*, uhuru wa hii mihimili mitatu na majukumu ya hii mihimili mitatu. Sisi kama Bunge tunapata fursa ya kufanya kazi zetu kwa Ibara ya 62, 63 na kuendelea ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema mgawanyo wa kimajukumu wa hii mihimili mitatu, kama msemaji aliyepita, Mheshimiwa Salome Makamba aliposema *separations of power* halafu akaiacha hewani; *separation of power* haimaanishi hii mihimili mitatu ifanye kazi kwa kujitegemea, ndiyo maana kuna kitu kinaongezeka. *Separation of power, checks and balance* ikimaanisha, *the three pillars should work independently*, lakini katika kufanya kazi kule pamoja, inategemeana. Ndiyo maana kunakuwa na *checks and balance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kidogo kwa manufaa ya watu ambao hawakuwahi kumsoma *Montesquieu* na Jean-Jacques Rousseau hebu tuwasaidie kidogo waweze kujua. Huu msingi wa *separation of power*, unatokana na maandikio aliyowahi kuyaandika *Baron De Montesquieu*, huyu ni mwanafalsafa wa Kifaransa kwenye kitabu chake cha *The Spirit of Law* cha mwaka 1748. Katika kuelezea alisema tunapaswa kuwa na mfumo ambao kila *organ* inajitegemea ili kuepusha *fusions of power* kwenda kwa *entity* moja. Maana yake alikuwa anapinga kipindi kile mifumo ya *aristocracy*, alikuwa anapinga mifumo ya *ki-monarchy*, alikuwa anapinga mifumo ya *autocracy*. Sasa katika kuweka hivi ndio sisi hapa tunakuwa tunatunga sheria, sasa nikamshangaa sana ukiunganisha hoja ya Mheshimiwa Salome na ya Mheshimiwa Kubenea zinakuja kukutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea anasema sisi tutunge sheria, tukishatunga sheria, hatuwezi tena sisi tukatafsiri sheria, hatuwezi sisi tena tuka-*enforce law*. Tuna maeneo yetu sisi lazima tuishie, ndio maana kuna msemu wa Kilatini unaosimamia hilo unasema *trias politica principle* ukimaanisha *(The separation of power, checks*

and balances). Hii mifumo lazima ifanye kazi kwa kutegemeana, huwezi ukawa na Mahakama isiyokuwa na aliyeanzisha shtaka yaani *Executive* katika maana ya Polisi. Huwezi ukawa na mtafsiri wa sheria bila kuwa na mtu aliyetunga sheria. Hawa watu wote wanafanya kazi kwa kushirikiana. Kikubwa zaidi kinachonishangaza, sikutegemea kama hii ingekuwa kweli ajenda ya kujadiliwa kwenye nyumba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Wanasheria. Mwanasheria amemwalika Polisi, Mwanasheria kwa hiari yake mwenyewe ameamua kumwalika mgeni rasmi awe Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya au mtu mwingine yeyote, tatizo liko wapi? Hivi kweli ukiweka *red carpet* pale ukawaweka Majaji, ukamweka na Mkuu wa Mkoa, maana yake kweli Mkuu wa Mkoa ni mkubwa kuliko Jaji au Jaji Mkuu kuliko Mkuu wa Mkoa? Ile ni *context*, ile ni shughuli kama shughuli nyingine ina taratibu zake haiingilii mamlaka ya Jaji kama Jaji na wala haiingilii mamlaka ya Mkuu wa Mkoa kama Mkuu wa Mkoa.

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata kwenye harusi, bibi harusi ndio huwa anapita kwenye *carpet* nyekundu na wazazi wanapita pembeni sasa sijui mkubwa ni mzazi au bibi harusi.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa...

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kusema hapa kwa kuanza hii mifano ya nyuma, hii mihimili mitatu inafanya kazi kwa kutegemeana sana. Bunge lako tukufu lisiwe sehemu ya kufarakanisha kwa

kuweka chuki, nani mkubwa, nani mdogo, hoja ambazo hazitusaidii, ni vyema tujielekeze kwenye kuifanya hii mihimili ifanye kazi zake ufasaha, Wenyeviti wa Kamati wameelezea hapa changamoto zao, tuwasaidie kwenye kutatua changamoto ili kazi zao ziwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba niongee kidogo kwenye *mobile court*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Mheshimiwa Kubenea ni Mjumbe mwenzangu, wote tulikuwa kwenye kikao, sielewi amefanya kwa makusudi kwa kutaka kupotosha au hajui maana ya *mobile court*. Ukisoma Ripoti ya UNDP kuhusu Mahakama zinazotembea, ripoti iliyofanyia kazi Sierra Leone, Democratic Republic of Congo na Somalia inaeleza *mobile court* au Kiswahili (Mahakama inayotembea). *Mobile Courts are defined as the formal courts that conduct proceedings in location other than their home Offices, usually in remote areas where no justice service are available.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa anachotaka kuongelea ni kwamba, *mobile courts* si lile gari, *mobile court* ni kwamba zile huduma zinatoka Mahakamani tulivyo zoea kuziona, zinaenda sehemu nyingine, zinaweza zikawa kwenye bajaji, zikawafikisha Mahakimu na timu wakafanya kazi zao kule au wakatamia mfumo mwingine wowote wa kufika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka *scenario* kama hii iliwahi kutokea kipindi cha *genocide* Rwanda, walikuwa na *court* zao zilikuwa zinaitwa *Gacaca* ambao watu walikuwa wanatoka wanakwenda maeneo ambapo watu hawajapata huduma na kwa sababu Mahakama zilikuwa zina msongamano sana wa watu na *cell* zilikuwa zimejaa, wakalazimika kutafuta *mechanism* ya kutatua matatizo. *Mobile courts* labda kwa lugha tunaweza tu tukasema, kuna hizi *mobile banks* mnazona eeh, au *mobile clinic* haimaanishi kuwa lile gari, unaweza ukatumia chombo chochote...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, kengele ya pili, Mheshimiwa Mlinga.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kidogo nataka nianze kwa historia. Katika ukuaji wa lugha matendo huzaa nomino. Enzi hizo wakati mimi niko mdogo kulikuwa kuna Mwanamuziki mmoja anaitwa Mbaraka Mwishehe na mwingine alikuwa anaitwa Juma Kilaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Juma Kilaza alikuwa ni mtu mwenye majigambo sana, yaani yeye kila kitu anajua, anajifanya anajua kuimba muziki. Sasa wakasema tukate mzizi wa fitna, wakaweka pambano. Baada ya kuweka pambano la muziki, Mbaraka Mwishehe akaonesha shamra shamra zake, Juma Kilaza akaonyesha udhaifu wake. Kuanzia siku hiyo, mtu yeyote ambaye alikuwa hajui akawa anaitwa Kilaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo miaka ya nyuma wakati niko mdogo Ubunge Jimbo la Temeke kuna mtu mmoja Lamwai na mwingine alikuwa anaitwa Kihyo. Wakagombea, baada ya kugombea Mheshimiwa Kihyo aliweka vyeti feki, Lamwai akaenda Mahakamani kuweka pingamizi. Baada ya kuthibitisha yule mtu kuwa vile vyeti alifoji akang'olewa Ubunge, kwa hiyo tangu siku hiyo mtu ambaye hajasoma alikuwa anaitwa Kihyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudi sasa hivi. Rais wa TFF juzi alisema kwa sababu katika nchi ameshaonekana mtu mbishi sana ambaye anajifanya anajua sana lakini hajui, hakubali chochote, akatoa mfano wa Mheshimiwa Tundu Lissu akasema kuwa msilete Utundulisu kwa sababu ya matendo yake huo ndio ukuaji wa lugha haizuiliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa, jana ilizuka mijadala miwili humu ndani, mwisho alimalizia Mheshimiwa Joseph Selasini kwa kuomba Mheshimiwa Rais aingilie kati suala la Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Ester Matiko. Nataka nimwambie Rais wangu mimi bado kijana mdogo sana, asije akaingia kwenye huu mtego hata wakimfuata kwa kuburuza magoti. CHADEMA ndio wamekuwa wakizunguka dunia nzima kusema Rais hafuati Katiba..

T A A R I F A

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Hansard* yako ya jana isomwe, nataka nimpe taarifa sijawahi mimi kusimama katika Bunge hili kumwomba Mheshimiwa Rais aingilie kati suala la Mheshimiwa Mbowe na Matiko. Kwa hiyo, naomba mzungumzaji aweke kumbukumbu zake sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga futa jina la Selasini, endelea.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kujua kama wanawajali au hawawajali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitamkwa humu Bungeni, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Rais hawa ndio wanaozunguka dunia nzima... (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga wewe sema tu nafuta jina la Mheshimiwa Selasini ili tuendelee.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Basi ili aridhike nalifuta hilo jina la Mheshimiwa Selasini, lakini *message* imefika. Kwa hiyo

namuomba Mheshimiwa Rais aje akaingia kwenye huo mtego, kwa sababu hawa ndio wanazunguka dunia nzima kusema Rais wetu hafuati Katiba, hafuati sheria, hafuati kanuni za nchi hii, hafuati taratibu, yeye ni dikteta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nataka nizungumze kuna kitu sasa hivi watu wanazunguka duniani wanasema Tanzania hakuna *freedom of expression*. Wote ni shahidi, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye vyombo vingi vya habari katika Bara la Afrika. Tanzania ina magazeti 216 yakiwemo ya CHADEMA. Nchi yetu ina Redio 158, nchi yetu ina TV 34 na hazijawekewa mazui ya kuandika. Tuna *Online TV* 224, tuna *blogs* zaidi ya 60. Hivi vyote vinafanya kazi bila ya kufuatiliwa. Kwa kuthibitisha hilo tuambiwe ni Mwandishi wa Habari gani sasa hivi yuko jela, kama hakuna *freedom of expression*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchora katuni mmoja anaitwa Masoud, kwa katuni anazomchora Mheshimiwa Rais, ningekuwa mimi nisingemwacha, lakini yote haya yameruhusiwa watu wanafanya lakini watu wengine wanazunguka dunia nzima wanasema Tanzania hakuna *freedom of expression*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi anayoitolea mfano, kwa mfano mwenzetu mmoja yuko Marekani, hiyo nchi ya Marekani kuna uhuru lakini wanaweka mipaka, hata hiyo *freedom of expression*. Marekani *freedom of expression* ipo lakini usije ukaongopa, usije ukadhalilisha mtu, usije ukamsingizia mtu kitu, usije ukavuruga usalama wa nchi na kwa kuthibisha hilo kuna mtu mmoja anaitwa Edward Snowden, waulize kwa nini Marekani wanamtafuta yule pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa upande wa Mahakama. Najiuliza Mahakimu wanafanya kazi kubwa kwelikweli, wanafanya maamuzi magumu, hivi kwa nini Hakimu hapewi ulinzi, *OCD* anapewa ulinzi. *OCD* ambaye kazi yake kukamata tu mtu, lakini Hakimu kazi yake kumuhumu mtu aozee jela au anyongwe, kwa nini hapewi

ulinzi. Naomba Mahakimuwapewe ulinzi kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, leo kumezuka mjadala wa mwisho humu. Watu wanataka wafungwa waruhusiwe kufanya matendo ya ndoa na wake zao. Wafungwa wana haki nyingi sana na ndio maana wameitwa wafungwa. Lakini sasa tukianza kuwawekea huru, maana yake tendo la ndoa ndio tendo zito kuliko yote duniani.

Mheshimwa Mwenyekiti, wanaume sisi tunakuwa majambazi, tunaenda kuiba hela tunapokea rushwa ili tufanikiwe kupata hilo tendo kirahisi. Leo hii mfungwa ambaye amefungiwa gerezani anaambiwa aruhusiwe kufanya tendo la ndoa na mke wake au na mume wake. Hilo suala halikubaliki sisi ndio tutakuwa wa kwanza katika nchi zenye demokrasia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara dakika saba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Jiandae Mheshimiwa Antony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naunga mkono hoja Kamati zote mbili, Kamati ya Sheria Ndogo ambayo inaongozwa na Mtemi Chenge na Kamati ya Sheria ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Mchengerwa. Kuna hoja zimejitokeza hapa zinazohusiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni ile ambayo Waheshimiwa wa Kamati ya Sheria Ndogo wamepitia na kweli kwamba kulikuwa na upungufu katika Halmashauri zetu umetajwa, sina sababu ya kuutaja hapa. Tunaomba tuseme kwamba tumepokea maoni yenu na mapendekezo yenu tutayafanyia kazi na kuboresha ili sheria ndogo kwenye Halmashauri zetu ziendane sawasawa na sheria mama pamoja na matumizi bora ya kuboresha utawala bora katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hili jambo bado lipo kwenye mchakato hatujachelewa. Kwa kawaida mambo ya kisheria na Wanasheria wanafahamu, Mheshimiwa Salome Makamba alikuwa anachangia hapa, ni kwamba jambo hili limeanza mchakato wa kuangalia uchaguzi uliopita, upungufu ambao ulijitokeza, malalamiko yaliyotolewa na wananchi na wagombea waliokuwa wanagombea nafasi mbalimbali, wakiwemo wagombea wa Uenyekiti wa Mtaa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yamepokelewa na wataalam wetu katika Ofisi ya TAMISEMI yatarudishwa kwenye Halmashauri zetu, yatakuja kwenye vyama vya siasa, tutapokea maoni, kwa hiyo jambo hili mtashirikishwa vizuri. Tumeanza kufanyia maboresho maoni ya 2014 ambayo pia watu walitoa. Kwa hiyo ni jambo ambalo bado liko kwenye mikono salama, naomba mwendeele kutupa imani yenu, tutatoa ushirikiano hakuna tatizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu. Tumezungumza kodi ya majengo, hili jambo ni kweli wakati yametolewa maeneo ya kukusanya kodi ya majengo, yamekuja maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani na Halmashauri na wadau mbalimbali na wananchi wenyewe na hasa wafanyabiashara ambao kimsingi wanalipa kodi kwa Watanzania jambo limechukuliwa na Serikali ambayo ni sikivu ya Chama cha Mapinduzi, limefanyika kwenye

mchakato, yatakuja maboresho humu na Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kutoa maoni yenu ili tufanye maboresho ya namna bora ya kusimamia kodi ya majengo bila kuleta kero na malalamiko kwa wananchi wetu. Hili jambo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo limezungumzwa hapa, kuna Mbunge mmoja amezungumza anasema kuna mjumbe wa *NEC* alikuwa anasemwa huko mtaani kwamba sijui nilikwenda kwenye Mkutano fulani nikitaka watu wampinge Tundu Lissu. Naomba niseme kwamba, Tundu Lissu mke wake ni Mkurya anaitwa Robi, ameoia Nyarero pale nyumbani, kwa hiyo ni shemeji yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili, nataka niseme msimamo wangu ni kwamba, Tundu Lissu ana maumivu, alipatwa na tatizo na watu wote walimpa pole na sio kumwambia hadharani, lakini sasa baada ya kupata madhara hayo amegeuza machungu yake yawe machungu ya Watanzania, hatuwezi kukubali. Machungu ya mtu mmoja, hayawezi kugeuzwa machungu ya Taifa. Savimbi sio lazima awe na mandevu, unaweza ukawa Savimbi kwa matendo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayofanyika duniani. Huyu ni Mtanzania, angerudi hapa Tanzania aeleze machungu yake, maumivu yake, tumsikilize, tumsaidie kulia. Ameamua kwenda ughaibuni, anamtukana Rais wa nchi, anasema Rais wetu ambaye ni Daktari, ni msomi wa hesabu kama mimi, wa hesabu na kemia, eti Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli hawezi kutunga hata sentensi moja ya Kiingereza, sio kweli *this is very unfair*, hizo haki mnazozungumza sijui mnatoa wapi? Hamwezi kuwa na haki ya kusema muonewe wenyewe huruma lakini haki ya kutukana wenzenu, kuwadhalilisha watu wazima na familia zao, hilo halikubaliki na haliwezi kuungwa mkono, ni *very unfair*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika maelezo anasema, anapaka matope Taifa ili Serikali

ianguke, amesema wakati anahojiwa *Ai...International Study of Africa*, nimemsikiliza, anasema yeye anapaka matope Taifa ili akirudi hapa asikilizwe, apate uongozi na Serikali ianguke, huyu atakuwa ni mhaini, anataka kuiangusha Serikali, anaipaka matope Tanzania, misaada ambayo inakuja hapa, Watanzania wa Singida, watu wa Mara, Wagogo, makabila yote, wanawake, wazee na vijana wananufaika, leo mnazungumza habari ya maji hapa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio mambo ambayo hatuwezi kuyakubali yakafanyike. Tumeshasema kama kuna mtu ameonewa katika Taifa aseme, tutasimama upande wake kumtetea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): ...lakini sio anageuza mambo yake binafsi, mtu ambaye anatetea tumbo lake...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): ...halafu anageuza tena tuzungumze kama ya Taifa, haiwezekani...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Kwa

mambo ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu anayafanya Watanzania wasimame na watambue...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, kaa chini.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Watambue wazalendo ni wapi, wanafiki ni wapi, wasaliti ni wapi. Tanzania ni ya kwetu, una jambo lako rudi Tanzania, tukae pamoja, tujadiliane, tupange mipango yetu, uongozi wa nchi hii utatolewa na Watanzania, uongozi wa nchi hii hutakabidhiwa Ulaya, tutakupa sisi Watanzania kwa muda tutakaotaka. *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Antony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja za Kamati zote mbili. Pia nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati zote mbili.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Kamati tunapochangia hapa Mawaziri wanachangia kama Wabunge hawachangii kama Mawaziri, sasa unaponyima hoja ya kutoa mwongozo haututendei haki kwa sababu hapa sio kama Mawaziri, ni kama Wabunge nao kuisaidia Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kaa chini, Mheshimiwa Mavunde endelea. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja kama ambavyo zimewasilishwa na Kamati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Kabudi ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na eneo la kwanza ambalo limegusiwa na wachangiaji ikiwemo mapendekezo ya Kamati, imezungumzwa hoja ya kuhusu uanzishwaji wa Baraza la Watu wenye Ulemavu na litangazwe mapema.

Ni kweli kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 inayozungumzia watu wenye ulemavu, imeweka bayana kwamba kutakuwepo kuna Baraza la Watu wenye Ulemavu. Hivi sasa navyozungumzia tayari Serikali imeshakamilisha zoezi la kutoa mapendekezo la kumpata Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Taifa la Watu wenye Ulemavu. Kwa hiyo, muda sio mrefu uteuzi huu utafanyika na litazinduliwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia imezungumzwa hoja ya kwamba kuanzishwe kifungu maalumu kwa maana ya kasma ya masuala ya watu wenye ulemavu. Wizara tayari imeshafanyia kazi eneo hili na kifungu hiki kimepatikana. Kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 kifungu hiki kitaonekana na kitatengewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imezungumzwa hoja ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu. Kama Wizara, kwa maana Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeshandaa rasimu ya mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu na tumeshawashirikisha wadau, tumefanya kikao cha Dar es Salaam na eneo hili, Mheshimiwa Ikupa analisimamia kwa ukamilifu sana. Kwa hiyo, muda siyo mrefu baada ya sehemu hii kukamilika basi tutaona namna bora ya uanzishwaji wa Mfuko huu wa Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilizungumzwa hoja ya kuweka usimamizi mzuri wa fedha kwa ajili ya watu wenye ulemavu kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatengwa na Halmashauri. Ni dhahiri kwamba Serikali imeelekeza kila Halmashauri nchini kutenga asilimia 2 ya mapato yake ya ndani ili kuwawezesha watu wenye ulemavu. Katika eneo hili pia, tumeandaa rasimu ya mwongozo mzuri wa utoaji wa fedha hizi za asilimia 2 kwa watu wenye ulemavu ili ziweze kuwafikia kirahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilizungumzwa hoja ya namna ya kuwashirikisha watu wenye ulemavu kwenye shughuli za michezo. Niseme tu kwamba kama Wizara tumekuwa tukifanya hivyo pale yanapotokea maombi. Mwaka 2009 tuliwahi kuisaidia Timu ya Watu wenye Ulemavu wa Akili ambao walikwenda katika Bara la Asia kushiriki mashindano ya mpira wa miguu na mbio. Halikadhalika kwa sababu BASATA na Baraza la Michezo Tanzania ziko chini ya Wizara, tutahakikisha kwamba tunafanya ushirikiano wa kutosha ili kundi hili pia liweze kuangaliwa katika masuala ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa pia hoja kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Eneo hili limezungumziwa sana na moja kati jambo ambalo limezungumzwa ni usimamizi na udhibiti ili kuhakikisha kwamba fedha za mfuko huu zinawafikia walengwa ambao ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote ambazo zinadaiwa fedha ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo vijana wamekopa na fedha hizi zinatakiwa zirudishwe, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeanza kuchukua hatua kuzifuatilia fedha hizi ili ziweze kurudishwa. Wale ambao tumeshawapa taarifa ya kurejesha fedha hizi bado hawajafanya kwa wakati, taratibu za kisheria zitachukuliwa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarudi ili vijana wengi zaidi waweze kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu, fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Vijana zimelengwa kwa ajili ya vikundi vya vijana ambapo utaratibu wake ni kwamba kila Halmashauri nchi nzima inaandaa SACCOS ya vijana yenyewe ndiyo inayokopa kupitia Halmashauri na ndiyo inayokwenda kukopesha vikundi vya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja ya Mheshimiwa Bobali, kwa kweli nimeshindwa kuelewa vizuri Mheshimiwa Bobali na nilitamani angekuwepo hapa Mbunge mwenzangu kijana kabisa anasema kwamba haujui Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na vijana wake hawajanufaika. Nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Bobali kwamba mwaka 2016 nilikwenda mwenyewe katika Wilaya ya Lindi Vijijini ambako nilikuwa na Programu ya Kuwawezesha Vijana Kiuchumi. Katika programu ile walikuwepo vijana 683 wakitoka katika majimbo mawili, la Mchinga na Mtama na Mheshimiwa Nape alikuwepo Mheshimiwa Bobali hakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hilo vijana hawa waliwezesha kiuchumi lakini pia baada ya kuhitimu mafunzo yao ya kuwezesha kiuchumi tulitenga utaratibu mzuri wa kuwakopesha kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Ninavyozungumza hivi sana, kwenye Wilaya ambayo anatoka Mheshimiwa Bobali, tumeshakopesha vikundi na moja ya kikundi ambacho kimekopeshwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni kikundi ambacho kinaitwa Juhudi kilichokopa Sh.3,500,000 na kingine kinaitwa Kitongamano walikopa Sh.6,000,000 na kikundi cha Mshikamano. Nikimsikia Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba haujui mfuko huu na vijana wake hawajanufaika jambo hili si la kweli, mfuko huu unawafikia vijana wengi nchi nzima na vijana wengi wamenufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yalikuja mapendekezo hapa ya kutaka kuwe na namna bora ya mfuko huu kuwafikia watu nje ya mfumo wa SACCOS. Sheria ya kuratibu mfuko huu ilitungwa mwaka 1994. Sisi kama Wizara tukaona ni miaka mingi imepita, kwa sababu masharti ya mwongozo

wa mfuko huu inataka SACCOS ndiyo ikopeshwe, tumeenda mbali zaidi, hivi sasa tumeanza kupitia mwongozo wetu ili baadaye kuruhusu vikundi vya vijana kwa maana ya makampuni na vikundi tofauti tofauti, nje ya SACCOS na wenyewe waweze kukopa. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba mfuko huu utawafikia vijana wengi zaidi na wengi watakopa kwa ajili ya kupata fursa hii ya kiuwezesaji kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Ofisi ya Waziri Mkuu tunaendesha Programun ya Ukuzaji Ujuzi Nchini ambayo ina lengo la kuwafikia vijana takribani...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Kabudi. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Sheria Ndogo kwa taarifa nzuri ambazo wameziwasilisha mbele ya Bunge hili. Mengi ambayo wameyaainisha katika ripoti zao kama mapendekezo tutayafanya kazi ili kuboresha huduma zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tuna bahati kubwa sana ya kuzaliwa katika nchi hii ya Tanzania na katika mfumo ambao unatoa haki na uhuru kwa watu kuliko nchi nyingi nyingine. Watanzania tuna uhuru, tuna haki ambazo zinalindwa na Katiba lakini viko pia viko vyombo vingi ambavyo vimeundwa kuhakikisha kuwa haki hizo ambazo ziko ndani ya Katiba zinaheshimiwa au zinafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni miongoni mwa nchi chache sana katika Bara la Afrika ambazo hazifiki nne, ambazo zimewaruhusu raia wake kuweza kuishtaki Serikali katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Hivi tunapozungumza sasa katika Mahakama hiyo yako mashauri 113 ambayo yamepelekwa na Watanzania dhidi

ya Serikali. Nchi moja ya jirani baada ya kufanyiwa hivyo imejiondoa katika Mahakama hiyo. Tunavyozungumza leo asilimia 75 ya mashauri yote katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu yanatoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Watanzania sasa wana haki na wameitumia haki hiyo kwenda kufungua mashtaka dhidi ya Serikali kwa madai mbalimbali katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki. Tunapozungumza sasa mashauri 13 ya Watanzania wanaodai kuwa haki zao za binadamu zimevunjwa yako katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki. Nchi nyingine zimehakikisha raia wao mashtaka hayo hayaendi na sina haja ya kuzitaja kwa sababu zinafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunavyozungumza sana yako zaidi ya mashauri ya Kikatiba 40 katika Mahakama Kuu ya Tanzania; mashauri matano ya Kikatiba katika Mahakama ya Rufaa, hayo yote yanaonyesha kwamba tunao mfumo na taasisi zinazowawezesha Watanzania kusimamia haki zao. Ndiyo maana hivi karibuni Mahakamu Kuu, katika kesi ya Emmanuel Simphorian Masawe imetoa mwongozo wa jinsi ambavyo Mkurugenzi wa Mashtaka atatumia mamlaka aliyonayo kuhusu suala zima la kutoa *certificate* ya kuzua *bail* inapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tunajadili suala la haki za binadamu hapa nchini bila kuangalia maamuzi ya Mahakama. Labda hilo nisiwalaumu Watanzania, nijilaumu mimi pamoja na Maprofesa na wasomi wengine ambao tumeshindwa kuandika *commentary* ya maamuzi ya Mahakama ya Rufaa ambayo yametoa tafsiri ya vifungu mbalimbali vya Katiba ndiyo maana kila mtu amekuwa anasoma Katiba ilivyo bila kwenda kwenye maamuzi mbalimbali ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza sana Mahakama, inafanya kazi kubwa. Kwa kweli Mahakama ya Tanzania iko mbali sana. Wote ambao walisikiliza hotuba ya Jaji Mkuu siku ya Jumatano, hotuba ya kurasa 40 na niko tayari, hotuba hiyo kuichapa na

kuwagawia Wabunge wote waone mambo aliyoyasema kwa ufasaha na umakini Profesa Ibrahim Hamis Juma. Jaji Mkuu wa mfano, Jaji Mkuu mweledi, Jaji Mkuu mcha Mungu alieleza wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Law Day*, bahati mbaya sana Watanzania mambo madogo tunayafanya kuwa makubwa. Mimi naona aibu kubwa sana kuona Wanasheria nchi hii wanajadili suala la Mkuu wa Mkoa kupita kwenye *red carpet* wanasahau ile ilikuwa ni siku ya kuzindua Mwaka wa Mahakama na anayezindua Mwaka wa Mahakama ni *Head of State* na anayemwakilisha *Head of State* ngazi ya Mkoa na Wilaya ni *RC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda muone Mwaka wa Mahakama unavyozinduliwa Uingereza, unazinduliwa na Askofu Mkuu wa Canterbury, kwa nini? Ni kwa sababu kwa Waingereza Askofu Mkuu wa Canterbury kwa *protocol* ni namba mbili na hakuna anayeuliza kwa sababu ni taratibu yao. *Head of State* (Malkia) hawezi kuhudhuria ile sherehe, anayehudhuria ni *number two*, ni *Archbishop of Canterbury*. Kwa hiyo, hii ni *Head of State* na wala tusiikuze kwa sababu ni kuzindua Mwaka wa Mahakama. Nawaomba Wanasheria Tanzania wazingatie mambo muhimu yaliyozungumzwa na Jaji Mkuu, tuache nani kapita kwenye *red carpet*, *yellow carpet* au *green carpet*, hayo siyo mambo ya msingi kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Mahakama. Mahakama imefanya kazi kubwa sana katika kupunguza mlundikano wa mashauri. Kwa Mahakama ya Mwanzo imejipa muda kwamba ndani ya miezi sita mashauri yawe yamekwisha na mpaka sasa mashauri ambayo yamevuka miezi sita ni 16 tu. Mahakama ya Wilaya imejipa mwaka mmoja kuwa imemaliza mashauri na mpaka sasa kesi ambazo zimezidi mwaka mmoja ni 837. Katika Mahakama Kuu ni miaka miwili na kesi ambazo zimevuka miaka miwili ni 1,860. Katika Mahakama ya Rufani ni miaka miwili na kwa kesi ambazo zimevuka miaka miwili ni 729.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuiongezea Mahakama idadi ya wafanyakazi mwaka jana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia mamlaka aliyonayo ndani ya Katiba akishauriwa na *Judicial Service Commission* aliteua Majaji wawili (2) wa Mahakama ya Rufaa na Majaji kumi (10) wa Mahakama Kuu. Mwaka huu kwa kutumia mamlaka yake hayo hayo, akishauriwa na *Judicial Service Commission* amechagua Majaji sita (6) wa Mahakama wa Rufaa na katika Majaji hao wanne (4) ni wanawake na wawili (2) ni wanaume, namba kubwa sana. Kwa hiyo, pia akina mama ndani ya nchi hii mjipongeze na kujisifia kwamba mwaka huu mmeweza kutoa Majaji wa Rufaa wanne (4). Hayo ndiyo mambo ya kujadili badala ya kujadili mambo madogomadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais ameteua Majaji wa Mahakama Kuu kumi na tano (15). Kwa mara ya kwanza katika Majaji hawa kumi na tano (15), Mheshimiwa Rais ameweza kuteua Mahakimu wa Kawaida (*Resident Magistrate*) mmoja (1) kutoka Bukoba, kijana mdogo na mwingine kutoka Shinyanga aliyekuwa Hakimu wa Shinyanga ili kuonyesha kwamba Ujaji unaendana pia na weledi lakini pia ujasiri na kusimamia sheria na haki. Kwa hiyo, niipongeze sana Mahakama kwa kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Mahakama zinazotembea (*Mobile Court*) tulisema hata wakati ule tulipondoa hiyo hoja katika Bunge, tuliondoa hoja hiyo kwa sababu Jaji Mkuu ana mamlaka ya kuzianzisha Mahakama hizo bila kuleta sheria Bungeni. Ametumia mamlaka aliyonayo, Mahakama hizo amezianzisha na zitaendelea kufanya kazi. Tayari magari mawili yamefika na yataanza kufanya kazi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Dar es Salaam Mahakama hizo zinazotembea itakuwa Bunju Wilaya ya Ilala, Chanika Wilaya ya Temeke, Buza na Kibamba Wilaya ya Ubungo. Kwa Mkoa wa Mwanza ambao pia una mashauri mengi, gari linakwenda Mwanza na litatoa huduma hizo

kwenye Wilaya ya Ilemela huko Buhongwa na Igoma na Wilaya ya Nyamagana kule Buswelu. Baadaye magari yatakapoongezeka huduma zitasambaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyomsikia wenyewe Mheshimiwa Rais ametoa maagizo linunuliwe gari La *Mobile Court* na gari hilo liwe na Mahakimu wanawake kwa ajili ya kushughulikia kesi za mirathi za wanawake. Tutatekeleza maagizo hayo ili tuhakishe tuna Mahakama inayotembea kwa ajili ya kushughulikia kesi za mirathi ya wajane ambazo Mheshimiwa Rais amesema kesi zao zinachukua muda na wanaonewa. Kwa hiyo, Mahakama hizo zinazotembea zitaendelea kufanya kazi na hakuna mahali tulipovunja sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa watu wayajue magari haya. Ndani ya magari hayo kuna huduma nyingi, kuna televisheni kwa ajili ya kurekodi ushahidi, kuna *computer*, *printer* na lifti ya kuwainua watu wenye ulemavu, kuingia na kushuka. Kwa hiyo, hiyo bei ya gari siyo gari tu ni pamoja na *facilities* nyingine ambazo ziko ndani ya gari hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza sana Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ni Ofisi ambayo imeanza hivi karibuni lakini imefanya kazi kubwa sana. Imesimamia kesi nyingi za mashauri ya usuluhishi na mpaka sasa inasimamia mashauri 42 ya usuluhishi kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha jambo hilo pia tutaanzisha kitu ambacho kinaitwa Haki Mtandao. Hivi karibuni Mahakama imeshaweka mtandao siyo lazima wafungwa au mahabusu watoke gerezani kwenda Mahakamani. Mambo ya kuahirisha kesi yatafanywa hukohuko mfungwa akiwa gerezani na Hakimu akiwa Mahakamani, kwa kutumia *video link* kesi hiyo itamalizwa na itaondoa tatizo la kubeba mahabusu kwa magari. Ni kweli kabisa mahabusu wako wengi na Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa tunapunguza idadi

ya mahabusu hasa wale wa kesi ndogo ndogo kwa kuwapeleka katika *community service*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo limezungumzwa hapa na napenda nilizungumzie pia, nalo ni suala la haki ya tendo la ndoa kwa wafungwa. Napenda kusema kwamba tendo la ndoa si haki ya msingi ni jambo la hiari, ndiyo maana wako Waseja na Watawa wa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusilifanye suala la tendo la ndoa kuwa suala la msingi. Ni moja ya haki ambayo mfungwa anaweza kunyimwa kwa sababu siyo haki ya msingi. Hanyimwi chakula, mavazi na maji kwa sababu ni haki ya msingi lakini tendo la ndoa ni la hiari. Wako ambao ni rijali lakini kwa hiari wameamua wasilifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si vyema tukaanza kujiingiza katika mambo hayo ambayo kwa kawaida si utamaduni wa Waafrika kuanza kuzungumzia mambo ya tendo la ndoa. Ndiyo maana sisi ni mambo binafsi mno. Sasa tusianze kuiga mila nyingine, hata huko kwenyewe tendo la ndoa, kwa sisi tunaofahamu huko halifanywi gerezani, wale wafungwa huwa wanaruhusiwa kwenda kutembelea familia zao. Wenzetu kule ukihukumiwa mwisho wa mwaka huendi gerezani, unaripoti gerezani tarehe 2 Januari, ni utaratibu wao. Kwa hiyo, wale wenye umuhimu wa kufanya hivyo wanaruhusiwa kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kabisa Bunge hili lisichukue muda mrefu katika jambo hili. Suala hili liliwahi kuwa ni moja ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti na Tume ya Kurekebisha Sheria na likaonekana kwa nchi yetu halifai. Nchi moja ya jirani walitaka kufanya hivyo walishindwa kwa sababu ni suala la faragha, sasa kila mtu anajua mnaingia, hata uwezo unapotea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tumelipokea tutalifanyia kazi ni kuwachanganya wafungwa wenye umri tofauti, vijana na watu wazima. Hili ni suala la

msingi sana na tutalifanyia kazi. Tutazimbelea Mahakama na kwa kweli tutahakikisha kwamba wafungwa hawa wanatenganishwa, hili ni moja ya jambo ambalo tunalipokea. Tayari Tume ya Kurekebisha Sheria imetoa ripoti inayoitwa *Review of Police and Prisons Legislation*, tutaona nini kifanyike ili kuhakikisha kwamba jambo hili linazingatiwa ili tutenganishe wafungwa kwa rika na umri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la matumizi ya Kiswahili katika utungaji wa sheria, ni kweli kabisa wakati umefika wa kuanza kuzitunga sheria zetu kwa Kiswahili. Hata hivyo, napenda nitoe indhari siyo tahadhari maana ipo tofauti kati ya tahadhari na indhari. Ni kwamba hata tutakapoanza kuandika sheria nyingi kwa Kiswahili na sasa tayari tunaandika Miswada mingi kwa Kiswahili lakini someni Miswada ya Kiswahili si Kiswahili cha mtaani, ni Kiswahili chenye istilahi mbalimbali za kisheria ambazo ina maana baada ya muda itabidi tena watu wajifunze na wazielewe istilahi hizo na nyingine zinaweza kuwa zinakera masikioni kwa sababu hazijazoeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia Sheria ya Kiswahili ya Usimamizi wa Mazingira neno *monitoring* ni kupelemba lakini upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania neno kupelemba lina maana tofauti kabisa na ukienda huko usilitumie maana yake ni kumtongoza mwanamke. Kwa hiyo, hata huko pia tutakapoanza kutumia Kiswahili tujue kutakuwa na istilahi ambazo pia itabidi watu wazifahamu lakini ni kweli kabisa ni muhimu kuanza kutunga sheria zetu nyingi kwa Kiswahili badala ya Kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchelewashaji wa kesi, hili tumeshaliwekea mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapunguza ucheleweshaji wa kesi. Ucheleweshaji huo wa kesi unachangiwa na uchunguzi na sasa tunafanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa uchunguzi wa masuala mbalimbali ya kesi unamalizika kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto, zipo kesi nyingine zimechukua muda mrefu kwa sababu uchunguzi unahusisha kupata ushahidi kutoka nje ya nchi. Nashukuru kwa kuanza kutumia huu mtindo wa *e-Justice* hivi karibuni kuna kesi ambayo imesikilizwa ambapo shahidi alikuwa Ufaransa na kesi imefanyika Tanzania na shahidi aliweza kutoa ushahidi kutoka Ufaransa bila yeye kulazimika kuja. Kwa hiyo, ni moja ya maeneo ambayo tutayafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuongezewa idadi ya Majaji na Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu napenda kusema kwamba tunaishukuru sana Kamati kwa mambo mengi ambayo imeyaorodhesha. Kwa Watanzania kwa ujumla, napenda sana tujue hatuna nchi nyingine nje ya Tanzania na labda tunaichezea kwa sababu hatujaenda kuona nchi nyingine ambazo zimechezea amani yake zimeishia wapi. Siyo lugha nzuri na wala haipendezi kutaka kuleta mabadiliko kwa kuanza na vitisho, nchi hii itaendelea kuwepo na itaendelea kuwa na amani kama sisi wenyewe tutaamua kuwa na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima Watanzania tuwe na staha, tumefika mahali sasa tumeanza kukosa staha. Baadhi ya lugha tunazosisikia ndani na nje ya nchi haziendani kabisa na Utanzania wetu, utanzania ni pamoja na kustahi/kuyaheshimu mamlaka. Mkuu wa nchi ni taswira ya nchi hii, mkuu wa nchi anawakilisha nchi hii, kwa hiyo, siyo vyema tunapoanza kumbeza, kumzalilisha na kumdharau na tukadhani kwamba hiyo ndiyo demokrasia. Ni lazima tutofautishe kati ya demokrasia na *laxity*, *there is a big difference between democracy and laxity*. Tulizoea *laxity* na wakati wa *laxity* umekwisha. Kwa hiyo, demokrasia ni pamoja na kujua na mipaka yako na heshima hasa kuheshimu mamlaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uvumilivu mkubwa sana alionao. Amevumilia upumbavu, upuuzi na ujinga mwingi lakini tusiendeleo kufanya hivyo kwa sababu sisi wengine

ambao tumepewa kazi ya kuhakikisha heshima hiyo inalindwa tutatekeleza wajibu wetu na tutatekeleza bila tashwishwi hata kama baadaye watu watasema tumebadilika kwa sababu...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Dakika moja Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, *mobile court*, kutokana na msongamano ulivyo na tulishawahi kushauri kwa nini Mahakama nazo haziendi jela au mahabusu na kupunguza msongamano?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hilo limechukuliwa na moja ya hatua ambazo tumekubaliana, tunaanza katika awamu hii ni kuanza kutemebelea Magereza. Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Mahakimu wakitembelea Magereza wana haki ya kutoa maamuzi ya kuwaachia baadhi ya wafungwa pale ambapo Mkurugenzi wa Mashtaka ameridhika kwamba watu hao kwa kweli kesi zao ni ndogo na tayari amekwishafanya hivyo. Katika hotuba ya bajeti tutaeleza idadi ya mahabusu walioachiwa baada ya ziara za *DPP* kuanza katika Magereza mbalimbali.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, dakika 15 lakini naona Serikali imekujibia kila kitu.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitambue michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Idadi ya Wabunge waliochangia ni 18 na kwa nafuu ya muda

sitawataja majina. Pia nitambue michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri wote na katika baadhi ya hoja ambazo tayari Waheshimiwa Mawaziri wameshajibu, sitakwenda huko tena kwa sababu ninaamini kama ni ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge basi utakuwa umechukuliwa na Waheshimiwa Mawaziri na pengine wataufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo limezungumzwa kwa kina pengine napenda kulisitiza sana ni kuomba Kiti chako kwamba hizi semina kwa Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana ili kila mmoja wetu aweze kutambua mipaka ya kuchangia hususan inapohusu mihimili hii mitatu inayounda Serikali. Kwa sababu ipo michango mingi ambayo imezungumzia kuhusu Mahakama na inatambulika kabisa kwamba Mahakimu au Majaji wana kinga na malalamiko yoyote dhidi ya Hakimu/Jaji mamlaka yake ya juu ni kukatia rufaa kutokana na maamuzi ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge walitambue hilo na pengine tutumie fursa ya uelewa wetu kuwaambia wananchi wetu umuhimu wa kuheshimu mihimili hii yote mitatu lakini hususan kabisa mhimili wa Mahakama ambao ndiyo umepewa mamlaka yote ya utoaji haki kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge watambue kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Jaji Mkuu lakini pia watendaji wa Mahakama wamefanya kazi nzuri sana kuboresha mifumo ya utoaji haki hapa nchini. Natambua hilo kwa kuwa mimi ni miongoni mwa vijana ambao tumekulia kule, najua hali ilivyokuwa huko nyuma na hali ilivyo sasa kwa kweli Mahakama imefanya kazi kubwa sana, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo yamezungumzwa kuhusu mamlaka ya utoaji haki na masuala ya dhamana. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwamba ni vyema wakajikita kabisa

katika kusoma vizuri Ibara ya 26 ya Katiba ambayo inamtaka kila Mtanzania kutii Katiba na sheria zetu za nchi ambazo zinatuoongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukaitambua mipaka ya utoaji haki na ni vizuri tukajikita kutafuta wataalam watusaidie katika maeneo ambapo tunaamini kabisa hatukutendewa haki. Ukisoma vizuri Katiba na sheria za nchi yetu zimetoa maelekezo mazuri kabisa ni namna gani ambapo mtu anapaswa kukata rufaa lakini ni namna gani ambapo Mahakama inapaswa kutoa dhamana na masuala mengine yote ambayo yamezungumzwa kwa kina hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyosema Wabunge 18 ndiyo waliozungumza mambo mbalimbali na kwa kuwa tayari mengine yameshajibiwa na Waheshimiwa Mawaziri na tunaamini mengine yamechukuliwa vizuri na Waheshimiwa Mawaziri, naomba nijikite tu kwenye baadhi ya masuala machache ya muhimu ili kuongeza msisitizo katika maeneo hayo. Kwa ujumla utendaji wa Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati yangu ya Katiba na Sheria ni wa kuridhisha sana ukiacha baadhi ya changamoto ambazo tayari Serikali imeshaanza kuzitafutia ufumbuzi. Hivyo, Kamati inaipongeza na kuishukuru Serikali kwa ushauri wao mzuri uliofanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Maeneo ambayo Kamati imebaini kuwa na changamoto, imetoa mapendekezo yake kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi kama yanavyoainishwa katika Sehemu ya Tatu ya taarifa ya Kamati kuanzia ukurasa wa 39 mpaka 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo hayo yaliyobainishwa na kutolewa mapendekezo ni pamoja na Serikali iongeze usimamizi na uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu nchini na itangaze rasmi Wajumbe wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu. Jambo hili tayari Naibu Waziri wa Vijana ameshalizingumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine mwingine ni Serikali ianzishe pia Mfuko wa Masuala ya

Wenye Ulemavu na kuanzisha fungu dogo la kibajeti kwa kulitengea fedha kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020. Ushauri huu pia umezingatia maoni ya wadau wengi wa kundi hili muhimu katika jamii ambao wamechangia yetu kupitia vikao mbalimbali vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine ni Serikali pia iongeze usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa lengo la kuimarisha SACCOS zilizopo na kudhibiti SACCOS hewa za vijana ambazo hukopeshwa na kupokea fedha za Serikali. Pia Ofisi ya Waziri Mkuu iwe na ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ndiyo wenye dhamana ya Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila Halmashauri inawajibika na kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana na kusimamia marejesho yake kwa wakati. Maoni na mapendekezo ya Kamati ni kama ambavyo imefafanuliwa katika taarifa yangu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kukubali maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii ili yawe maazimio ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, ahsante Mwenyekiti. Sasa nitawahoji kuhusu Bunge kupokea na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 pamoja na maoni na mapendekezo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda, hongereni sana Kamati kwa kazi nzuri. Sasa hizi ni kumbukumbu rasmi za Kamati kwenye Bunge na ni maagizo rasmi kutoka Bungeni kwenda Serikalini. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuhitimisha hoja yangu. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati hii lakini baadhi yao hasa wale Wajumbe wa Kamati yenyewe; Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Salome Makamba na wameelezea vizuri. Yupo Mheshimiwa Mnzava sikujua ni mwanasheria huyu, alielezea vizuri sana, namshukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Kolimba na Mheshimiwa Mukasa, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifanye sahihisho moja, limetumika neno Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo, hii siyo Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Tuelewane, hizi ni sheria za nchi wala siyo sheria ndogo ndogo, ni sheria kabisa zinazotokana na mamlaka ya Kikatiba ambapo Bunge linapoona inafaa kukasimu, linakasimu madaraka yake. Kupitia Kamati hii ndiyo linachungulia kudhibiti yale ambayo limekasimu kuona kama yamekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumesema sheria hizi zinapotungwa na mamlaka inayokasimiwa zinaanza kutumika kabla ya kuwasilishwa humu Bungeni. Ndiyo maana busara ya Spika kwamba tuwahishe Kamati hii iwe inatoa taarifa zake mapema ili kusaidia kutoonea wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunakoelekea bado nashauri ni vyema tukaangalia utaratibu huu wa Sheria Ndogo kuanza kutumika zinapochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, hiyo ndiyo hoja na inazungumzika. Ndani ya nchi za Jumuiya ya Madola baadhi ya nchi zimebadilisha utaratibu ambao Tanzania tunautumia lakini nasema kwa sasa huo ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nichukue muda mrefu, matokeo ya uchambuzi wa kazi tuliyofanya kwa mwaka mzima mnayaona kwenye taarifa pamoja na lile jedwali. Tumeelezea changamoto ambazo zipo, ni kama tano, tunaiachia Serikali ione namna gani tunavyoweza kuzipunguza. Zipo zile za wazi kabisa, hii ya ku-copy tu Sheria Ndogo za Halmashauri fulani bila hata kuzamia, nadhani hapa ni suala la kutokuwa makini tu kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja, Ofisi ya Waziri Mkuu hasa kupitia Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama amekuwa mtu wa karibu sana katika kuunganisha shughuli za Kamati na Serikali, yeye kama daraja na wanayaona mapema na hasa zile ambazo zinahusu Ofisi ya TAMISEMI wanawapelekea haraka sana ili wafanye masahihisho na hatimaye kuzichapisha tena na kuletwa humu Bungeni. Tunamshukuru sana kwa kazi hiyo na tutaendelea kushirikiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hii changamoto kubwa ya uandishi wa sheria, uchache wa wataalam hawa, hili sio la Tanzania tu. Nimekulia kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu naelewa kazi nzito walizonazo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa upande wa Idara ya Uandishi. Kazi hii siyo ya kila mwanasheria, kazi hii unahitaji wanasheria wanaoipenda ile kazi, wenye weledi, wanaoifahamu sheria katika mapana yake sio katika eneo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapowapata wanasheria kama hawa, changamoto kubwa ipo namna ya kuwatunza wabaki Serikalini au kwenye taasisi za Serikali. Ni utaalam wa kipekee huu, tunao wachache lakini

naishauri Serikali iendelee kuwekeza kwenye eneo hili, bado hatujafanya vizuri. Tulifanya vizuri mpaka miaka ya 1980 sasa tumeanza kuwapoteza hawa ambao tulikuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu, TAMISEMI wajitahidi kwa kadri inavyoweza kuwanoa wanasheria walionao. Mimi najua baadhi yao wanaweza wakapata mafunzo wakaongeza weledi wao wa namna ya kuzichambua na kuziandaa hizi sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ndilo linakasimu mamlaka yake kwa mamlaka mbalimbali, nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge shughuli ya kukasimu itaendelea tu kwa sababu Bunge haliwezi likafanya kazi zote na kutunga sheria *aspect* zote zikawa kwenye sheria. Tunapokubali kama Bunge kukasimu nawaombeni sana tuwe makini kwamba ile misingi ambayo tunakasimu ikatungiwe kanuni lazima tuiweke katika lugha ambayo siyo pana sana na hii ndiyo kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Ofisi ya Bunge, Katibu wa Bunge katika kuwajengea uwezo Wabunge wa kuchambua Miswada, naomba hili liendelee. Serikali nayo ione uwezekano huu wa kuwajengea uwezo Wabunge wa kuchambua Miswada, tusiachie wageni kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kamati inachambua makaratasi na yanashuka kama mvua. Siyo kazi nyepesi na inafanywa na watu ambao siyo wanasheria, mimi nawapongeza sana lakini nazidi kuiomba Ofisi ya Katibu wa Bunge waangalieni kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Bunge kupokea na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2018 pamoja na maoni na mapendekezo.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo
kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018
Ilipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda, hongera sana Mtemi Chenge, hongera sana Mheshimiwa Mchengerwa, Mawaziri mmejibu majibu mazuri sana, ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kabudi, niwashukuru *Chief Whip* wa pande zote mbili na niwashukuru Wabunge kwa michango yenu.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi siku ya Jumamosi.

*(Saa 12.18 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,
Tarehe 9 Februari, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*